
Nipashe
Alhamisi Oktoba 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581097
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

SUPA JACKPOT
TZS. 1,039,594,915
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Gharama** matibabu matumizi ya nishati chafu yazidi kupaa

UKURASA 3



**BURNA BOY AJIMWAGA NA BEYONCE**

UKURASA 27




# Watanzania kufikiwa na bima ya afya hivi

UKURASA 2


TANZANIA REVENUE AUTHORITY
CERTIFICATE OF REGISTRATION FOR
TAXPAYER IDENTIFICATION NUMBER (TIN)
THIS IS TO CERTIFY THAT

**Vitambulisho vya uraia vinavyotolewa na NIDA na leseni za udereva kutumika katika usajili wa wanachama kufanikisha bima ya afya kwa wote.**





**Laini za simu zilizosajiliwa pia zitatumika kuwafikia wananchi mchakato wa bima ya afya.**

## LAAC yatimua kikaoni vigogo H/shauri Mlele

UKURASA 3

## Wafanyakazi 8 BoT kortini madai ya kuharibu noti bil. 4.6/-

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAWAHI SUDAN UK.32

The Guardian
Nipashe
KUMBUKIZI YA HAYATI MWALIMU NYERERE



MIAKA 23
1999-2022

Kampuni ya uchapishaji ya The Guardian Ltd kupitia magazeti yake, 'The Guardian' na 'Nipashe' itatoa Toleo Maalum Oktoba 14, 2022 ya kumbukizi ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere (1922-1999).

Kupata nafasi kwa matangazo, wasiliana nasi kwa namba 0782253676, 0745 700 710

Wahi kwa kuweka ujumbe wako leo!

# Watanzania kufikiwa bima ya afya hivi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeeleza namna Watanzania watakavyofikiwa na Bima ya Afya kwa Wote kwa kufunganamanisha upatikanaji wa baadhi ya huduma na umiliki wa bima ya afya ili kuhakikisha hakuna atakayeachwa nyuma.

Njia hizo ni hati za kusafiria na visa kwa wageni, bima za vyombo vya moto (magari, bajaji na pikipiki), utambulisho wa mlipakodi, laini za simu, uanachama katika vyama vya ushirika, wanafunzi kujiandikisha kidato cha tano, sita na vyuoni na kitambulisho cha uraia.

Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa Maandalizi ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Janeth Kibambo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa habari katika mkutano wa kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya afya bila usumbufu ndiyo maana vimetumika viambatanisho mbalimbali ili kuwapata kwa urahisi kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

Pia alisema viwango vya uchangiaji vinavyopendekezwa vimezingatia gharama za matibabu, uwezo wa wananchi na uzoefu katika soko la bima ya afya kwa Mifuko ya Bima ya Afya kwa Umma pamoja na kampuni binafsi za bima.

Mjumbe huyo alisema usajili wa wanachama utafanyika kwa utaratibu wa kaya kwa baba na mama, wategemezi wanne ambao wanaweza kuwa mzazi, watoto wa kuzaliwa, kuasili au wa kambo, ndugu wa damu wasiozidi umri wa miaka 21.

"Iwapo Sheria ya Bima ya Afya itapita haitatekelezwa kwa kukamata watu na kuwashitaki katika vyombo vya sheria kama watakataa. Tutaendelea kuwaelimisha na kufungamanisha huduma mbalimbali," alibainisha.

Alisema wananchi wasiwe na wasiwasi kwa kuwa kupitia utaratibu wa Bima ya Afya kwa Wote, huduma za afya zitaboreshwa kwa kuhakikisha dawa zinapatikana na kuboresha huduma kwa kuongeza wataalamu na watoa huduma katika vituo vyote vya afya nchini.

"Tunafahamu kuwa kulikuwa na tatizo la baadhi ya wananchi waliojiunga na bima ya afya, ikiwemo ya CHF. Wakienda kwenye vituo vya afya hawapati huduma au wanakosa dawa. Kupitia utaratibu huu, serikali imejipanga dawa zitapatikana za kutosha, wahudumu wetu wanaotoa huduma za afya nao tunaendelea kuwajengea misingi ili kutoa huduma bora," alisema.

"Mwananchi ukishajiunga na bima hii ya afya kwa wote unapata uhakika wa matibabu wakati wowote unapougua hata kama huna fedha. Pia utapata uhakika wa huduma kuanzia ngazi ya zahanati kwa kiwango hicho hicho ulichojiunga nacho," alisema.

Pia alisema sheria hiyo itapitishwa na bunge, hakutakuwa na makundi ya mafao ya bima na kwamba mtu akishajiunga, kila kilichokuwa kwenye kitita cha msingi atakipata.

"Tupo katika hatua ya mjadala na kupokea maoni, ila viwango hivi vya uchangiaji huwa vinagawiwa kwa kuzingatia gharama halisi ya tiba na mahitaji halisi ya wananchi kwa maana ya afya.

"Kwa kuzingatia hesabu na ili hospitali na vituo vya afya vitoe huduma, tumependekeza Sh. 340,000 kutolewa kwa kila kaya na kwa mtu mmoja ambaye hana familia atatakiwa kuchangia Sh. 84,000. Hii ni kwa kuanzia lakini nasisitiza bado tupo kwenye majadiliano," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa mwananchi ambaye hatakuwa na uwezo wa kuchangia viwango hivyo kwa mkupuo, utaratibu utawekwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ili kundi hilo lichangie na kupata fursa ya bima kulingana na uwezo wa kipato chao.

Aliongeza kuwa wasikuwa na familia watachangia Sh. 84,000 kwa mtu mmoja mmoja kwa mwaka ambayo ni sawa na wastani wa Sh. 7,000 kwa mwezi.

Alibainisha kuwa kwa wananchi watakaotambuliwa kutokuwa na uwezo wataendelea kupatiwa huduma kwa utaratibu utakaowekwa na serikali kwa kila mtu kuwa na kadi yake ya Bima ya Afya.

Iwapo mambo yatakwenda kama yalivyopangwa, alisema sheria hiyo itaanza kutumika Julai 1, 2023 na kwamba wananchi na wadau watatwa kutoa maoni yao. Muswada wa sheria hiyo ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge Septemba 27, mwaka huu.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akizungumza na Spika wa Baraza la Wawakilishi la Jamhuri ya Indonesia, Dk. Puan Maharani, walipokutana katika Mkutano wa 145 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) unaoendelea jijini Kigali, nchini Rwanda jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wafanyakazi BoT kortini madai ya kuharibu noti za bilioni 4.6/-

**Na Grace Gurisha**

WAFANYAKAZI wanane wa Benki Kuu ya Tanzania na wenzao watano, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa madai ya kuharibu noti.

Kesi hiyo ambayo jana ilitajwa kwa mara nyingine baada ya hivi karibuni kufikishwa mahakamani hapo, inatarajiwa kutajwa Novemba 9, mwaka huu.

Wafanyakazi hao ni Mariagoreth Kunzugala, Henry Mbowe, Asha Sekiboko, Cecilia Mpande, Agripina Komba, Zubeda Mjewa, Khadija Kassunsumo na Mwanaheri Omary, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Wakati kesi hiyo ikitajwa jana, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate kuwa upelelezi bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo.

Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 9 kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Mbali na wafanyakazi hao washtakiwa wengine ni ambao si watumishi wa BoT ni Aristides Genand, Musa Chengula, Zaituni Chihipo na Respicius Rutabilwa.

Washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa mashtaka matano ambayo ni kuongoza genge la uhalifu, kufanya uhalifu wa kupanga, kuharibu noti, kujipatia faida kwa udanganyifu na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 4.6.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa kati ya Januari, 2017 hadi Septemba 30, 2019 washtakiwa wakiwa watumishi wa BoT, kwa kuvunja majukumu yao ya kazi waliwezesha utendekaji wa kosa la kuongoza genge la uhalifu.

Pia inadaiwa Genand, Chengula, Chihipo na Rutabilwa wakiwa si watumishi wa BoT, kwa kushirikiana na watumishi hao wa BoT, kwa makusudi waliwezesha kutendeka kwa uhalifu wa kupanga.

Katika shtaka la tatu, washtakiwa wote bila ya kuwa na kibali na kutokuwa wazalendo, waliharibu kwa kuzikatakata noti 460,000 zenye thamani ya Sh. 10,000 kila moja ambazo zote gharama yake ni Sh. bilioni 4.6.

Katika shtaka la nne, siku na maeneo hayo, kwa mawasilisho ya kilaghai, kwa kujua na kwa mpango wa kitapeli, washtakiwa wote wanadaiwa kujipatia faida ya Sh. bilioni 1.5 kutoka BoT baada ya kuwasilisha noti hizo.

Katika shtaka la tano, washtakiwa wote wanadaiwa kuisababishia BoT hasara ya Sh. bilioni 4.6.

# Serikali yafafanua masharti usajili NGO

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imesema ililazimika kufanya maboresho katika kanuni za usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) ili kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji katika uendeshaji wa mashirika hayo.

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao, alitoa kauli hiyo jijini hapo jana wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC 2022), akijibu hoja ya Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Wakili Francis Kiwanga.

Katika mkutano huo, Wakili Kiwanga, mbali na mambo mengine, alisema kuna haja serikali kufanya alichokiita 'kupunguza ukali wa masharti' katika usajili na utendaji wa asasi za kiraia, yakiwamo ya kutakiwa kuripoti serikalini kila wanapopata ufadhili wa mradi unaozidi Sh. milioni 20.

Akitoa ufafanuzi kuhusu hoja hiyo, Vickness alisema serikali imelazimika kuweka masharti hayo ili kuhakikisha mashirika hayo yanakuwa na uwajibikaji kiutendaji.

Mayao aliyahakikishia mashirika yasiyo ya kiserikali kwamba serikali imefungua milango ikitambua mashirika hayo ni njia sahihi ya kuifikia jamii kwa haraka kuihamisha kushiriki shughuli za serikali.

"Serikali imeona umuhimu wa mashirika haya, inatambua yapo karibu zaidi na wananchi na hivyo ni daraja kutoa elimu kwa wananchi na kuwahamasisha kushiriki katika utekelezaji wa shughuli za serikali," alisema.



Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Kilian Luwena, akidhibiti upotevu wa maji katika bomba la inchi 10 jirani na Kanisa la Efatha, Kata ya Saranga, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# LAAC yawatimua vigogo h'shauri Mlele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imewatimua vigogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kwenye kikao baada ya kutoridhika na majibu yaliyotolewa kwenye hoja mbalimbali za ukaguzi.

Kutokana na hali hiyo, LAAC imeagiza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufuatilia na kuchukua hatua katika dosari zilizobainika kabla ya Desemba mwaka huu.



Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Mabula (pichani), aliyasema hayo jana jijini hapa baada ya kamati hiyo kushindwa kuendelea na mahojiano na halmashauri hiyo kutokana na hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) za mwaka 2020/21.

Mabula alisema kamati hiyo imeshindwa kuendelea na mahojiano na Halmashauri hiyo na wanaiondoa kwenye meza ya mahojiano.

Alitaja dosari hizo kuwa ni kubainika kuwepo matumizi ya fedha mbichi Sh. milioni 441 ambapo matumizi hayakuonekana kwenye mifumo ya kielektroniki ya matumizi ya fedha za umma.

"Hili ni kosa kubwa na wewe mkurugenzi umekiri kwa hiyo sio jambo ambalo linapaswa kuendelea," alisema.

Pia alisema kuna udhaifu mkubwa kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo kamati imebaini Halmashauri iliweka makisio madogo.

"Unawezaje kukusanya mapato asilimia 185 tuseme mli 'underestimate' malengo ya ukusanyaji ndiyo maana mmefika huko, kumbe mngejiwekea malengo mazuri mngefanya vizuri zaidi na kuwa halmashauri bora,"alisema.

Kadhalika, alisema hawachangii kabisa kikamilifu kwenye miradi ya maendeleo.

"Kuna udhaifu pia kwenye kudai marejesho ya mikopo ya vikundi, tunaona kuna Sh. milioni 127 hazijakusanywa zipo kwenye vikundi, tafsiri yake ni uzembe, pia kuna madai ya watumishi zaidi ya Sh. bilioni 1.1 kila mara tumekuwa tukisema hili, na watumishi wanapokosa kulipwa madai yao usitegemee ufanisi,"alisema.

Mabula alisema kuna mashine 13 za POS zilikuwa zimezimwa hazisomani kati ya siku 81 hadi 1220 sawa na miaka mitatu.

"Tunaona kamati suala hili sio zuri na kungekuwa na majibu naamini lisingefika kwenye kamati hii,"alisema.

Hata hivyo, Makamu Mwenyekiti huyo alisema Sh. milioni 174.3 zilihamishwa kutoka kwenye mapato ya ndani na kupelekwa kwenye akaunti ya amana kwa namna yenye kutia shaka.

"Michanganuo ya mapato na matumizi ya miradi 18, hayaakisi uhalisia wa fedha zilizotolewa na kutumika,"alisema.

# Madhara matumizi nishati chafu yazidi kupaa

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema matumizi ya nishati chafu yamekuwa mzigo kwa matibabu wa magonjwa ya kupumua na kwamba zaidi ya Watanzania 33,000 hufariki kila mwaka kutokana na matumizi hayo hususan kuni.

Kutokana na tatizo hilo, amesema serikali imejipanga kuwafikia asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi miaka 10 ijayo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, jana kuhusu kongamano la nishati safi ya kupikia litakalofanyika Novemba 1 hadi 2, mwaka huu, alisema wataalamu watatoa suluhisho la changamoto za nishati chafu zilizoko kwenye jamii.

"Athari ya kwanza ni afya si tu kwa Watanzania hata katika mfumo wa utoaji wa huduma za afya hapa nchini kwa sababu asilimia 70 ya magonjwa nchini ni magonjwa yasiyoambukizwa, yakiwamo ya mfumo wa upumuaji," alisema.

Waziri Makamba alisema vituo vya afya vinaelemewa na mzigo mkubwa wa utoaji wa huduma za afya kutokana na namna mojawapo ya kupika.

Aidha, alisema asilimia 72 ya nishati yote ya nchini inatumika nyumbani na asilimia nane ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia isiyotoa moshi wa kuangamiza afya zao. Pia alisema asilimia 63.5 ya nishati yote inayotumika nyumbani ni kuni na asilimia 26.2 ni mkaa hivyo ni sawa na asilimia 90.

Alisema kongamano hilo litakuwa na malengo matano ambayo ni hali halisi ya sasa katika matumizi ya nishati ya kupika, kupata uelewa wa pamoja kwa wadau wote kuhusiana na changamoto iliyopo.

"Tutabadilishana uzoefu, ujuzi na fursa zitakazowezekana kuondokana na changamoto za upatikanaji wa nishati safi ya kupika nchini kwani kuna nchi zimefanikiwa katika hili tunatarajia kupata huo uzoefu," alibainisha.

Makamba alisema washiriki watapitia sera, sheria na mikakati ya kifedha na teknolojia itakayowawezesha kuelekea katika nishati safi na salama, na kwamba majibu yapo mengi na mapendekezo yapo mengi, hivyo mazungumzo yatasaidia kupata muelekeo wa njia sahihi wanapotaka kwenda.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kuna athari za mazingira na zingine ikiwamo wanawake kutumia zaidi ya saa sita porini kutafuta nishati ya kupika na kujikuta wanapoteza muda kwa ajili ya kufanya majukumu mengine.

Waziri huyo alisema wao kama wizara wanaamini tatizo la namna ya kupika ni kubwa kuliko wanavyolijadili na kulichukulia hatua.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Telegram: "Uvuvi"
Simu: 255 026 2322612
Fax: 255 026 2322613
E-Mail: ps@uvuvi.go.tz
Web:http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
40487 DODOMA.
10 Oktoba, 2022

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA MSIMU WA UVUVI WA KAMBAMITI (PRAWNS) KWA MSIMU WA MWAKA 2023

Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) kupitia Idara ya Uvuvi inapenda kuwatangazia wananchi wote kwamba uvuvi wa Kambamiti (Prawns) kwa msimu wa mwaka 2023 utafunguliwa tarehe 1 Machi mpaka tarehe 30 Septemba, 2023 kwa Kanda ya Kaskazini (Dar Es Salaam, Tanga, Bagamoyo na Saadani) na tarehe 01 Aprili hadi tarehe 31 Agosti, 2023 kwa Kanda ya Kusini (Kisiju, Rufiji delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara).

Kwa tangazo hili, kila kampuni au mwananchi mwenye nia ya kufanya uvuvi wa kambamiti kwa msimu wa mwaka 2023, anaombwa kutuma maombi kuanzia tarehe 20 Oktoba mpaka tarehe 09 Novemba, 2022. Waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na Marekebisho yake ya Mwaka 2020. Aidha, vigezo vya kuzingatia katika maombi ya uvuvi tajwa vinapatikana katika Tovuti ya Wizara **(www.mifugouvuvi.go.tz)** na katika Ofisi za Wizara Kanda ya Dar Es Salaam na Pwani.

Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo yatumwe katika Halmashauri husika na wavuvi wakubwa maombi yatumwe kwa Katibu Mkuu-Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Imetolewa na:
DKt. Rashid A. Tamatamah
KATIBU MKUU-UVUVI

21708902

# CYNTHIA STACEY TARIMO tutakukumbuka kwa uzalendo


Cynthia Lillian Stacey Tarimo 1945 - 2022.

Na Mwandishi Wetu

ALIPENDA kuitwa 'Mzungu' akifurahia utani na kuchangamka, kujichanganya na watu akisalimia kwa ufupi 'jambo' ndivyo alivyofanya kazi katika chumba cha habari cha The Guardian Limited.

Alikuwa na safu yake inayotoka kila wiki ya 'Start the Week With Cynthia Stacey', iliyosomwa kila Jumatatu kwenye gazeti la The Guardian.

Cynthia Lillian Stacey Tarimo, ametwaliwa na kuufanya 'ulimwengu wa The Guardian Limited, alioutumikia kwa zaidi ya miaka 20 kuwa na simanzi ukiomboleza kifo cha mwanahabari huyo aliyekuwa chachu ya kuibua mijadala, kupenda kufuatilia masuala ya maendeleo ya watu na pia kuhimiza uzalendo.

**Akizaliwa Aprili, 1945 katika familia ya watoto watatu ya Mama Marguerite Chaganis na baba mzee Sydney Stacey, amefariki akiwa na umri wa miaka 77.**

Kwa mujibu wa familia ya Ernest Tarimo, Cynthia alipata mashambulizi mbalimbali ya magonjwa akiwa likizo nchini Uingereza mwaka 2021, alipona na kurudi Tanzania, Mei mwaka huu aliugua tena hadi kulazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, akisumbuliwa na kifua na shinikizo la damu (presha kushuka sana) na kulazimu kulazwa chumba cha uangalizi maalumu hadi alipofariki Alhamisi Oktoba 6 na kuzikwa Oktoba 12, kijijini Mande Kilimanjaro.

Cynthia amefanya mengi, licha ya kuwa 'Mzungu', aliipenda Tanzania akitumia juhudi kuboresha maisha ya wengine hasa maskini.

Mara nyingi, anamrejea Mwalimu Julius Nyerere kama mfano wa mtu aliyeishi kwa ukamilifu na utimilifu asiyekuwa na tamaa ya mali, umaarufu wala kujilimbikizia mali huku wengine wakishindia maji au kipande cha muwa.

Licha ya kutoka kwenye taifa lililoendelea, Cynthia Stacey alikuwa mjamaa na asiyependa maisha makubwa, wanaomfahamu wanasema alikuwa wakawaida mno. 'Hafagilii' mavazi ya bei mbaya, sherehe kubwa za harusi, kujipamba kupindukia, kuishi kwenye makazi au nyumba za gharama kubwa, lakini kujistarehesha kupindukia wakati watu wengi wanaishi maisha magumu.

Akizaliwa Aprili, 1945 katika familia ya watoto watatu ya Mama Marguerite Chaganis na baba mzee Sydney Stacey, amefariki akiwa na umri wa miaka 77. Amesoma huko Uingereza, lakini akiwa na mapenzi na fani ya sanaa na ubunifu na alipata cheti katika fani ya Sanaa na Ujuzi wa Mitindo (art and design skills) bila kusahau uandishi wa habari.

Alivisoma vyote huko mjini South Tyneside akipata pia Diploma ya Creative Media Practice, katika chuo hicho na akaanza ustawi katika taaluma ya uandishi wa habari.

Ana sifa ya udadisi na kutaka kujua mambo kwa kuhoji maswali mengi yakilenga utendaji katika maisha na maendeleo ya watu yenye lengo la kuelimisha jamii. Ndicho alichokifanya muda mwingi kwenye uandishi wake.

Cynthia aliipenda fani ya sanaa na kwa kuanza aliajiriwa katika Taasisi ya Serikali ya Uingereza ya Iaing Art Gallery iliyoko Newcastle kama 'curator' mhifadhi kwa muda mrefu akihusika rasmi na elimu ya uhifadhi wa vitu na nyaraka za kale, kazi aliyoifanya hadi mwaka 1976, kabla ya kuja Tanzania na kujikita katika uandishi.

### KUJA TANZANIA

Amekuwa sehemu ya wanahabari wa Tanzania baada ya kuja nchini Januari 1980 na kufunga ndoa na Ernest Tarimo, mwaka huo na kujenga familia iliyokuwa na watoto na wajukuu. Maisha yake nchini yalikuwa kwenye 'media' mwandishi huru na maarufu wa kujitegemea akianza kwanza na gazeti binafsi la Kiingereza la 'The Family Mirror'.

Nguli huyo aliandika safu maarufu iliyomtambulisha kama 'The Mirror Musings' au 'Tafakuri za Mirror' na baadaye kuendelea kutoa maandiko mbalimbali katika magazeti ya The Business Times, The African, The Citizen na mwisho The Guardian alikosikika kwa muda mrefu, kila siku ya Jumatatu kupitia makala yake ya Start The Week With Cynthia Stacey.

Cynthia alikuwa mwanachama wa Chama cha Wanahabari cha National Union of Journalists cha Uingereza (NUJ) pamoja na Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu na Msamaha -Amnesty International.

Kwa ujumla harakati zake za uandishi na uanaharakati zilimkutanisha na wananchi wengi na viongozi wa serikali na taasisi mbalimbali katika kufuatilia maswali na masuala yaliyomgusa yaliyohitaji majibu na ufumbuzi kwa manufaa ya taifa na umma mkubwa uliokuwa ukisoma taarifa zake.

Matokeo ya harakati na juhudi zake ni pamoja na kuongezeka uwajibikaji na uwazi katika maeneo aliyoyagusia na katika maboresho ya huduma na utunzaji wa mazingira. Mojawapo ya matokeo ya juhudi zake ni katika eneo la mazingira lililoshuhudia kunusuru mbuyu mkubwa pembeni ya kituo cha mabasi cha Namanga, jijini Dar es Salaam, uliokuwa katika mchakato wa kukatwa na mkandarasi wakati wa ujenzi wa barabara ya Ali Hassan Mwinyi, wakati wa uongozi wa awamu ya tatu.

Cynthia aliipenda sana Tanzania na mdau wa Muungano akibarikiwa na mafanikio yake katika nyanja mbalimbali na kila alipochoka au kuzidiwa na joto kidogo la Bara alikimbilia Zanzibar alikokuwa na makao mengi na marafiki pia.

### NGULI MAENEO HAYA

Cynthia alipendelea kutembea na kusafiri alikuwa na utashi, katika sanaa ya upangaji wa upambaji au ' interior design skills' na alipendelea sana, kupangua na kupanga na kila alipoingia mahali jambo la kwanza lilikuwa ni mpangilio, kubadilisha, kuboresha na kupendezesha mwonekano kiubunifu. Kwa ujumla alikuwa mtu mwenye upendo na ukarimu mwingi, mcheshi na mwenye kufurahia maisha nyumbani na kazini.

***Bwana ametoa, Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. Amina.***

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

# TOLEO MAALUMU LA SIKU YA MBOLEA DUNIANI OKTOBA 13, 2022

**1. Utangulizi**

**Tarehe 13 Oktoba kila mwaka Dunia huadhimisha Siku ya Mbolea. Hivyo katika Siku hiyo, Tanzania huungana na nchi nyingine Duniani kuadhimisha siku hii muhimu katika tasnia ya mbolea. Idadi ya watu duniani inatarajiwa kufikia bilioni 9.7 kufikia mwaka 2050. Ni dhahiri kuwa kuongezeka kwa idadi ya watu na maendeleo ya uchumi wa viwanda kutapelekea uhitaji wa kuzalisha mazao mengi kutoka katika eneo dogo. Kwa mfano mwaka 1960 ekari moja iliweza kutoa chakula cha kutosheleza watu 2 (wawili) lakini inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025 ekari hiyo itapaswa kulisha watu 5 (watano). Katika nchi zilizoendelea kama Marekani, baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakitumika kwa malengo mengine yamebadilishwa kuwa mashamba ya chakula yenye rutuba kutokana na matumizi ya mbolea. Hali hii inaendana na juhudi zinazoendelea hapa nchini kwetu Tanzania za kuhamasisha wakulima kutumia mbolea hususan maeneo yenye udongo usio na rutuba. Rutuba ya udongo ni uwezo wa udongo wa kutoa viinilishe vyote muhimu kwa kiasi kinachotosheleza ukuaji wa mmea.**

Siku ya Mbolea Duniani iliadhimishwa kwa mara ya kwanza tarehe 13 Oktoba 2016 huko nchini Uingereza. Siku hii inalenga katika kuhamasisha wadau wa tasnia ya mbolea duniani kote kuhusu jukumu lao kubwa katika kuhakikisha kuwa wakulima wanatumia mbolea bora na kwa usahihi ili kuleta mapinduzi ya kijani na kuwa na uhakika wa chakula.

Siku hiyo ni kumbukizi ya maadhimisho ya uvumbuzi wa mbolea aina ya amonia uliofanywa na Bwana Fritz Haber mwaka 1908.

na matumizi ya mbolea yaliyosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa janga la njaa na kuleta uhakika wa chakula katika nchi nyingi duniani.

Lengo la maadhimisho ya siku ya mbolea duniani nchini Tanzania ni kupata wigo mpana zaidi wa kuelezea masuala mbalimbali katika tasnia ya mbolea. Masuala haya ni pamoja na mafaniko ya tasnia ya mbolea nchini, kuwahabarisha wadau wa mbolea hususani wakulima na wafanyabiashara wa mbolea mifumo mbalimbali ya upatikanaji na usambazaji wa mbolea.

Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani kwa mwaka 2022 yamefanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2022 na kufikia kilele chake leo tarehe 13 oktoba mwaka huu. Mamlaka ya udhibiti wa Mbolea Tanzania( TFRA) ndio muandaaji na mratibu mkuu wa madhimisho haya ambayo yanafanyika katika Viwanja vya Kimondo Mlowo, halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoa wa Songwe .Mamlaka inaeleza Sababu ya kuchagua mkoa wa Songwe ni kutokana na mkoa huu kuwa moja ya mikoa inayoongoza katika uzalishaji wa mazao Nchini, matumizi makubwa ya mbolea na mkoa wenye idadi kubwa ya wafanyabiashara wa mbolea.Maadhimisho ya mwaka huu hayanabebwa na Kauli mbiu " Matumizi Sahihi ya Mbolea ya Ruzuku kwa Kilimo chenye Tija". Mgeni rasmi katika maadhimisho ya siku ya mbolea Duniani ni Waziri Wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (MB).

**2. Mbolea ni nini?**

Kama kilivyo chakula kwa mwili wa binadamu, mbolea ni viinilishe au chakula cha mmea chenye viasili (Virutubisho) vikuu vya aina tatu ambavyo ni Naitrojeni (N), Fosforasi (P) na Potasiamu (K). Viasili (Virutubisho) hivyo husaidia katika kujenga mwili, kutia nguvu na kuwezesha mifumo iliyomo kwenye mmea kufanya kazi. Mbolea inaweza kutokana na ardhi yenyewe, masalia ya mazao, mikojo, vinyesi au miili ya viumbe wenye asili ya nyama waliokufa au mbolea za kutengenezwa viwandani.



*Dkt. Stephan Ngailo Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).*

Kirutubisho/kiasili cha Fosforasi (Phosphorus) huwezesha mbegu iliyopandwa kutengeneza mizizi yenye nguvu. Mbolea yenye kiasili cha Fosforasi (Phosphorus) inayotumika zaidi Tanzania ni Di-Ammonium Phosphate (DAP). Aina ya pili ya kiasili cha Naitrojeni husaidia mmea katika ukuaji na mbolea yenye kiasili cha Naitrogeni inayotumika zaidi Tanzania ni UREA. Aina ya tatu ya kirutubisho ni Potasiam ambacho husaidia mmea katika kutengeneza chakula (Photosynthesis), kufungua na kufunga matundu yanayosaidia upumuaji wa mmea (stomata). Kwa lugha nyingine, Potasiam husaidia mmea katika kuchukua hewa ya ukaa (CO2 – Carbon Dioxide) kutoka angani ambayo ni moja ya malighafi za ukuaji wa mmea. Potasiam huchochea kemikali za uyeyushaji wa chakula cha mmea (enzymes) na ni muhimu kwa uzalishaji wa kemikali za kutoa nguvu za mmea iitwayo Adenosine Triphosphate (ATP). Aina kuu ya mbolea yenye viasili vya Potassium itumikayo Tanzania huitwa Muriate of Potash (MOP). Matumizi ya DAP na UREA ni zaidi ya asilimia 60 ya mbolea zote zitumikazo nchini Tanzania.

Kutokana na mahitaji ya udongo na mazao, vituo vya utafiti wa kilimo vilivyoko kote nchini hupendekeza muunganiko wa viasili katika uwiano tofauti ili kutengeneza mbolea mseto ziitwazo NPK (Nitrogen, Phosphorus na Potassium). Hadi sasa hapa Tanzania, kuna aina zaidi ya mbolea 70 za NPK ambazo ni maalum kwa ajili ya mazao mbalimbali kama vile tumbaku, chai, kahawa na pareto.

Mbolea hufanya kazi katika mazingira yasiyo na tindikali au nyongo. Kwa lengo la kurekebisha hali ya udongo ili mbolea ifanye kazi vizuri, mbolea huongezewa viasili vingine (supplements) kulingana na hali ya udongo. Kama udongo una tindikali nyingi, basi huwekewa kiasili cha Calcium au Sodium. Kama udongo una nyongo (alkali) nyingi, basi mbolea huongezewa viasili vya Sulphur. Aidha Mbolea huongezewa pia viasili vya aina zingine kwa lengo la kuongeza muda wa mboga au matunda kuharibika baada ya kuvunwa. Viasili vya aina hii viko vingi na huwekwa kutokana na aina ya zao.

**3. Mafanikio ya tasnia ya mbolea nchini Tanzania**

Tanzania imekuwa ikifanya juhudi kubwa katika kufikia lengo la Azimio la Maputo la kuongeza matumizi ya mbolea kutoka kilo 19 za virutubisho kwa hekta hadi kufikia kilo 50 kwa hekta ili kuongeza uzalishaji na tija katika eneo la ukanda wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo



*Mhe. Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo*

Kusini mwa Afrika (SADC). Tangu kuanza kutekeleza majukumu yake mwaka 2012, TFRA imepata mafanikio mengi katika tasnia ya mbolea na kwa uchumi wa taifa kwa ujumla. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

3.1 Kudhibiti ubora wa mbolea kwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mbolea ili kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bidhaa bora wakati wote

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini imeendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti na usambazaji wa mbolea ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbolea bora wakati wote. Mifumo hiyo ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maghala ya kuhifadhia mbolea na wafanyabiashara wa mbolea nchini, kusajili wafanyabiashara wa mbolea, viwanda vya kuzalisha mbolea na mbolea zinazotumika hapa nchini.

**3.2 Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini;**

Mamlaka imeweza kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbolea 169, kusajili mbolea 447 na hivyo kuongezeka kwa mbolea zilizohakikiwa kufaa kwake katika urutubishaji wa udongo, kuwatambua na kuongeza usajili wa wafanyabiashara kutoka 632 hadi 4378, kuwafuatilia na kuwapa elimu juu ya utunzaji bora wa mbolea na utambuzi wa mbolea zisizokidhi viwango. Hatua hizi zimezaa ongezeko la matumizi ya mbolea kutoka tani 296,036 mwaka 2016/17 hadi kufikia tani 476,870 mwaka 2020/21 zilizochochea uzalishaji. Hili ni ongezeko la asilimia 61. Ongezeko hili ni baada ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuanzisha Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja ulioanza kutumika msimu wa kilimo 2017/2018 na kuwawezesha wakulima wadogo kutumia mbolea zaidi kutokana na kupata punguzo la bei litokanalo na kununua na kusafirisha baharini mbolea nyingi kwa wakati mmoja. Pia limetokana na elimu ya matumizi sahihi ya mbolea inayotolewa na TFRA kwa kushirikiana na wadau katika sekta ya kilimo. Ni jambo la faraja kwamba ongezeko la matumizi ya mbolea limekwenda sambamba na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao.

Aidha, ikiwa ni mwendelezo wa kuwawezesha wakulima kupata mbolea kwa bei nafuu, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali imetenga bajeti ya shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wote nchini. Mpango huu wa ruzuku utachochea kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini.

**3.3 Wadau wa mbolea kupunguziwa gharama, muda na umbali kufuata huduma Makao Makuu yaliyoko Dar es Salaam.**

Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania imeimarisha utoaji wa huduma kwa wateja. Uimarishaji huo umefanyika katika maeneo yafuatayo: -

**3.2.1 Uanzishwaji wa Ofisi za Kanda**

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Mamlaka katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Mamlaka imeanzisha Ofisi za Kanda nne ambazo ni Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Kati (Tabora) na Kanda ya kaskazini (Arusha). Aidha, kanda hizo zimepatiwa watumishi na vitendea kazi ili kuweza kutoa huduma za Mamlaka katika maeneo yao bila kuhitajika wadau kufuata huduma hizo makao makuu au watendaji kutoka makao makuu kwenda kutoa huduma katika maeneo hayo. Hii imepunguza gharama na muda.

**3.2.2 Utoaji huduma kielektroniki**

Katika kuimarisha utoaji huduma Mamlaka imeanzisha Mfumo wa Kimtandao wa Mbolea (Fertilizer Information System - FIS) ambao umeboresha utoaji wa huduma kwa wateja, kwa kutoa huduma za usajili wa wafanyabiashara wa mbolea na utoaji wa leseni, vibali vya kutoa na kuingiza mbolea nchini na usajili wa mbolea. Tangu kuanza kutumika kwake mwezi Machi 2021, mfumo umeongeza ufanisi na kupunguza adha ya utoaji na upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Mamlaka.

**3.4 Kuongezeka kwa viwanda vya mbolea na visaidizi nchini**

Katika miaka mitatu iliyopita kumekuwa na ongezeko la viwanda vya ndani vya mbolea kutoka 12 mwaka 2018 hadi kufikia viwanda 16 (13 mbolea na 3 visaidizi vya mbolea) mwaka 2022. Viwanda hivyo ni pamoja na MINJINGU MINES & FERTILIZER COMPANY LTD kilichopo Mkoani Manyara, kinachozalisha Mbolea za organiki zenye viritubisho vya fosfeti; DODOMA CEMENT LTD Kilichopo mkoani Dodoma, Kinachozalisha Chokaa mazao (Agricultural lime), KEENFEEDERS (T) LTD kilichopo mkoani Arusha, kinachozalisha mbolea za kimiminika zenye viinilishe vya Nitrojen na micronutriens; ABM EQUIPMENT SERVICES kilichopo Mkoani Tanga kinachozalisha Chokaa Mazao, Gypsum na kiinilishe cha Calcium. GUAVAY LTD kilichopo Jijini Dar es Salaam kinachozalisha mbolea za organic zitokanazo na masalia ya mazao kutoka katika masoko makubwa Dar es salaam. Hata hivyo bado uzalishaji wa mbolea zinazotengenezwa na viwanda vya hapa nchini bado uko chini kutosheleza mahitaji ya mbolea kwa wakulima wa Tanzania. Takribani asilimia 90 ya mbolea inayotumika nchini inaagizwa kutoka nje ya nchi. Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania imeendelea kutoa mafunzo kwa viwanda vya ndani vya mbolea ili viweze kuongeza uzalishaji wa mbolea kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

**4. Hitimisho**

Juhudi za Serikali katika uimarishaji wa tasnia ya mbolea kwa kushirikiana na sekta binafsi kumewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kwa wakulima ambako kumekwenda sambamba na kuongezeka kwa tija na uzalishaji mazao. Hii imeongeza kipato cha mkulima, usalama wa chakula, kuongeza wigo wa upatikanaji wa malighafi za viwanda na kuongeza pato la Taifa kunakotokana na uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi.

Ili kufanya maboresho zaidi katika tasnia ya mbolea, TFRA imeanza kutoa huduma kielektroniki katika kutoa huduma zake. Huduma hizi zimepunguza usumbufu kwa wadau katika tasnia ya mbolea. Mwisho, Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya udhibiti wa Mbolea Tanzania inaendelea kutoa wito kwa wafanyabiashara wa mbolea kujenga viwanda vya mbolea ili kuendelea kupunguza bei ya mbolea kwa mkulima.



*Shehena ya Mbolea ya Ruzuku iliyo katika moja ya ghala nchini tayari kunufaisha wakulima msimu wa kilimo 2022/2023.*

217085902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushirikiano Tanzania na Uganda kudhibiti ebola ni wa kupongeza

**JANA** nchi za Tanzania na Uganda zimeingia makubaliano ya ushirikiano mipakani mkoani Kagera, kudhibiti ugonjwa wa ebola.

Ushirikiano huo una lengo la kuhakikisha kuwa ugonjwa wa ebola hauingii nchini Tanzania hasa ikizingatiwa kuwa nchi hizo ni majirani na kuwa rahisi kupenya.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana katika mpaka wa Bugango, Wilaya ya Misenyi mkoani humo, kati ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Issessanda Kaniki na maofisa afya nchini Uganda.

Katika ushirikiano huo walikubaliana kufanya ukaguzi kwa wasafiri, kuwapima maambukizi ya ugonjwa wa ebola, kutoa cheti na kuweka vifaa vya kuzuia maambukizi vikiwamo vitakasa mikono, sabuni na maji tiririka.

Walikubaliana kuwa maofisa afya wote wa mipakani watoe elimu ya tahadhari na kuchukua hatua za pamoja kutoa huduma na kutatua matatizo yoyote yatakayojitokeza kwa pamoja.

Hatua hiyo iliyofikiwa na nchi hizo mbili ni ya kutia moyo kwa sababu bila ushirikiano katika kudhibiti ugonjwa huo utasambaa na kuathiri nchi nyingine za jirani. Magonjwa ya milipuko yanapojitokeza na serikali kuchukua hatua haraka, zinasaidia kudhibiti maambukizi kuenea kwa kasi.

Tanzania na Uganda zina ukaribu ambao watu wake hasa mipakani huingia kwa njia mbalimbali zikiwamo za kibiashara na hata katika shughuli zingine.

Undugu wa nchi hizo umetokana na mambo mengi kwani hata watu huoana na kutengeneza familia ambazo huimarisha udugu huo.

Hata lugha baina ya nchi hizo mbili watu wake husikilizana, hivyo makubaliano ya ushirikiano huo katika kudhibiti ugonjwa huo utaleta manufaa makubwa na kuondoa hofu kwa wananchi wake.

Imeelezwa katika makubaliano hayo kuwa ni ya ujirani mwema katika kudhibiti tishio la ugonjwa huo usiingie nchini kupitia mipaka yote mkoani Kagera, nchini Tanzania. Na kwa upande wa Ofisa Afya kutoka nchini Uganda, Mlekateka Jesca, alisema ushirikiano huo utasaidia kuwaelimisha wananchi wa pande zote kujikinga na ugonjwa huo.

Viongozi wa nchi hizo mbili waliwahakikishia wananchi kuwa ugonjwa wa ebola haupo Wilaya ya Mubende na Kampala na ushirikiano huo utatusaidia kuendelea kuudhibiti ili usiingie wala kuvuka kwenda Tanzania.


Katika makubaliano hayo ambayo pia yalihudhuriwa na watendaji kutoka Mkoa wa Kagera, ambao waliweka bayana kuwa tangu wamepata taarifa ya tishio la ugonjwa huo wanashirikiana na maofisa afya kutoa elimu kwa jamii kuhusu kujikinga na ugonjwa huo.

Wataalamu wa afya kutoka Kituo cha Mbale kwa upande wa Uganda na viongozi mbalimbali wa kata na vijiji, kwa upande wa Tanzania pia walikuwapo katika makubaliano hayo kuonesha kuwa nguvu inayotumika kudhibiti ugonjwa huo ni kubwa na kuhakikisha hauvuki kuingia Tanzania ili wananchi waendelee kufanya shughuli za kuzalisha mali bila hofu.

Magonjwa ya milipuko ni hatari kwasababu yanarudisha nyuma shughuli za maendeleo kutokana na gharama kubwa kutumika yanapokuwa yameingia kwenye nchi yoyote bila kuchukuliwa tahadhari.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Beatrice Moses

# Fursa kuongeza mbaazi shambani, tuitumie kwa afya na uchumi bora

**MBAAZI** ni kati ya mazao jamii ya mikunde ambayo kwa mujibu wa wataalamu wa lishe, sifa kubwa ya jumla ya mazao hayo ni kuwa na kiwango kikubwa cha protini, ikilinganishwa na zinazopatikana kwenye nyama na maziwa.

Pamoja na sifa hiyo, mbaazi zina sifa za ziada kwenye afya, japo maharagwe ndiyo yamebeba umaarufu kwenye kundi hilo, inapendwa na kuliwa zaidi, ikilinganishwa na mbaazi au kunde na mazao mengineyo yanayofanana nayo.

Hapo ndipo Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT), inaeleza kwamba, kupitia wadau wao wa utafiti imebainika mbaazi pamoja na sifa nyinginezo, inasaidia kupunguza udumavu wa akili.

Nakumbuka, Mtendaji Mkuu wa AMDT Charles Ogutu, akatuomba waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, kwamba wamekusudia kuyatekeleza na watashiriki kuhakikisha zao hilo linalimwa vya kutosha, pia kwa umuhimu wake iliwe kwa wingi kwenye familia hadi shuleni.

Hatua hiyo inatarajiwa kufanikiwa ndani ya uwekezaji mkubwa kwa wakulima 100,000 wa mazao ya mikunde na alizeti kwenye mikoa 11 nchini, ndani ya miradi inayotajwa kugharimu shilingi bilioni 4.5 .

Hivyo, uwekezaji huo unalenga katika kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora za mazao hayo, katika mikao inayotajwa kuwa ni Manyara, Singida, Morogoro, Dodoma, Lindi, Arusha, Ruvuma, Songwe, Rukwa na Njombe.

Kinachofurahisha zaidi ni kwamba, itatekelezwa hadi mwaka 2023 na endapo itakuwa na mafanikio, itaongezewa muda hadi mwaka 2024.

Nionavyo, AMDT ilianzishwa mwaka 2015 ikishirikiana na serikali tano, ambazo ni za Sweden, Ireland, Denmark na Uswisi, kwa kushirikiana na Tanzania.

**Sababu kubwa ya matatizo ya afya ya akili ni mabadiliko katika mfumo wa malezi ndani ya familia na jamii, msongo wa mawazo unaotokana na ugumu wa kushindwa kuhimili mahitaji ya kila siku, na matumizi ya vilevi hususani pombe, bangi na dawa nyingine za kulevya.**

Mtazamo wao ni kile kinachonigusa zaidi, kwamba kuleta mapinduzi kwenye kilimo. Hapo ina sura njema, kuhakikisha mazao yanapatikana kwenye masoko, pia jamii inatambua umuhimu wa chakula hicho bora kwa afya yao.

Katika kikao cha kazi kilichohusisha Watendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), pamoja na wadau wa maendeleo kuhusu Masuala ya Lishe nchini mnamo Juni 8, mwaka huu bungeni jijini Dodoma, serikali iliahidi kufanya uwekezaji kitaifa katika masuala ya lishe nchini

Lingine la faraja hiyo, ni pale Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, mgeni rasmi katika tukio hilo, akabainisha kwamba ni muhimu kuweka jitihada za kupambana na matatizo ya lishe kwa umma.

Pia akakumbusha kwamba mtu anapokosa lishe nzuri, anapata matatizo ya afya na mara zote kinamama na hasa wajawazito wanapokosa afya bora na watoto kuwa na udumavu wa akili na mwili, pia serikali itapata hasara, kwa sababu ya kuwa na watu wasio na afya bora, kutokana na maradhi yatokanayo na ukosefu wa lishe bora.

Iko wazi, lishe bora ina sura ya 'kila kitu.' Hiyo inalea umuhimu kwa watu wote na hasa watoto ambao kuna wengine, kati yao huwa na usumbufu kwenye kula vyakula vya aina fulani, huku vingine wakivikataa. Kwa kuwa wenzetu hao wadogo hawatambui maudhui ya umuhimu, wakivutiwa na ladha pekee, ni vyema wazazi wakaongeza umakini na kuweka mbinu sahihi za kuhakikisha wadogo wanakula.

Udumavu wa akili ni wazi nao una mchango kwenye utegemezi. Kwa hiyo, kama kuna namna nzuri ya kuupunguza, ni vyema familia na shule zikaona umuhimu wa kuwa na mlo wa mbaazi zaidi, kama ilivyo maharagwe ilivyozoeleka.

## HABARI KITAIFA

### NMB yazindua kampeni maalumu kufanikisha msimu mpya korosho

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa mwaka huu wa korosho unaanza rasmi kesho ukilenga kuzalishaji tani 400,000 za zao hilo, lengo ambalo Benki ya NMB imesema iko tayari na ina uwezo kifedha kuhakikisha linafanikiwa.

Katika kutimiza azma hiyo, jana benki hiyo ilibainisha utayari wake wa kufanya hivyo na kubainisha mikakati iliyonayo kulisaidia taifa kupata matokeo chanya kwenye msimu huu wa 2022/23.

Mbali ya mikopo na huduma zake zingine, NMB inapanga kutumia kampeni maalumu ya kuhamasisha matumizi ya benki kuufanya msimu huu mpya kuwa wa mafanikio makubwa zaidi kiuzalishaji na kibiashara kulinganishwa na misimu iliyopita.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa benki hiyo, Isaac Masusu, alisema kampeni hiyo imepewa jina la "Bonge la Mpango - Mchongo wa Kusini" na mchakato mzima unawalenga wakulima wa korosho na vyama vyao vya ushirika (AMCOS).

"Ili kuendelea kuhamasisha matumizi ya huduma za Benki ya NMB kwa wakulima na vyama vya ushirika, leo hii tunawaletea kampeni maalum tunayoiita 'Bonge la Mpango' na kwa mwaka huu tumekuja na kaulimbiu ya 'Mchongo wa Kusini'.

"Tumeona ni vyema tukailenga zaidi kanda hii ya kusini kwani tunataka kuendelea kuvihamasisha vyama vya wakulima (AMCOS) pamoja na wakulima hususani katika kipindi hiki cha msimu wa korosho kuendelea kufanya malipo na kuhifadhi fedha zao katika Benki ya NMB kwa usalama zaidi huku wakiendelea kunufaika na huduma zetu zilizo bora na zilizoenea katika maeneo mbalimbali," kiongozi huyo alibainisha.

Benki hiyo ilizindua kampeni hiyo jana kwenye Kongamano na Viongozi wa Vyama vya Ushirika mkoani Mtwara ililoliandaa kwa ajili ya kubadilishana mawazo jinsi ya kuufanikisha msimu huu na wadau wa zao hilo.

Alisema kongamano hilo pia limefanyika kwa kutambua namna kilimo cha korosho kimekuwa nguzo muhimu kwa ustawi wa Kanda ya Kusini hususani mikoa ya Lindi na Mtwara, pia kwa taifa na hata Benki ya NMB.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi (kulia), akimlisha keki mteja wa benki hiyo, Deodarus Nkeyera, alipokwenda kupata huduma Tawi la Mlimani City, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja. Kushoto ni Meneja wa Tawi hilo, Happy Ernest. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Gwajima atangaza kampeni kusaka wakatili wa watoto

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima ametangaza operesheni ya mtaa kwa mtaa, nyumba kwa nyumba, kuwasaka wanaowafanyia ukatili watoto.

Kwa mujibu wa Dk. Gwajima, hata wanaoshuhudia watoto kufanyiwa vitendo hivyo vya ukatili na kushindwa kutoa taarifa watachukuliwa hatua kali.

"Mapambano ya kulinda mtoto yanapamba moto nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, hatutakubali kuumiza watoto kwa sababu ya hasira na matatizo yetu watu wazima, hilo halikubaliki," alisema Dk. Gwajima.

Aliwataka wakuu wa mikoa, madiwani na wakurugenzi kwenye halmashauri zote kuwa karibu na wananchi na kuwapatia namba ambazo watakuwa wanatoa taarifa za vitendo vya ukatili vinapofanyika kwenye maeneo yao.

Alisema asilimia 60 ya vitendo vya ukatili kwa watoto vinafanyika kwenye familia zao na asilimia 40 nje ya nyumbani ikiwamo shuleni na kwingineko.

"Haiwezekani tukaendelea hivi, hawa wenye roho za ukatili tunawajua, ndiyo maana wakati mwingime tunapowakamata, utasikia wananchi wanaanza kusema huyu alianza zamani kufanya hivyo kwa sababu wanafahamu, kwa hiyo tushirikiane kutoa taarifa hizi," alisema.

"Sheria ya mtoto ya mwaka 2009 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2019 kwenye kipengele cha 95, inasema aliyeona, aliyeshuhudia vitendo hivyo vya ukatili kwa mtoto halafu akanyamaza na yeye ana hatia. Sasa haiwezekani tukawa tunaendelea kufanyia kazi matukio, lazima tuwe na mkakati, kila mtu awe na wivu wa kulinda mtoto wake na wa mwenzake kwa kutoa taarifa ili tuchukue hatua za kuzuia yasiendelee kutokea."

Aliwataka wazazi na walezi wa watoto, kuwa walinzi wakuu na faraja kwa watoto wao badala ya kugeuka kuwa chanzo cha kuwafanyia ukatili watoto.

"Mzazi ni mtu wa mwisho na wa kwanza anayetakiwa kuwa faraja kwa mtoto wake, hatuwezi kuendelea kuvumilia kuona kuna wazazi ambao wanaacha dhamana ya kuwa faraja na walezi wanawakatili watoto," alisema Dk. Gwajima.

"Serikali itamfikia kila mlezi, mzazi na mwanajamii aliyefanya ukatili kwa mwanajamii mwingine hususani kwa watoto. Nikiwa waziri mwenye dhamana, watoto ni mboni ya taifa, ukiwagusa umegusa taifa."

"Haivumiliki na wala hakutakalika, ni lazima tukupate ukimkatili mtoto, ni lazima wanajamii tuwalinde hawa watoto, ni zawadi na ni tunu. Taifa lina wivu mkubwa na hawa watoto. Ndio msaada wetu, kimbilio na faraja yetu katika siku zetu tunapoelekea kwenye uzee, lazima tuwalinde. Mimi ninashindwa kuelewa, jamii inaweza kuishi katika eneo ambalo mtoto anakatiliwa, lakini hawatoi taarifa mpaka madhara yatokee, ni lazima tutoke huko."

## KABWELA



# NBAA ilivyochangia kudhibiti fedha haramu

Na Joseph Mwendapole

BODI ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), imesema moja ya mafanikio inayojivunia ni kushiriki kikamilifu kuzuia utakatishaji wa fedha haramu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa bodi hiyo, Dk. Neema Kiure, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho yatakayofanyika Novemba 10 hadi 12 mwaka huu.

Alisema NBAA kwa miaka 50 tangu kuanzishwa kwake imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kwa wanachama wake ambao ni wahasibu na wakaguzi kurekodi miamala yote watakayoona ina mashaka na haieleweki.

Dk. Neema alisema bodi imekuwa ikiwaelekeza wakaguzi na wahasibu kuhakikisha wanatoa taarifa kwa vyombo vya usalama wanapoona miamala yenye mashaka ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa watu wanaohusika nayo.

"NBAA imekuwa ikitoa miongozo hiyo ikishirikiana na taasisi mbalimbali za serikali na wakaguzi wao ndio wamekuwa wakitoa maoni kuhusu taarifa za fedha na kwasababu wahasibu ndio wanapitisha miamala ya fedha kwa hiyo popote wanapoona utata ni jukumu lao kuripoti kwa mamlaka husika ili hatua zichukuliwe," alisema.

Kuhusu chemsha bongo ya masuala ya uhasibu, Dk. Neema alisema wataitoa kwenye vyombo mbalimbali vya habari na washindi watapatiwa zawadi wakati wa kilele cha maadhimisho hayo Novemba 30, mwaka huu.

"Chemsha bongo itakuwa katika masuala ya kila siku ya uhasibu kwa mfano je, unafikiri ni muhimu kwa kampuni za biashara kuwa na wahasibu? Au je, unaona kuna umuhimu gani wa kutoa risiti?" Alihoji.

"Mara nyingi tunapozungumzia mambo ya risiti watu wanafikiri ni masuala ya kodi tu hapana, unapokuwa mhasibu au mkaguzi ili utoe uthibitisho kwamba miamala ilifanyika lazima utoe risiti kuthibitisha kwamba kuna fedha ilitumika," alisema Neema ambaye ni msomi wa ngazi ya juu kabisa ya uhasibu CPA.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa elimu ya uhasibu kuanzia chini ngazi ya shule za msingi ili watu wajue masuala ya fedha na kwamba ndiyo sababu chemsha bongo hiyo haitahusisha utaalamu wa juu wa masuala ya uhasibu ili watu wengi waweze kushiriki.

Dk. Neema alitoa wito kwa wananchi wengi kushiriki maonyesho ya kihasibu yatakayofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam kwani mashirika mbalimbali yatatoa elimu bure kuhusu namna bora ya kutayarisha taarifa za fedha.



Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitambulisha huduma mpya ya kibenki isiyo na mipaka kati ya Tanzania na Comoro inayolenga kutoa miamala ya gharama nafuu kwa wateja na wafanyabiashara kati ya nchi hizo mbili. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Uwekezaji wa Kimkakati na matawi ya nje wa benki hiyo, Sumit Shekhar (kushoto), Mkuu wa Bidhaa za Rejareja na Uhakika wa Mapato wa benki hiyo, Mtenya Cheya (kulia) na Meneja Msaidizi wa Biashara na Taasisi za Fedha, Bruno Tarimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania, Uganda nguvu moja ebola

**Na Mary Geofrey,** MISSENYI

TANZANIA na Uganda zimeingia makubaliano ya ushirikiano mipakani mkoani Kagera, kudhibiti ebola kuingia nchini.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana katika mpaka wa Bugango, Wilaya ya Misenyi mkoani humo, kati ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Issessanda Kaniki na maofisa afya nchini Uganda.

Dk. Kaniki alisema walikubaliana kushirikiana kufanya ukaguzi wa kina kwa wasafiri, kuwapima maambukizi ya ugonjwa wa ebola, kutoa cheti na kuweka vifaa vya kuzuia maambukizi ikiwa ni vitakasa mikono, sabuni na maji tiririka.

Alisema walikubaliana kuwa maofisa afya wote wa mipakani wanatakiwa kutoa elimu ya tahadhari pamoja na kuchukua hatua za pamoja kutoa huduma na kutatua matatizo yoyote yatakayojitokeza kwa pamoja.

"Mkubaliano haya ni ya ujirani mwema katika kudhibiti tishio la ugonjwa huu usiingie nchini kupitia mipaka yote mkoani hapa," alisema Kaniki.

Naye Ofisa Afya kutoka nchini Uganda, Mlekateka Jesca, alisema ushirikiano huo utasaidia kuwaelimisha wananchi wa pande zote kupatiwa elimu ya kujikinga.

"Hapa mpakani hakuna ugonjwa wa ebola upo Wilaya ya Mubende na Kampala, ushirikiano huu utatusaidia kuendelea kuudhibiti ili usiingie hapa wala kuvuka kwenda Tanzania," alisema Mlekateka.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE
BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Majaribio ya Nguzo za Chuma**
**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-TMP-TP-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao kwa huduma za:

**Majaribio ya Nguzo za Chuma Baharini**
Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni, kituo cha kuhifadhia mafuta kilichopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
Mkandarasi Msaidizi lazima asaidie usakinishaji, utekelezaji, na uchanganuzi wa:
- Vipimo vya Static Tension,
- Vipimo vya Static Compression,
- Vipimo vya Static Lateral,
- Dymanic PDA wakati wa kusimika nguzo na baada ya kusimika nguzo,
- Dynamic DLT (Restrikes)

Vifaa vya kufanyia Static Tension Test na Compression Test vitatolewa na BBN (Mkandarasi Mkuu). Vifaa vingine vyote (vya majaribio) vitatolewa na Mkandarasi Msaidizi.

Pamoja na ugavi wa nyenzo, mkandarasi msaidizi pia ana jukumu la kutoa:
- taarifa za kina na mbinu za utekelezaji kwa kila hatua tofauti za majaribio,
- cheti cha urekebishaji (calibration Certificate),
- mpango-kazi wa majaribio / ukaguzi pamoja tathmini ya athari / hatari,
- vifaa / vipimo vya nyenzo,
- uchambuzi wa data na ripoti za kila matokeo ya majaribio,
- uchambuzi kamili wa mlinganisho wa ripoti kati ya matokeo ya majaribio ya Preliminary Static Load Test na Dynamic Tests,
- kuwasilisha ripoti na matokeo ya majaribio kwa EACOP

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:
- Uwezekano wa kutekeleza kandarasi hii kati ya FEB 2023 - MAY 2023 (kipindi cha majaribio ya nguzo za chuma),
- Orodha ya historia / rekodi inayofaa, inayoonyesha uzoefu usiopungua chini ya miaka mitano (5) katika utekelezaji wa majaribio ya static na/au dynamic ya nguzo za chuma baharini (offshore pile testing),
- Wafanyakazi wenye uzoefu na shughuli za Kuthibitisha Ubora / Kudhibiti Ubora (QA/QC),
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi husika,
- alama ya ubora ya CE,
- Kazi ya wakandarasi wasaidizi lazima ziwe kwa mujibu wa viwango vifuatavyo: ISO 22477-1/2 na 4.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia ya maslahi, unashauriwa.
- Kuzingatia kanuni za Matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com; **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 27 Oktoba 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217090502

# Benki yatambulisha huduma isiyo na mipaka

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Exim Tanzania imetambulisha huduma yake mpya ya kibenki isiyo na mipaka kati ya Tanzania na Comoro, inayolenga kutoa miamala ya gharama nafuu kwa wateja na wafanyabiashara kati ya nchi hizo mbili.

Akitambulisha huduma hiyo mpya katika soko la Tanzania jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Uwekezaji Kimkakati na Matawi ya Nje wa Benki hiyo, Sumit Shekhar, alisema huduma hiyo inatoa fursa kwa wateja wa benki hiyo kufanya miamala ya kifedha kati ya nchi hizo kwa kuwezesha malipo kutoka kwenye akaunti za wateja.

"Tunafuraha kuanza huduma hii tukilenga kurahisisha biashara kwa Wacomoro wanaotembelea Tanzania. Kama tunavyojua sote Comoro ni nchi ya visiwa vilivyopo katika Bahari ya Hindi inayoshiriki mipaka ya baharini na Tanzania kaskazini-magharibi, na tayari tumeshuhudia kuongezeka kwa maslahi ya biashara kati ya nchi hizo mbili."

Alitaja baadhi ya bidhaa ambazo zinapelekwa zaidi visiwani Comoro kuwa ni pamoja na mchele, saruji, samaki, vyakula, sukari, nishati ya mafuta na magari.

"Kwa upande wao wenyewe wanaleta Tanzania zaidi karafuu, vanila, na vyombo vya usafiri wa majini. Tanzania yenye idadi kubwa ya makampuni ya viwanda nchini na miundombinu mikubwa ya bandari inatoa ushirikiano mkubwa wa kibiashara kati ya nchi zote mbili. Hivyo bidhaa hii inalenga kurahisisha hilo," aliongeza Shekhar.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja wadogo na kati wa Benki ya Exim Tanzania, Andrew Lyimo alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kuongeza ufanisi wa huduma zake za kibenki za kielektroniki, ili kuwapa wateja huduma bora zaidi pamoja na kujitanua zaidi katika ukanda wa Afrika.

"Exim ni kati ya benki tano bora nchini Tanzania na benki kubwa zaidi katika visiwa vya Comoros na ni taasisi pekee ya kifedha kuwa na uwepo wake katika nchi zote mbili. Ujio wa huduma hii pamoja na faida za kibiashara na zile za kijamii pia utasaidia kuboresha ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizi mbili na pia kutengeneza fursa kwa wafanyabiashara na wazalishaji katika nchi zote mbili." alisema Lyimo.

# 'Rasilimali pekee hazitoshi kuipa Tanzania maendeleo'

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BALOZI wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, amesema rasilimali pekee hazitoshi kuipa Tanzania maendeleo, inapaswa kuwekeza katika nguvukazi yenye usawa wa kijinsia.

Alisema ikiwa wanawake watapewa fursa ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi, uchumi wa dunia utaongezeka kwa Dola za Marekani trilioni 28.

Balozi Elizabeth alitoa kauli hiyo jana alipowasilisha mada kuhusu ajenda ya usawa wa kijinsia wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) unaofanyika jijini hapo.

"Usawa wa kijinsia ni zaidi ya haki za binadamu, unakwenda hadi kwenye uchumi. Nchi yoyote inayohitaji kupiga hatua katika usawa wa kijinsia, lazima ihakikishe wanawake wanashiriki katika uchumi.

"Rasilimali peke yake hazitoshi kuchochea maendeleo ya nchi, bali nguvukazi iliyoko ndani ya nchi husika. Tanzania ina mafuta na gesi. Je, ushiriki wa wananchi ukoje? Wanawake wanashiriki vipi katika fursa hizi?

Alisema kwa kuwa na rasilimali hizo, anaamini Tanzania itazitumia kuhakikisha wanawake wanashiriki zaidi, akizipongeza asasi za kiraia nchini kwa kufanya kazi kubwa kuchochea ajenda ya usawa wa kijinsia.

Alisema kuna haja ya kuzingatia umuhimu wa kuwa na uchaguzi huru na kutoa nafasi kwa wanawake kushiriki kuchagua na kuchaguliwa, akisisitiza viongozi wa vyama vya siasa na madhehebu ya dini wanapaswa kuisaidia serikali katika hilo na yenyewe ihakikishe vyombo vya habari vinakuwa huru.

Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, aliunga mkono hoja hiyo, akibainisha kuwa ushiriki wa vijana na wanawake nchini katika kutoa uamuzi ni mdogo, akihimiza serikali na wadau wake kuchukua hatua kurekebisha kasoro hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, alisema mkutano huo wa siku mbili ni jukwaa muhimu kwa serikali na wadau kubadilishana mawazo ya namna ya kutatua shida zinazohusu masuala ya uwazi na uwajibikaji na kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za serikali.

Taasisi ya WAJIBU ilianza kuandaa mkutano huo mwaka jana, ukihudhuriwa na washiriki kutoka nchi mbalimbali duniani, baadhi wakishiriki kwa njia ya mtandao.




Mkuu wa Kitengo cha Kadi wa Benki ya CRDB, Farid Seif (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya 500,000/- kwa mshindi wa pili wa promosheni ya "Tisha na TemboCard" kwa mwezi Septemba, Diana Lucas Rutainurwa, katika duka la vifaa vya michezo la GSM Salamander Tower, Mtaa wa Samora, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Meneja Biashara ya Kadi na Malipo ya Kidigital Benki ya CRDB, Getrude Moragwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CWT yaonya walimu utovu wa nidhamu

**Na Steven William,**

MUHEZA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimewaonya walimu watakaojihusisha na utovu wa nidhamu ikiwamo uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi.

Onyo hilo limetolewa jana na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya CWT Taifa, Mashaka Mussa, wakati wa mkutano mkuu wa nusu muhula wa chama hicho uliofanyika wilayani Muheza.

Alitoa mfano wa mkoani Mwanza, ambako mwalimu alipata matatizo ya kama hayo na chama kililazimika kutumia Sh. milioni 187 kwa kumwekea wakili.

Mussa alisema nidhamu ni muhimu kuzingatiwa kwa kila mwalimu ili kulinda hadhi na kwamba ni marufuku kwa walimu kujihusisha kimapenzi na wanafunzi kwa kuwa ni kinyume na matakwa ya kazi na gharama kwa CWT.

Aliwakumbusha walimu kutumia Benki ya Walimu kupata mikopo ya kuwawezesha kujikwamua kimaisha kwa sasa na wakistaafu.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Erasto Mhina, alisema ni muhimu walimu wakatambua na kuheshimu taaluma yao, dhamana na imani waliyopewa kisha kuacha kutenda mambo yaliyo kinyume na maadili ya Mtanzania.

Aidha, aliwataka walimu kujenga mshikamano na upendo baina yao ili kujenga chama imara kwa kuwa bila kufanya hivyo kitakufa.

Kwa upande wake, Katibu wa CWT Jiji la Tanga, Andrew Kombo, alisema wawakilishi wa walimu mahala pa kazi wasisambaze sumu kwa walimu shuleni, kwa kuwa wanatakiwa kushirikiana ili chama kisonge mbele na sio kukibomoa kupitia mitandao ya kijamii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Tanga Mohamed Seif, alisema wawakilishi wa walimu mahala pa kazi waangalie changamoto na suluhisho lao kwa kuwa mkutano kama huo utafanyika tena mwaka 2025.

Naye Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Muheza, Mashauri Kanyama, alisema wako tayari kushirikiana na walimu ikiwamo kuwatetea mahala pa kazi wanapopata matatizo.

Naye Katibu wa CWT Wilaya ya Muheza, Mashaka Selemani, alisema mkutano huo ni wa kikatiba huku akipongeza ushirikiano na kazi nzuri inayofanywa na walimu na ndiyo maana ufaulu unaongezeka siku hadi siku.

# Usafi wa mikono kujikinga ebola, corona wasisitizwa

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wameshauriwa kupenda kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, ili kujiepusha na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza hasa kipindi hiki cha tishio la ebola na UVIKO-19.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Afya Mkoa wa Dar es Salaam, Enezael Ayo, wakati akikabidhiwa msaada wa sabuni kutoka Shirika la WaterAid Tanzania, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Unawaji wa Mikono Duniani ambayo hufanyika Oktoba 15, kila mwaka.

Alisema mkakati wa mkoa ni kuhakikisha kila kaya, taasisi za umma na binafsi, vituo vya kutolea huduma vya afya na maeneo yote yanakuwa na maji tiririka na sabuni.

"Tunafahamu kuna UVIKO-19 na sasa tumeingia kwenye tishio la ebola linatishia nchi ya Uganda na kama unavyoelewa nchi hiyo ni jirani na Dar es Salaam kama kitovu cha biashara kuna ndege nyingi zinaingia kutoka nchi mbalimbali, kwa hiyo wananchi wote tunatakiwa usafi wa mikono, kunawa sio tu kunazuia UVIKO-19 bali na magonjwa mengine ya kuhara, kipindupindu," alisema Ayo.

Wakati UVIKO-19 ilipoingia, alisema mwamko ulikuwa mkubwa na kila mtu kwenye eneo lake kunawa mikono, lakini kwa sasa umepungua.

Alisema msaada walioupata watagawa katika Hospitali ya Mwananyamala kwenye vituo vya afya vidogo, zahanati na wataangalia kwenye uhitaji mkubwa.

Kuelekea Siku ya Maadhimisho ya Unawaji Mikono, alitoa wito kwa wadau wengine kuendelea kuisaidia jamii unawaji mikono ili kuepukana na magonjwa hatarishi kwa afya yao.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwananyamala, Dk. Aileen Barongo, alisema wanashukuru kwa msaada walioupata na wanaendelea kuwahamasisha wananchi umuhimu wa kunawa mikono.

Alisema wanaofika hospitalini hapo wameonyesha mwamko wa kunawa mikono na wamejitahidi kuweka vituo vya kutosha vyenye maji tiririka ili kulinda afya zao.

Ofisa Mawasiliano na Kampeni wa Shirika la WaterAid Tanzania, Neema Kimaro, alisema wamekabidhi katoni 11 za sabuni ambazo ni sawa na lita 220 kwa ajili ya kusaidia kuzuia maambukizi ya ebola na UVIKO-19 katika vituo walivyotengeneza vya kunawa mikono Jiji la Dar es Salaam.

"Tunatamani wadau wengine kwenye masula ya unawaji mikono kuungana na sisi kuelekea siku ya maadhimisho ya unawaji mikono duniani na kukabiliana na janga hili la ebola na UVIKO-19," alisema Kimaro.

Kimaro alisema wananchi wanatakiwa kuzingatia umuhimu wa kunawa mikono kwa ajili ya kulinda afya zao na kuepuka kupata magonjwa hatarishi ambayo wanaweza kuyazuia.

# LATRA yataka usalama wa watu SGR

**Na Pilly Kigome**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), imelitaka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kulinda usalama wa wananchi kwenye miundombinu ya Reli ya Kisasa (SGR).

Kaimu Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi LATRA, Henry Bantu, alitoa agizo hilo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya wiki ya usalama wa reli.

Alilitaka shirika hilo kuzingatia usalama wa wananchi katika maeneo ya miundombinu ya reli kwa kutoa elimu stahiki kwa wananchi wa mijini na vijijini, ili wafahamu alama za usalama hali itakayosaidia kupunguza ajali za treni.

Alilitaka shirika hilo liweke kitengo maalumu kitakachoshughulika na ulinzi na usalama, miundombinu ya reli, abiria na watumiaji wengine wa reli.

Alisema TRC iweke baadhi ya alama za ishara na mambo muhimu ambayo mtumiaji wa reli anapaswa kuzingatia, ili kuhakikisha mtumiaji wa reli anakuwa salama.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu TRC, Mhandisi Masanja Kadogosa, aliziomba halmashauri nchini kuwa na utaratibu wa kuishirikisha TRC kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili kuepusha mwingiliano wa miradi baina ya mamlaka hizo.

Alisema katika maendeleo ya sekta ya reli nchini, serikali imeweka fedha nyingi katika ukarabati na ujenzi wa miundombinu mipya ya reli ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa SGR, ili kuhakikisha usalama wa miundombinu ya reli kwa watumiaji ni lazima kuwepo kwa mikakati madhubuti ya kuhakikisha jamii inapata elimu ya usalama wa reli.

Pia aliwataka wananchi wakiwamo wafugaji wanaochunga maeneo ya njia ya reli kuacha shughuli hizo maeneo hayo ili kuepusha ajali ambazo sio za lazima.

Kadogosa aliwataka wananchi wanaokwenda kupiga picha kwenye reli hiyo kuwa makini kwa kuwa wanaweza kupata madhara makubwa.

Aidha, alisema ujenzi wa SGR umekamilika kwa asilimia 100 na sasa wako kwenye majaribio.

Katika maadhimisho hayo ya wiki ya usalama wa reli inayojumuisha nchi wanachama wa SADC chini ya Umoja wa Vyama vya Reli Kusini mwa Afrika (SARA), yanafanyika kwa kaulimbiu ya "chukua tahadhari, treni zina mwendo wa haraka, ni hatari".




Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mawasiliano wa Halotel, Sakina Makabu (kushoto), Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Patrick Rwegoshora' na Ofisa Masoko Roxana Kadio, wakikata utepe wa zawadi ya gari itakayotolewa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHC kuzindua sera ubia na sekta binafsi

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limesema sera ya ubia itakayofungua milango kwa wawekezaji binafsi wa sekta ya nyumba itakamilika Ijumaa ijayo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, Meneja wa Habari na Uhusiano NHC, Muungano Saguya, alisema sera hiyo itazinduliwa sambamba na kaulimbiu "Tunajenga Taifa letu kwa Ubia na Sekta Binafsi'.

Alisema lengo ni kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi kuendeleza maeneo yaliyoko katikati ya miji yenye thamani kubwa kuliko majengo yaliyoko sasa.

Alisema tangu kuanza kwa utaratibu wa uwekezaji, NHC imetekeleza miradi 111 yenye thamani ya Sh. bilioni 300, kati yake 81 ya Sh. bilioni 240 imekamilika 30 ya Sh. bilioni 60 iko katika hatua mbalimbali.

"Miradi hii imechangia upatikanaji wa ajira, kuboresha mandhari ya miji yetu, kuongeza mapato ya shirika, wigo wa kodi za serikali, kupanga miji na kuongeza maeneo kwa ajili ya biashara na makazi," alisema na kuongeza:

"Katika uzinduzi huu tunatarajia kuwa na washiriki takribani 600 kutoka taasisi mbalimbali za serikali na binafsi, vyama na bodi za kitaaluma, wawekezaji binafsi wa ndani na nje ya nchi, mabalozi wa nchi zenye wawekezaji wakubwa na wawakilishi wa kamati za bunge wanaogusa shughuli za shirika."

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa NHC, William Genya, alisema wameamua kufanya marekebisho ya sera hiyo ili kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, kuvutia uwekezaji nchini ili ilete miradi mipya yenye tija kwa shirika na taifa kwa ujumla.

Alisema dhana ya ubia itaruhusu taasisi zaidi ya moja kufanya mradi kwa pamoja, huku akieleza kuwa shirika litatumia ardhi yake iliyoko katikati ya mji yote nchini kama mtaji katika kuwezesha miradi hiyo kufanyika.

"Shirika lina miradi mingi na wakati linaendelea nayo, linatoa pia ardhi yake kwa wabia wa sekta binafsi na ya umma kufanya miradi mingine kwa sababu mahitaji ya nyumba ni makubwa kuliko uwezo wa shirika ndiyo maana tukaamua kushirikiana, ili tuweze kuwa na nyumba nyingi Watanzania wapate makazi ya sehemu za kufanyia biashara kwa wingi," alisema.

"Ardhi hizi tunazozitoa katika miradi ya ubia ziko katikati ya miji na ili ubia uweze kufanya kazi ni lazima hicho kiwanja kiwe sehemu yenye thamani, na vingine vina majengo ambayo thamani yake ni ndogo hivyo tutayavunja ili kuruhusu uwekezaji mkubwa kufanyika na kwa kuanzia tumeweka orodha ya viwanja 60 kwa nchi nzima," alisema Genya.

Aidha, alibainisha kuwa sera hiyo wameiboresha ili kuepukana na changamoto walizokutana nazo siku za nyuma, ikiwamo ya kupata mbia ambaye hana uwezo mzuri wa kujenga jambo ambalo lilisababisha baadhi ya mambo kutokuenda sawa, pamoja na kutoa miradi mingi kwa mtu mmoja ambaye anashindwa kuitekeleza yote.

Genya alisema kwenye sera hiyo kuna vipengele vitawawezesha uwekezaji na kupata mbia ambaye ana uwezo atakayepata mradi mmoja kwa wakati mmoja kabla hajapata mwingine.

Vile vile, alisema katika majengo ya makazi ambayo yatakuwa na wananchi wanaoishi ndani wakati wa uwekezaji wataondolewa kwa muda na baada ya mradi kukamilika watarudishwa.

# Halotel kutoa zawadi ya gari ikisherehekea miaka 7 ya huduma

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Kampuni ya Mawasiliano ya Halotel wataanza kujishindia zawadi ikiwamo ya gari kupitia bahati nasibu inayoendeshwa na kampuni hiyo katika kusherehekea miaka saba ya huduma zao.

Kampuni hiyo pia imekuwa ikibuni bidhaa mpya zenye lengo la kuwazawadia wateja wake na Watanzania kwa ujumla wanaotumia huduma za mtandao mjini na vijijini.

Akiongea na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Sakina Makabu alisema wamezindua kampeni mpya inayojulikana "7 bang bang" kwa wateja wao ambao wamekuwa nao toka walipoanza miaka saba iliyopita.

"Kampeni hii itawapa fursa wateja kushiriki katika promosheni itakayowawezesha wateja wetu na wananchi wote kwa wale ambao watajiunga na mtandao wetu kushiriki katika bahati nasibu na kujishindia zawadi mbalimbali zikiwamo vocha, simu janja, televisheni janja 50, jokofu, Wifi router ya 4G na gari mpya aina ya IST ndani ya wiki 10," alisema Sakina.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Halotel, Patrick Rwegoshora, alisema promosheni hiyo ni moja ya ishara ya kuwashukuru kwa kuchagua na kutumia mtandao wao.

"Washindi 95 kila wiki, 32 kila mwezi, 16 kwa robo hii ya mwisho wa mwaka na mshindi moja wa mwisho wa promosheni (Grand draw) atajishindia gari mpya aina ya IST. Hivyo kutoa zawadi kwa jumla ya washindi 143 mpaka mwisho wa promosheni," alisema.

**Washindi 95 kila wiki, 32 kila mwezi, 16 kwa robo hii ya mwisho wa mwaka na mshindi moja wa mwisho wa promosheni (Grand draw) atajishindia gari mpya aina ya IST.**

HABARI KASKAZINI

## Waziri Ndumbaro aomba msaada wa kunusuru mahakama

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

SERIKALI imeziangukia taasisi za kimataifa zinazotoa misaada ya kibinadamu, kuitupia 'jicho' la huruma Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda (ICTR) iliyoko jijini hapo.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema mahakama hiyo kwa sasa inakabiliwa na changamoto mbalimbali na inahitaji uwezeshwaji ili kutekeleza majukumu yake.

Dk. Ndumbaro, aliipigia chapuo mahakama hiyo jana ili kupata mafungu ya uwezeshaji, alipoitembelea na kukagua shughuli zake zinavyoendelea katika eneo la Kisongo.

"Wito wetu kama serikali ya Tanzania ni kwamba tunaziomba nchi wahisani ziendelee kusaidia taasisi za kitaifa na kimataifa zinazoshughulikia masuala ya amani na utoaji haki ambazo ziko hapa nchini kwetu, ikiwamo mahakama inayoshughulikia mabaki ya kesi za mauaji ya kimbari ya Rwanda," alisema.

Akiwa katika mahakama hiyo, Dk. Ndumbaro alizungumza na baadhi ya watendaji ambao walimweleza wanavyotekeleza majukumu yao, mafanikio na baadhi ya matatizo yanayowakabili.

Baada ya mazungumzo hayo, Waziri Ndumbaro alisema Tanzania itaendelea kutoa ushirikiano kwa mahakama hiyo kuhakikisha inaendelea kutekeleza majukumu yake kama kawaida na kama ilivyotarajiwa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za mahakama hiyo, Msajili wa Mahakama hiyo ya ICTR, Abubakar Tambadou, aliishukuru Tanzania kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi za kimataifa, ikiwamo mahakama hiyo.

Mahakama hiyo ni sehemu ya Divisheni ya Mahakama za Makosa ya Jinai (International Residual Mechanism for Criminal Tribunals-IRMCT), yenye ofisi zake The Hague, Uholanzi.

# Msekwa ataja mbinu kukomesha ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SPIKA wa zamani wa Bunge, Pius Msekwa, amesema ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia nchini, linaweza kupungua kama Watanzania wataiishi falsafa ya binadamu wote ni sawa na kila mtu anastahili kuheshimiwa utu wake.

Msekwa ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), amesema kuna haja kama taifa kuanza kuiishi falsafa hiyo aliyokuwa akiitumia Hayati Mwalimu Julius Nyerere ili kukabiliana na wimbi hilo, ambalo alisema hivi sasa ni janga.

Alikuwa akizungumza jana na wanataaluma, wasomi wa kada mbalimbali na watumishi wa MoCU, alipokwenda kutangaza uteuzi wake wa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Utawala na Fedha, Prof. Fredy Kilima.

**Wizara ya Madini, inafuatilia taratibu za ukamilishaji wa mchakato wa kuundwa kwa bodi hiyo, ili sekta za nishati, madini, maji na zingine mnazohusiana nazo ziweze kusimamiwa kwa weledi kwa manufaa ya nchi.**

"Bado matukio ya ukatili yanaendelea kwa kasi kubwa katika nchi yetu, licha ya jitihada za serikali na wadau mbalimbali wa masuala ya jinsia kupiga vita matukio hayo. Hayati Mwalimu Nyerere alikuwa muumini wa dhati wa dhana ile falsafa inayosema binadamu wote ni sawa na kila mtu anastahili kuheshimiwa utu wake.

"Ni vyema sasa, tunapomuenzi Hayati Mwalimu Julius Nyerere Oktoba 14, mwaka huu, natumaini kwamba imani hiyo au falsafa hiyo ikisambaa kwa watu wengi zaidi, inawezekana itasaidia kupunguza baadhi ya migogoro inayochipua hivi sasa, hasa hili la unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa aina mbalimbali," alisema.

"Kama kila mtu akijua kwamba binadamu wote ni sawa na wanastahili kuheshimiwa, huu ukatili unaoendelea sasa utakoma kama si kupungua," aliongeza.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), watu 15,131 walifanyiwa ukatili wa kijinsia kati ya Januari hadi Juni 2021, idadi ambayo ni wastani wa matukio 2,522 kwa mwezi na wastani wa 14 kwa siku.

Hata hivyo idadi hiyo ni pungufu ya matukio 4,209 ambayo ni asilimia 21.8 katika kipindi kama hicho mwaka juzi.

Maeneo yaliyoongoza katika kipindi hicho kwa ukatili wa kijinsia ni Arusha (1,697), Ilala (1,486), Tanga (1,347), Kinondoni (924) na Lindi matukio 780.



Spika mstaafu na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Dk. Pius Msekwa (kulia), akikabidhi nyenzo za kutekeleza majukumu kwa Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Utawala na Fedha, Prof. Fredy Kilima, aliyemteua kushika nafasi hiyo kwa awamu ya pili, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Chanzo cha maji cha Isanja hatarini kutoweka

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

CHANZO cha maji cha Isanja kilichoko Kata ya Nasai, Siha mkoani Kilimanjaro, kiko kwenye hatari ya kutoweka kutokana na kukithiri kwa shughuli za binadamu katika eneo hilo.

Aidha, baadhi ya wafugaji wa jamii ya Kimasai kutoka wilaya jirani za Longido, mkoani Arusha na Simanjiro mkoani Manyara, wanatuhumiwa kugeuza chanzo hicho sehemu ya malisho ya mifugo.

Akizungumzia jana kuhusu hatari ya kutoweka kwa chanzo hicho, Ofisa Tarafa ya Siha Kaskazini, Asteria Alfred, alisema kutokana na kujitokeza kwa madhara hayo, ameagiza viongozi wa serikali za vijiji na vitongoji kukilinda kwa hali na mali chanzo hicho dhidi ya wavamizi.

"Kuanzia Oktoba 11, mwaka huu, tumeanza kutumia sheria ndogo inayoelekeza kwamba yeyote atakayekutwa ameingiza mifugo kwenye chanzo hiki, ashughulikiwe.

"Faini ya kila mifugo ni Sh. 25,000 na ninyi wananchi wa Isanja, watangazieni kabisa na wengine hasa hao wavamizi kwamba muziki ni mnene, hatutawachekea maana nia yao si njema," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumia Maji ya Mto Sanya, Goodchance Moshi, aliyekwenda kuzuru eneo hilo kujionea madhara hayo, alisema ni wajibu kwa viongozi hao kukilinda chanzo hicho kwa ili maji yaweze kuwepo kwa kizazi cha sasa na kinachokuja.

"Sheria Namba 11 ya Mwaka 2009, imefafanua wazi kwamba chemichemi, matindiga na maeneo oevu kama hili la Isanja, yanatakiwa kulindwa kisheria na vijiji vinavyolizunguka eneo hilo, bila kungoja serikali kuu.

"Mtu anapokuja na kuanza kulima au kuingiza mifugo, serikali ya kijiji inatakiwa kumchukulia hatua. Kwa sababu ndani ya mita 60, hakutakiwi kufanyika shughuli za kibinadamu," alisema.

Chanzo hicho cha Isanja, kinazungukwa na vijiji sita, kikiwamo Kijiji cha Koboko Kaskazini.

Licha ya tahadhari hiyo, Joseph Mmari, ambaye ni mfugaji katika eneo hilo, aliwashangaza viongozi wa serikali baada ya kusisitiza kuwa wataendelea kuchunga mifugo ndani ya chanzo hicho.

"Tunaomba mturuhusu tuendelee kuchungia kwenye eneo hili kwa sababu kwa miaka mingi tumekuwa tukichungia hapa na hakuna aliyetuzuia. Hapa Isanja, ndiyo lilikuwa kimbilio letu kwa kuchungia ng'ombe. Hata nyie mnajua kwa sasa hali ni tete kwa mifugo yetu, inakufa kwa njaa kutokana na hali ya ukame," alisema.

# Waziri asisitiza mikopo riba nafuu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amezikumbusha taasisi za fedha nchini kutekeleza maelekezo ya serikali ya kutoa mikopo isiyo na riba kubwa kwa wafanyabiashara.

Pia amewaagiza watumishi wanaofanya kazi katika kituo hicho kujiepusha na rushwa na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara.

Waziri Mhagama alirejea maelekezo hayo jana, alipokuwa akizindua Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara katika Jiji la Arusha.

**Kati ya vituo 20 vilivyoanzishwa hapa nchini, kituo hiki cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara, kinaongoza kwa kutoa huduma bora.**

"Kati ya vituo 20 vilivyoanzishwa hapa nchini, kituo hiki cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara, kinaongoza kwa kutoa huduma bora.

"Natoa wito kwa taasisi za fedha, kuhakikisha zinatoa mikopo isiyo kuwa na riba kubwa kwa wafanyabiashara hasa wadogo wanaokopa kwenye taasisi zao kwa ajili ya kukuza mitaji yao," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali ilianzisha vituo 20 vya urasimishaji na uendelezaji wa biashara katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kurasimisha biashara zao.

"Nimejulishwa hapa kwamba wajasiriamali hawa 1,326 waliainisha mahitaji katika biashara zao, wafanyabiashara 840 walipata mafunzo ya kurasimisha na kuendeleza biashara zao kati ya hao 891 walisajili biashara zao na kupata leseni.

"Kutokana na idadi kubwa ya wafanyabiashara wanaotaka kurasimisha biashara zao kaimu mkurugenzi ninakuagiza upange mafunzo mengine ili kuongeza wigo wa wafanyabiashara wengi zaidi kusajiliwa wakiwamo mama lishe, mama lishe, waendesha bodaboda, pamoja na wajasiriamali wa kada nyingine," alisema.

Kuhusu watumishi wa umma kutoka vitengo mbalimbali wanaofanya kazi katika kituo hicho, Waziri Mhagama aliwaagiza kujiepusha na rushwa pamoja na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Hargney Chitukulo, alisema kituo hicho kilianzishwa mahusus kwa ajili ya kurasmisha wafanyabiashara ambao wanapata huduma zote za ushauri wa pamoja na mahitaji yote sehemu moja kwa ajili ya kupunguza urasimu.

Alisema mapato kwa kipindi cha kuanzia Machi, hadi Septemba, mwaka huu, yalikuwa Sh. bilioni 3.16 kutokana na ada za leseni zilizorasmishwa kwa kutumia mfumo wa kituo hicho jumuishi.

"Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23 tumekusanya Sh. milioni 830.57 na biashara zilizorasmishwa kwa kipindi hicho zikiwa 6,159," alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga (kushoto), akipata maelezo kwa Ofisa Ugavi Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Claude Kilala (kulia), alipokagua ghala la kuhifadhi vifaa vya msaada wakati wa maafa, mkoani humo mapema wiki hii. **PICHA: OWM**

# Wanafunzi wadai kuswekwa lupango kushinikiza wazazi kupeleka chakula

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

BAADHI ya wazazi wa wanafunzi wanaosoma Shule ya Msingi Nangara Ziwani iliyoko Halmashauri ya Mji wa Babati, mkoani Manyara, wameutuhumu uongozi wa shule kuwafungia kwa saa nne darasani wanafunzi ambao hawajalipiwa pesa za chakula cha mchana.

Tuhuma hizo ziliibuliwa jana na mkazi wa eneo hilo, Hamisi Wema, anayedai kuwa watoto wake wawili walifungiwa darasani kwa sababu baba yao ameshindwa kuchangia chakula.

Akizungumzia kitendo hicho, Wema alisema alichokifanya Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Simon Mritha, si cha kiungwana kwa vile alikuwa na uwezo wa kuwarudisha nyumbani ili kushinikiza wazazi au walezi kuwalipia chakula.

"Mimi nilimwambia Mwalimu Mkuu angenipeleka mahakamani kwa kosa la kutokupeleka chakula cha watoto na si kujichukulia jukumu la kuwafungia watoto," alisema Wema.

Mkazi mwingine, Ramadhan Salim, alisema alipata taarifa hizo baada ya kupigiwa simu na ndugu yake kwamba mwalimu amewafungia ndani ili wazazi wao wapeleke chakula.

"Ilibidi niondoke niende shuleni hapo na nilipofika, nilikuta kweli wanafunzi wamefungiwa darasani na sikuruhusiwa kumtoa mtoto wangu," alisema.

Baada ya kuhoji, alisema mwalimu huyo alimwambia ajitahidi kesho yake apeleke maharage kilo mbili na nusu, mahindi kilo mbili na chumvi ya gramu 500.

Naye Frida Paul, alisema tatizo la kuwekwa ndani wanafunzi Babati ni la kawaida, kwa kuwa hata yeye mtoto wake anayesoma Shule ya Msingi Gallapo, aliwahi kuswekwa rumande kwa sababu hajachangia chakula.

Mzazi mwingine, Shaban Ramadhan, alisema uamuzi alioufanya mwalimu haukubaliki badala yake wazazi ndio wangetumiwa mgambo ili wakamatwe na si wanafunzi.

Alipotafutwa kuzungumzia malalamiko hayo, Mwalimu Mkuu Simon Mritha, aligoma kuzungumzia sakata hilo.

Kutokana na malalamiko hayo, Nipashe ilimtafuta, Ofisa Elimu ya Msingi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Simon Mumbee, ambaye alisema halifahamu jambo hilo, hivyo apewe muda wa kulifuatilia.

Kwa mujibu wa Mumbee, shule 36 za serikali wilayani hapo ndizo zinazotoa chakula cha mchana, isipokuwa shule za Himiti na Bonga, ambazo bado wanawashawishi wazazi wachangie chakula.

# Wataka wavuvi haramu wabanwe

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

WAKAZI wa Kata ya Moa, Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, wamewaita maofisa uvuvi kwenda kuwadhibiti wavuvi haramu kutoka nchi jirani ya Kenya, wanaodaiwa kufanya shughuli hiyo kwa kutumia baruti.

Moa ni eneo lenye idadi kubwa ya wananchi wanaotegemea uvuvi katika mwambao wa Bahari ya Hindi.

Mwakilishi wa wavuvi wa eneo hilo, Haruni Dongo, alifichua siri hiyo jana wakati Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alipotembelea soko la samaki la Moa.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, suala la uvuvi haramu limekuwa kero kubwa ambayo inawasababishia wavuvi wenyeji kufika mbali kwenda kuvua samaki. Katika shughuli zetu za usimamizi wa bahari, bado tunasumbuliwa na uvuvi haramu katika bahari yetu na wavuvi hao ni wenzetu wa nchi jirani ya Kenya.

"Ingawa tuko kwenye suala la ujirani mwema ni shida kubwa. Tunaomba uwalete maofisa uvuvi waje kudhibiti maana huu ni uhujumu. Kilichoko sasa kwa wavuvi wetu wanakwenda kuvua mbali. Mvuvi anatoka alfajiri akirudi hapa anarudi na samaki kilo moja. Hali ya bahari ni mbaya, uvuvi haramu umetawala katika maeneo yetu ya bahari, hivyo tunaomba serikali itunge mkono katika kupambana na hali hii," alisema.

Akijibu ombi hilo, Mgumba alisema atakwenda kukaa na kamati yake ya ulinzi na usalama, kabla ya kulipeleka tena kwenye vikao vya ujirani mwema kati ya Tanzania na Kenya.

"Hatuwezi kukubali waje wachukue rasilimali zetu huku wakati sisi tupo. Lakini niseme mmetukumbusha wajibu wetu, askari wetu wa kulinda mipaka," alisisitiza.

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI OKTOBA 13, 2022



## YALIYOJIFICHA BAHARINI... Uelewa, vifaa duni unavyowaachia kiharusi kundi kubwa la wavuvi

Ukurasa 14



## Ajenda kukabili ukatili inavyoshika mtaani Mabwepande kunusuru afya

Ukurasa 20

# Vyanzo vikuu saratani: Uasherati, kujisahau na utamaduni wa kigeni

**Na Pilly Kigome**

HADI sasa imethibitika kwamba ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani nchini Tanzania linatokana na kile kinachotafsiriwa 'kujisahau' na 'kutokuenzi utamaduni' wa asili, jamii ikijikita kuiga ya kigeni.

Ni hali inayotajwa kuchangia ongezeko kubwa la ugonjwa huo, ambao tayari una madhara kwa taifa. Kutokana na hali hiyo, sasa inaaswa Watanzania wawajibike katika kuchukua hatua stahiki.

Uhalisia ulioko sasa kwamba, ni hali inayotawala ni kwamba, kuwapo kundi kubwa la watu walio hatarini kupoteza maisha, kutokana na ugonjwa huo, unaoongezeka kwa kasi sasa.

Taasisi ya LANCET inasema, hadi sasa imeshafanya utafiti wake na kuikabidhi Wizara ya Afya na kusema zaidi ya watu milioni moja watapoteza maisha ifikapo 2030 na endapo hakutachukuliwa mikakati stahiki kukabiliana na tatizo hilo.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassoro Mazrui, anaiambia Nipashe kuwa chanzo kikubwa cha kuongezeka tatizo hilo nchini, Watanzania wengi wamebadilisha mitindo ya maisha na kuacha mitindo yao, iliyozoeleka tangu enzi za mababu zao.

Mazrui anaeleza mwelekeo ulioko kwamba, Watanzania wengi wanaiga mifumo ya kimaisha kutoka mataifa ya kigeni, jambo linalokuwa chanzo kikubwa cha kuongezeka ugonjwa huo, bila ya wenyewe kujua.



Sehemu ya mandhari ya Taasisi ya Saratani Ocean Road. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Hapo anafafanua kwamba, kuwapo ongezeko la suala kupinga utamaduni na maisha kutoka mataifa ya kigeni, imegeuka hasara kubwa na mmomonyoko wa afya za kundi kubwa la Watanzania, bila ya kuona namna wanavyomaliza afya zao.

Katika hilo, anatoa mfano wa miaka ya nyuma, hakukuwapo magonjwa mengi kama ilivyo sasa kutokana na kuwa wakuu wao, mababu na mabibi waliishi katika uhalisia wa jamii ya Kitanzania na hakukuwapo mfumo wa kuiga maisha ya kigeni.

Anasema kutokana na kuishi ndani ya uhalisia huo, wao wameweza kuepukana na magonjwa mengi ambayo kwa vizazi vya sasa wamekuwa wakilazimisha baadhi ya matatizo ya mmomonyoko huo wa afya zao.

"Zamani nakumbuka chakula kinapikwa kwenye jiko la kuni au mkaa na kinatoka, kinanukia na ladha inayotoka ni chakula halisi. Ona sasa hivi hayapo hayo mambo, sasa watu wanapikia gesi, vyakula vinapashwa na vipashio jambo ambalo kwa upande mwingine linaharibu afya," anasema.



Waziri wa Afya Zanzibar, Nassoro Mazrui.

Katika hilo anafafanua kuwapo mengi ambayo watu wanaiga matumizi ya vileo, mafuta ya kutumia ya nyumbani, hata ngozi binafsi, kwamba vinachangia kutokea maradhi ya saratani.

Mazrui sasa anawashauri Watanzania warudishe maisha ya kiasili na kuachana na kuiga wazungu, matumizi ya mafuta kupitia vitu vya asili ikiwemo ufuta, nazi na karanga kwa kutumia mapishi yetu ya kila siku.

**BINGWA TIBA YA SARATANI**

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road, ambaye ni mtaalamu bingwa wa magonjwa ya saratani, Dk. Mark Mseti, anaiambia Nipashe kuwa mfumo mzima wa maisha hayo, ndio kichocheo kikubwa cha kuongezeka ugonjwa huo.

Anataja kuwapo sababu nyingi zinazochangia kuongezeka tatizo hilo katika jamii ya Kitanzania, akiamini wanaweza wakajiepusha nazo, hata kama ama watapunguza au kuepuka kupatwa na matatizo haya.

Dk. Mseti anataja sababu hizo, ni unywaji pombe kupita kiasi, kutofanya mazoezi, vyote vinachangia kwa kiasi kikubwa vichocheo vya saratani. Vilevile, anarejea suala la ulaji usiozingatia virutubisho nalo ni tatizo kwa Watanzania wengi, kwa kuwa wameangukia katika mtiririko wa ulaji usioendana na viwango stahiki.

Katika sura ya pili, bingwa huyo na bosi wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, anataja uvutaji sigara na matumizi ya tumbaku kwa ujumla, kemikali na mionzi, vyote vinaingia katika orodha ya kuchangia madhara husika.

Lingine analolifafanua ni katika suala la ngono zembe ya kuwa na wapenzi wengi, nayo inachukua nafasi ya kuibua maradhi hayo kwa jamii.

Daktari Mseti anasema kuwa, suala la kuwa na wapenzi wengi imekuwa staili ya maisha katika jamii sasa, pasipo kutambua wanajihatarisha kwenye mustakabali wa afya zao, husuan kwenye saratani ya mlango wa kizazi.

AFYA

YALIYOJIFICHA BAHARINI...

# Uelewa, vifaa duni unavyowaachia kiharusi kundi kubwa la wavuvi



Shughuli za uvuvi zikiendelea majini.. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Jenifer Gilla**

SAA 12 na robo alfajiri, Yusuph Saidi (52), anapanda mtumbwini kuelekea kuvua, akiwa na matumaini makubwa ya kupata samaki kwa ajili ya biashara yake ya kila siku.

Akiwa na wenzake wanne, wanatembea mwendo wa dakika 15 baharini, kisha wanasimama. Hapo wanavaa mitungi na kuzamia chini ya bahari mita 24 na kuanza kuvua samaki.

Baada ya muda mfupi, anaanza kusikia baridi kali inayotokana na maji kujaa ndani ya suti aliyovaa, kwa kuwa haikuwa na uwezo wa kuzuia maji mwilini mwake, kwani ina ubora hafifu.

Baada ya dakika 20, baba huyo wa watoto watatu, anaanza kujisikia vibaya hata anaamua kurudi mtumbwini apumzike kidogo. Tofauti na matarajio, anapata kizunguzungu kikali na kupoteza fahamu.

Dakika tano baadaye anapata fahamu, akiendelea kujisikia vibaya. Anaamua kurudi tena majini akiamini ndiko kwenye uponyaji wake, kwa kuwa ndiko tatizo lilikoanzia, akijipa mopo 'dawa ya moto ni moto.'

"Nikakaa huko dakika 20 kisha nikapanda juu, tukarudi nchi kavu na wenzangu baada ya kumaliza kuvua, wakati natembea kuelekea nyumbani nikaanza kujisikia tena vibaya," anasimulia kwa ufafanuzi:

"Safari hii nikaanza kusikia viungo vya mwili vikianza kufa ganzi na kupoteza mawasiliano, kuanzia mguu wa kushoto. Kwa kuwa ilishatokea kwa wavuvi wengi, tukajua tu ni dalili za kiharusi, Nikaanza matibabu kwa waganga wa kienyeji."

Yusuf anasimulia mkasa huo sasa, akitumia fimbo maalum kutembelea, kutokana na kwamba sehemu za mwili wake bado hazijapona vizuri.

Takwimu zinaonyesha wavuvi 372 katika Mwalo wa Buyuni, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni walio katika hatari ya kupata maradhi ya kiharusi, kutokwa na damu puani na masikio kuziba, kwa sababu ya kutumia vifaa duni na kukosa elimu ya matumizi.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinataja ugonjwa kiharusi ni wa pili kusababisha vifo kwa asilimia 11.8, baada ya magonjwa ya moyo.

Anasema, ni ugonjwa wa tatu unaochangia ulemavu wa watu kwa asilimia 4.5 duniani, hivyo kuwasababisha washindwe kufanya shughuli zao za kila siku.

**KUKWAMA KIMAENDELEO**

Mvuvi Mohamed Musa (51), mwenye mkasa unaofanana na mtangulizi wake, anasema amelazimika kuuza mali alizozipigania miaka 15 ya uvuvi, ili apate pesa ya kujiuguza na kuhudumia familia.

"Unajua nimekaa ndani miaka minne siwezi kunyanyuka, familia yote ilikaa pembeni, nikabaki na mke wangu tu. Ilinilazimu niuze mali zangu, ili nipate kujiuguza na kuhudumia watoto," anasema.

Mohamed mwenye miaka 34, anasema licha kupata maradhi hayo mwaka 2003, hali yake haijatengemaa vizuri, kwani analazimika kutembelea fimbo maalum au msaada wa mtu mwingine.

Baba huyo mwenye watoto wanne, anasema hajawahi kufundishwa darasani namna ya kuzamia baharini. Anafafanua: "Nilianza shughuli hii nikiwa kijana mdogo wa miaka 14. Nilikuwa nikienda na baba yangu kumsaidia kutupa nyavu, kisha taratibu akanifundisha kuogelea na baadaye kuzamia."

Licha ya kuendelea kuugua, baba huyo mwenye watoto wanne, anasema hakukaa chini, bali akatafuta njia nyingine ya kupata riziki, aweze kuhudumia familia, akiendesha mtumbwi wenye wavuvi.

**MARADHI NA MADHARA**

Katibu wa Wavuvi Mwalo wa Buyuni (BMU), Mussa Kayanda, ana ushuhuda tangu kupata uongozi mahali hapo mwaka 2018, ameshuhudia vifo visivypongua 16 vinavyotokana na ajali za uvuvi na wengi wamebaki vilema kwa muda mrefu, ikiwamo viziwi.

Mussa, ambaye amepata mafunzo ya uzamiaji salama nchini Afrika Kusini, anataja sababu kuu ya maradhi hayo kila mara ni matumizi ya vifaa visivyokidhi viwango katika uvuvi, akitaja baadhi ni suti ya kuogelea inayopitisha maji.

"Kuna suti za aina tatu kulingana na ubora. Zile ambazo haziruhusu maji kuingia kwenye mwili zinauzwa Sh. 400,000. Sasa wengi wananunua za kawaida zinazouzwa Sh. 150,000 hadi Sh.250, 000.

"Hata mitungi tunayotumia imechakaa na haina vifaa vya kuonyesha gesi iliyobaki kwenye mtungi. Kwa hiyo, mvuvi atagundua gesi imeisha pale anaposhindwa kupumua, hali ambayo ni hatari," anaeleza Mussa.

Uhusiano kati ya kuzamia na kiharusi Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Dk Martin Mbwile , anasema kuwa kadiri mtu anavyozama kuelekea chini presha ya maji inaongezeka na kusababisha hewa aina ya naitrojeni kuingia ndani ya mwili na damu ya mzamiaji huyo.

"Hivyo mtu anapokuwa anarudi juu ghafla anatakiwa kusimama kwa dakika tatu kila baada ya mita tatu mpaka tano, ili ile hewa iliyoingia kwenye damu na nyama itoke.

Sasa mtu huyu anapokuja juu ghafla hewa hiyo inabaki ndani ya mwili na damu na wakati mwingine inasafiri mpaka kwenye ubongo kupitia mishipa ya damu na kusababisha mtu kupooza ," alifafanua Dk. Mbwile.

Aidha anasema pia kadiri mtu anapopanda juu ya maji hewa huongezeka hivyo anapopanda ghafla anaweza kuathiri mapafu na masikio na kupelekea kupata uziwi.

Dk Mbwile anasema kuwa mzamiaji anapopata matatizo hayo anatakiwa kupatiwa huduma maalum kwa kuwekwa kwenye chumba chenye msukumo mkubwa wa hewa ya oksijen ikiwa ni sehemu muhimu ya tiba ya tatizo hilo.

Aidha Daktari huyo anasema kuwa yapo mambo mengine ambayo yanaweza kusababisha kupata kiharusi ikiwamo kisukari, presha na magonjwa mengine na kuwashauri kuwa na tabia ya kuchunguza afya zao mara kwa mara.

Baadhi ya wavuvi wanataja sababu zao kutibiwa na waganga wa kienyeji, ni kukosa hospitali maalum za zinazowatibu wazamiaji wanaopata kiharusi.

Mvuvi, Abdallah Rashidi, anasema ikamlazimu kutembea umbali mrefu mpaka katikati ya mjini Dar es Salaam, kutafuta tiba ya kutokwa na damu masikioni, hadi bila mafanikio.

"Hakuna hospitali ya wazamiaji hapa Tanzania, kuna chemba moja tu ipo Unguja na gharama zake ni za juu, kwa sisi wa hali ya chini hatuwezi. Matokeo yake ni kwamba tunakwenda hospitali za kawaida, ambazo hazina msaada wowote, bora tu tutibiwe kienyeji," analalamika.

**WASIMAMIZI WAKE**

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa ya Kigamboni, Joshua Bullu, anaeleza kuwa manispaa yao haijawahi kuelimisha uzamiaji salama, bali wanaelimisha namna ya kutumia vifaa vinavyoruhusiwa kisheria, pia wanakopesha pesa za kuzinununa.

"Kuna vikundi vya vijana na wanawake wavuvi watatu katika manispaa hii, ambavyo tumeshawapa mikopo ya dhana, ikiwamo boti na neti za kisasa za kuvulia, ili kuwaongezea ufanisi katika shughuli zao, ikiwamo Buyuni na bado tunaendelea." anasema.

Katika uwasilisho wa Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika bajeti ya mwaka wa fedha uliopo, Waziri Mashimba, anasema serikali imewatengea Sh. bilioni 266, sekta ya uvuvi ikipewa asilimia 65.

Anasema wizara hiyo, kwa kushirikiana na Shirika la Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo (EMEDO) inatekeleza mradi wa Sh. bilioni 2.7, lengo ni kupunguza vifo vya wavuvi vinatokanavyo na kuzama majini.

Kwa kipindi cha miaka mitatu kuishia 2025, anasema ilianza na mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera.

**WADAU WAKUU**

Mkurugenzi taasisi ya wanasayansi wa viumbe bahari, iitwayo Aquafarm Organisation (AFO), Jerry Man'gena, anasema walianzisha mpango wa kuelimisha uzamiaji salama kwa wavuvi, kuwapunguzia madhara.

Anafafanua kwamba inahusu sheria za kanuni muhimu za kuzamia, ikiwamo kupumzika saa kadhaa kabla ya kwenda kuzamia, jambo ambalo wavuvi wengi hawazingatii, wakiweka mbele kupata pesa.

"Katika kufanya kazi ukaribu na wavuvi hawa, tuligundua kuwapo kwa hili tatizo, kwa hiyo tukawapatia elimu ya uvuvi salama na kumpeleka Afrika Kusini kiongozi wao mmoja kupata mafunzo haya ambaye sasa anawafundisha wenziwe," anafafanua.

Lingine anafafanua, pia wanatoa vifaa vya kujikinga na madhara yatokanayo na uvuvi, ikiwamo mabuti ya kinamama wanaochokoa samaki.

MAZINGIRA

## MAGEUZI KUTOKA STAMICO

# Teknolojia inayozindua mkaa mpya kusalimisha misitu, afya wajawazito

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

"Mama yangu nilimnunulia zawadi ya mtungi wa gesi, lakini kila nikimtembelea nilikuta anatumia mkaa. Nilipomuuliza kwanini hatumii gesi ambayo ni rahisi na haraka, akaniambia anaogopa itaisha haraka.

"Ni kwamba vipo vyakula kama maharage ambavyo haviwezi kutumia gesi, kwa sababu yanachukua muda mrefu. Aliniambia pia kuwa chakula kama wali huiva vizuri zaidi akitumia mkaa," anasimulia Zawadi Matumbi, mkazi wa jiji la Dodoma.

Mama yake Zawadi hayuko peke yake katika imani hiyo kuhusu mkaa na gesi, bali wapo wengi. Matembezi Nipashe jijini Dodoma yalikutana na kinamama Zawadi wengi, wenye kuamini zaidi katika matumizi ya mkaa badala ya gesi.

Majira ya jioni katika maeneo ya Viwanja vya Nyerere jijini Dodoma, akakutana na vijana wanawasha majiko ya mkaa, tayari kwa ajili ya kukaanga chakula maarufu kwa vijana mijini, chipsi, ikiambatana na nyama za kuchoma, maarufu mishikaki.

Hao pia wanaamini kwamba, hakuna nishati zaidi ya mkaa wanayoweza kutumia katika kazi yao. Hapo anaeleza: "Sasa unadhani naweza kuchoma mishikaki kwa kutumia jiko la umeme au gesi? Siwezi, lazima nitumie mkaa."

Mchoma nyama Juma, anaeleza imani hiyo kwa nishati ya gesi au umeme, kudhihirisha uwepo wa watu wengi wanaotumia nishati mkaa au kuni, kwa sababu ndio iliyo rahisi na inafahamika zaidi nchini kuliko nishati mbadala ambayo hawaifahamu.

Katika imani hiyo mbadala, kumekuwapo ubunifu mbalimbali wa nishati mbadala itumike badala ya mkaa na kuni.

Takwimu zinaonyesha takribani hekta 469,420 za misitu nchini zinaharibiwa kila mwaka kutokana na shughuli za kibinadamu, ikiwamo matumizi ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

Miongoni mwa yanayobuniwa katika kuokoa misitu nchini, ni matumizi mbadala unaotokana na makaa ya mawe, ambayo unatengenezwa katika kiwanda cha kuzalisha mkaa mbadala cha Rafiki Briquette.

Teknolojia hiyo mbadala imeibuliwa na Shirika la Madini Tanzania (STAMICO), ambayo Mkurugenzi Mtendaji wake, Dk.Venance Mwasse, anasema miongoni mwa mkakati wake wa kutatua tatizo la ukataji miti hovyo ni kuhamasisha matumizi mkaa huo.

Anafafanua kuwa, wanalenga kulinda misitu inayoangamizwa kwa matumizi ya kuni na mkaa akifafanua: "Lengo ni kuwanufaisha watanzania zaidi, tunaamini hata wachimbaji wadogo watanufaika na utumiaji wa mkaa mbadala."

Mkurugenzi huyo anasema, mkaa huo unauzwa kwa bei kilo moja shilingi 1,000 na una uwezo wa kutumika mara tatu zaidi ya mkaa unaotokana na kuni.

Anafafanua kwamba, mkaa huo una faida lukuki ikiwamo kuondokana na athari za kiafya, kuokoa fedha na unakaa kwa muda mrefu jikoni.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akizindua mkaa mbadala ulioanzishwa na STAMICO, katika hafla ya maadhimisho ya shirika hilo jijini Dodoma, hivi karibuni.

### WAZIRI JAFO

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Dk. Selemani Jafo anapongeza ubunifu uliofanywa na STAMICO kwa kuanzisha mradi wa mkaa mbadala wa kupikia unaotokana na makaa ya mawe.

Anasema, matumizi yake yatasaidia kupunguza athari za ukataji miti inayotumika kama nishati ya kupikia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kuongeza kwamba STAMICO imeona mbali.

"Mkaa huu kweli ni rafiki wa mazingira umeonyesha mwarobaini wa kudhibiti matumizi ya mkaa unaotokana na miti, angalieni njia rahisi ambayo itaongeza matumizi haya," anasema.

Anashauri shirika hilo la madini liviwezeshe vikundi kuwapa mashine za kuzalisha mkaa mbadala, ili kuzisambaza kwenye maeneo mbalimbali ajira ipatikane.

"Pia shirikianeni na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), kufanya kwa pamoja kampeni mbalimbali za kuzuia ukataji miti hovyo na badala yake kuhamasisha matumizi ya mkaa mbadala," anasema.

### KAMATI YA BUNGE

Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, nayo imeipongeza STAMICO kwa kuibua teknolojia hiyo, Mwenyekiti wake, Dustan Kitandula, akisema ni ubunifu unaolenga kuchangia jitihada za kutunza mazingira, kuongeza ajira na nishati ya kupika.

Anasema, ubunifu wa STAMICO ni mkubwa na unahitaji pongezi, kwa sababu unachangia ongezeko la nishati nchini, zinazomuondoa mwananchi kwenye matumizi ya mkaa na kuni.

Kitandula anaitaka STAMICO kuongeza kasi ya kukamilisha utaratibu wa uzalishaji, ili kuifanya bidhaa hiyo kupatikana kwa wingi sokoni, kwa kuwa ina mahitaji makubwa.

Ushauri wake ni kwamba, zifanyike jitihada za kuutangaza zaidi mkaa huo ambao anaueleza ni mkombozi kwa wananchi.

### MADHARA YA KUNI

Waziri wa Nishati, January Makamba, akifungua semina ya wabunge wanawake kuhusu matumizi ya nishati mbadala ya kupikia, anasema moshi wa kuni kupikia unaua watu 33,000 kwa mwaka, kutokana na kutengeneza sumu inayouwa taratibu huku ukichangia kuharibika mimba.

Makamba anasema, wanawake wengi vijijini na mijini wamekuwa wakiathirika na moshi huo wa kuni wakati wa kupika katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kama wizara tunahitaji kutatua hili, ili kuokoa maisha ya kinamama ambao ndio wanapika," anasema Makamba, huku akitaja athari nyingine kubwa kwa wanawake, ni mimba kutokana na watoto kuzaliwa njiti, kitu ambacho taifa linapoteza nguvu kazi.



Meneja wa Masoko na Uhusiano wa STAMICO, Geofrey Meena, akionyesaha mkaa mbadala kwenye mzani katika Maonyesho ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika mkoani Geita. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU.**

MAZINGIRA

# Namna vijana wanavyojumuishwa sasa kuhifadhi mazingira kwa kizazi kijacho

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI mbalimbali duniani zikiwamo zilizoendelea, zinasisitiza umuhimu wa kutunza mazingira kwa ustawi wa jamii, kwa kuwa ndio chanzo cha mapato, msingi wa maisha na usalama wa wakazi wake.

Msisitizo huo huonekana kila mwaka, pale mataifa yanapokutana na kujadili mabadiliko ya tabianchi, usalama wa chakula, biashara haramu za misitu na wanyamapori, ongezeko la uchafuzi wa mazingira na kadhalika.

Vijana Waafrika wanasikika pia katika michakato ya kimataifa, hasa kuhusiana na mabadiliko ya tabiachi. Wakati Muongo wa Umoja wa Mataifa wa Uboreshaji wa Mifumo ya Ikolojia (2021-2030) ulipoanza mwaka 2021, vijana Waafrika walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu hilo.

Dira ni ifikapo mwaka 2030, vijana wengi wanatarajiwa kushiriki katika michakato ya kuamua katika nchi zao na hata kuvuka mipaka.

Hata hivyo, inaelezwa makundi ya wanawake na vijana yanasahaulika linapokuja suala la ajira na ushiriki katika mchakato wa maamuzi mbalimbali yanayohusu ardhi na mazingira.

Kwa mfano, kamati nyingi zenye wajibu wa kutunza mazingira mijini na vijijini, zinakosa uwakilishi wa vijana. Hata pale sheria na taratibu zinapolazimu, bado vijana hawajapewa jukwaa na fursa za kutosha na huchukuliwa kuwa bado ni wachanga katika mijadala hiyo.

Ni jambo linaloibua msuguano kijamii, kukishuhudiwa kugombewa matumizi ya rasilimali za mazingira kama vile ardhi, misitu na maji, hali inayodhoofisha mtiririko wa matunzo na uhifadhi wa mazingira nchini na kwingineko duniani.

Barani Afrika, kunatajwa vijana wameanza kubuni ajira rafiki na mazingira, wakikuza na kuboresha uchumi kwa kutumia bidhaa zinazopatikana kwenye mazingira yao, ikiwapo ajira na kitega uchumi. Hivyo, inatajwa sera za kuunga mkono kazi rafiki na mazingira, ina sharti kuwa na mashiko yanayowajumuisha vijana.

"Tanzania, vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 35 ndiyo wanaochochea maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi. Hawa ni sehemu kubwa ya idadi ya Watanzania na ndiyo nguvukazi ya nchi. Ni karibu theluthi moja ya Watanzania wote.

"Kwa hiyo, ni muhimu vijana wakajengewa mazingira mazuri ya kufanya kazi za kilimo hifadhi, ikiwa nchi inataka kushuhudia ukuaji haraka wa uchumi na uhifadhi wa mazingira kwa wakati mmoja.

"Ili kufikia lengo hilo, vijana lazima wamiliki rasilimali za mazingira kama ardhi na wawe na haki ya kuitumia ardhi hiyo kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla," anasema Franklin Masika, Ofisa Programu wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili kutoka Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT).



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Pugu jijini Dar es Salaam, wakiwa ndani ya msitu wa asili wa Pugu kujifunza kuhusu uhifadhi wa mazingira. **PICHA: MTANDAO.**

### USHIRIKISHWAJI DUNI

Mara nyingi, vijana hasa wa kike, hawashirikishwi katika masuala ya mazingira na rasilimali zake, ikitolewa mfano, hashawashiriki katika vikao vya kugawa ardhi, iwe serikalini au kimila, hivyo wanakuwa hawana mchango.

Kwa kuwa, vijana wa kike wananyimwa haki ya kumiliki ardhi na uhuru wa kuitumia, ushiriki wao katika utunzaji wake na mazingira kwa ujumla unakuwa mdogo.

Inatajwa, kuwakosesha morali, wanahisi hawanufaiki, hivyo hata uharibifu wa ardhi na mazingira unapotokea, wao hujiona hawana cha kupoteza.

Ni mustakabali unaotajwa kuibua haja ya kubadili utaratibu wa usimamizi mazingira na ardhi vijijini, uwe wa kuwatambua kuwa vijana wakike na wakiume wana haki sawa ya kushiriki katika kuamua na kumiliki ardhi, kutumia kilimo – hifadhi na shughuli za maendeleo.

Pia hapo kuna marejeo kwamba, vijana ni kundi muhimu kuchochea utunzaji mazingira kwa ujumla. Linahitajiwa kushirikishwa kikamilifu, hata kupata fursa za kutumia rasilimali zinazopatikana katika mazingira, kujenga maisha yao.

Vijana wanatajwa ndio wanaoweza kuhamasisha utunzaji mazingira, huku wenyewe wakishiriki kikamilifu, wakijua mazingira ni sehemu ya maisha yao.

Kimsingi, kundi hilo la jamii likiwekwa kando wasinufaike na misitu, maji, ardhi na rasilimali nyingine za kimazingira, wanaweza wakafanya uharibifu mkubwa au kuhujumu matumizi ya rasilimali, zenye manufaa kwa jamii yote.

Mara zote, suala la uharibifu wa misitu, ni eneo ambalo vijana wanaweza kushiriki kwa kiasi kikubwa, kwani suala la ukataji miti ovyo, hakuhitaji mtaji, bali shoka au panga pekee.

Hivi karibuni kumeshuhudiwa kuwapo majumuiko ya kijamiii duniani kama vile 'Fridays for the Future' vijana barani Ulaya na Amerika, wanajitokeza kudai uwajibikaji wa wazee na wamiliki wa viwanda. Hata hivyo, barani Afrika msukumo unatajwa uko chini sana.

Kwa ujumla, pale vijana hawanufaiki na misitu, huwa ni rahisi wakashirikiana na wavunaji, pia wafanyabiashara haramu wa mazao misitu, kikubwa wakilenga manufaa yao binafsi na zao lake huishia kuharibu mazingira.

Ili kufikia lengo, kunatajwa haja ya vijana kushirikishwa katika kupanga matumizi ya misitu, ardhi na rasilimali nyinginezo, wawe sehemu ya wamilikaji rasilimali hizo.

Hapo ndipo kunapoonekana manufaa ya vijana wanapokuwa tayari kutunza misitu na ardhi, katika mtazamo wa kunufaika.

Hadi sasa, baadhi ya shule nchini zimeshaanzisha vilabu vya mazingira, lengo ni kutoa elimu hiyo kuihamasisha jamii kutunza kwa manufaa yao.

### WANASHERIA NA MAZINGIRA

Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), ikishirikiana na Shirika la Maendeleo Endelevu Rukwa (RUSUDEO), wanawashirikisha vijana kutekeleza Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili.

Katika hilo, wanataja kuanzisha vilabu vya mazingira katika shule 19 wilaya za Nkasi na Sumbawanga, dhima ikijumuisha kuongeza ufahamu wa utunzaji mazingira na maendeleo endelevu katika jamii.

Wanalitekeleza hilo kupitia jukwaa la wanafunzi wabunifu na viongozi katika jamii, wakiwashawishi wanafunzi wenzao kushiriki kutunza mazingira, wakikukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, wanazama katika kubuni na kukuza shughuli zinazosaidia utunzaji mazingira ya shule na jamii, wakiwa ni wazungumzaji mashuhuri shuleni wanaowatia moyo na kuwaelimisha wenzao kuhusu usimamizi endelevu wa maliasili.

Vijana hao wanaendesha ajenda katika makazi na mazingira ya shule, wakiwajibika kutunza vyanzo vya maji, ardhi na usimamizi wa taka shuleni.

### KILICHOKO KIMATAIFA

Kimataifa, Shirika la Mazingira Duniani (UNEP) limeanzisha mashindano ya kila mwaka ya waandishi wa habari za mazingira vijana, kuwajenga hamasa ya kutunza na kuhifadhi mazingira, wakieneza elimu duniani.

Mtazamo wa ushiriki wa vijana unajengwa kuanzia za chini mtaani au kijijini, wakishirikiana na asasi za kiraia, ngazi ya kutunga sera, mabaraza ya ushauri na makundi ya kitaifa ya vijana.

"Ni jambo muhimu kuwashirikisha vijana katika kutoa maamuzi yanayohusu usimamizi wa misitu, kwani itawasaidia kupanga mipango endelevu ya namna ya kupata kipato na kuboresha maisha yao," limeandika jarida la Forest News.

Inatajwa, vijana wengi duniani wameshaanza kutambua umuhimu wa kutunza na kuhifadhi misitu, lakini huenda hawajui namna bora ya kutekeleza.

"Tunawahitaji watu wenye uzoefu na utaalamu, ili wawasaidie vijana hao watumie njia sahihi za kuhifadhi misitu, kama vile kupanda miti katika maeneo ya mistu iliyotoweka, ili kurudisha uoto wa asili," linahitimisha jarida la Forest, Trees and Agroforestry.

MAZINGIRA

# Ruwasa inavyotumia Bil.15/- kutajirisha mkoa wa Songwe na huduma ya maji

**Na Ibrahim Yassin, Songwe**



Eneo la Majimoto mkoani Songwe, ambako ni moja ya vyanzo vya maji ya Ruwasa.

MKOA wa Songwe umekuwa ukikabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa maji safi na salama, hali inayowanyima usingizi viongozi wa ngazi zote, hasa wa kuchaguliwa, kutokana na changamoto hiyo sugu.

Kuna maeneo ya jamii ya wafugaji, maji ni shida hasa wilaya za Momba na Songwe, ikafika hatua wananchi wanagombania maji na mifugo katika visima vya kienyeji visivyo safi na salama.

Serikali imeamua kuchukua hatua na hivi karibuni, imeelekeza fedha shilingi bilioni 20.5 katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji mkoani Songwe.

Kila halmashauri za mkoa huo hadi sasa, kuna miradi inajengwa na baadhi yake ipo katika hatua za mwisho, sambamba na ujenzi wa matenki makubwa ya kusambaza maji kwa wakazi.

Wilaya nne za mkoa, yaani Ileje, Mbozi, Songwe na Momba, zina mito zaidi ya mitano ukiwemo Rukwa unaotiririshia maji katika safu kadhaa za milima, hata kuupatia utajiri wa vyanzo vya maji.

Kutokana na umuhimu huo, serikali sasa inajenga miradi ya maji na yenye matenki makubwa ujazo hadi wa lita 100,000, ikitegemea vyanzo hivyo muhimu.

Ni vyanzo vya maji vinavyowalenga wafugaji na wakulima, sambamba na kulinda mazingira kwenye vyanzo hivyo na kuchoma mikaa .

Kwa upande wa wafugaji, baadhi yao wamekuwa wakiingiza mifugo yao kunywa maji kwenye mito na kuharibu mazalia ya samaki, mwelekeo wa maji na kuifanya miradi mingi haidumu, kutokana na uharibifu huo.

Hadi sasa serikali imetoa fedha nyingi za kujenga miradi hiyo na watekelezaji wake ambao ni Ruwasa (Rural Water Supply and Sanitation Agency), ambao wamekuwa wakiweka vibao vimavyoonyesha katazo kwa watu kuacha kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo hivyo.

Kwenye uwekaji wa vibao hivyo, Nipashe imeshuhudia bado kuna baadhi wanakaidi ikiwemo chanzo cha Matula kilichopo wilayani Mbozi, ambacho kinatumiwa na taasisi mbalimbali kuvuna maji hapo na kutumia, huku shughuli za kibinadamu zikiendelea hapo.

Wakulima nao wamekuwa wakilima hadi kwenye kingo za mito na wafugaji wanaingiza mifugo yao kunywa maji na kusababisha migogoro, ingawa wote wana sura ya kukosea.

**BIL. 15/- ZA SERIKALI**

Serikali hivi karibuni imeshatoa zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa wilaya za Mbozi na Momba, kwa ajili ya kuboresha miradi ya maji na kujenga mipya, inayojumuisha kuwekwa mabomba na matenki mapya.

Meneja wa Ruwasa wilayani Mbozi,Injinia Gratius Haule, anasema kwa wastani wa mwaka mmoja uliopita, washapokea zaidi ya Sh. bilioni sita za kujenga miradi mipya ya maji kwa maeneo yenye uhitaji, ukarabati na miradi mipya.

Anaitaja miradi hiyo ni; Hiwinga, Hatelele, Mlangali, Mbewe, Ilomba, Idiwili,Lwati, Shitunguru, Oldvwawa, Mahenje, Mwansyana, Vwawa, Mlowo, Msia na Iganduka.

Pia, anasema, ukarabati wa miradi chakavu unafanyika na wananchi wanaendelea kuvuta maji kwenye kaya zao, huku wakiendelea kutoa elimu zaidi za matumizi.

Katika utekelezaji huo, Injinia Haule ana ufafanuzi kwamba, kuna vyanzo vinavyotumika vimeanza kutumika vimevamiwa na wakulima, akitaja cha Matula, licha ya kuwepo vibao vinavyoonyesha katazo hilo.

Meneja wa mamlaka hiyo wilayani Momba, kwenye majimbo mawili ya uchaguzi, Tunduma na Momba, Injinia Maua Mgala, anataja kiasi walichopokea hivi karibuni Sh. bilioni 9.1.

Anasema hiyo ni kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maji ya; Nandanga- Msinde, Uhuru-Tunduma, Ipito - Mji Mwema, Uhuru - Mwalimu Nyerere, Niumba - Msamba 11-Ngangamo,Mkulwe,Tindingoma-Momba, Mpapa-Masanyinta ,Mkomba-Samang'ombe na Mbao.

Anasema miradi yote hiyo inatumia visima virefu vilivyochimbwa katika maeneo mbalimbali, ambapo wananchi ndiyo wahusika wakuu, wakiombwa kuvilinda, pamoja na miradi, iwasaidie wao na vizazi vijavyo.

**UMUHIMU WA VYANZO**

Inaelezwa kwamba, kumekuwepo na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na kijamii, yenye mwelekeo wa kushirikisha wananchi, sekta binafsi na halmashauri za wilaya na miji, hali iliyopunguza majukumu ya serikali kuu katika uendeshaji na kutoa huduma za kijamii.

Katika ugatuaji huo wa madaraka kwa wananchi, inajulikana kwamba utunzaji wa vyanzo hivyo vya maji, nafasi ya miti ni muhimu sana katika ustawi wa mazingira, pia chanzo kikubwa cha maji.

Jamii nzima inashauriwa kutunza vyema mazingira katika vyanzo vya maji,huku mamlaka ya maji na usafi wa mazingira Ruwasa wakifuatilia kwa karibu kuhakikisha mazingira hayaharibiwi.

Ruwasa ilianzishwa kisheria mwaka 2019 na kuanza kazi rasmi mwaka huo.

- ***Mwandishi anapatikana kwa simu: + 255 718382817***




Kituo cha maji wilayani Mbozi, Songwe. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

# Kuipa uhai bima ya afya, hoja ivuke zaidi ya pombe na sigara

**Na Nimi Mweta**




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akishiriki tukio la kutoa kadi ya bima.

MJADALA umeshaanza katika maeneo tofauti kuhusu serikali, ifanye nini kufuatia uamuzi wa uwepo wa bima ya afya kwa wote na kuvunja mfumo wa sasa wa bima. Kulikuwapo na sura mbili za taasisi mbili za umma, Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na Mfuko wa Kitaifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Mfuko wa kijamii CHF uliokuwa unatumika katika vituo vya afya au zahanati umefutwa, kwani unatajwa kwamba hautoi huduma zinazopaswa. Suala sasa ni kubadili mfumo wa uendeshaji wa NHIF, ili ukidhi mahitaji ya jumla ya bima ya afya na ufikiwe na watu wote.

Kundi ambalo si dogo la wachangiaji mjadala, linalojumuisha siyo tu taasisi za kijamii, ila pia hospitali nyingi binafsi zinazoendeshwa na mashirika ya dini, wametoa pendekezo ambalo linaweza kuleta mkanganyiko kiasi katika mjadala huo.

Hapo ni kuelekeza nguvu katika kutoza kodi (kwa maana ya kuweka tozo maalum) kwenye mauzo ya pombe na sigara, ili kupata fedha za uendeshaji mfuko huo, unapokuwa mpana na mkubwa zaidi.

Ni pendekezo lenye sura ya kitaaluma na kiasi nje ya taaluma, ikiacha swali kama fedha hiyo itatosheleza mahitaji au la?

Ingekuwa pendekezo hilo limetolewa na jopo la kawaida la kitaaluma, ingetafsiriwa inalenga kile kinachoitwa 'luxuries,' anasa ambazo kimsingi hazihitajiki katika maisha, ila ipatikane kwa uchache.

Ni jambo la kawaida kwa bajeti kuelekeza nyongeza za kodi katika maeneo hayo, ila kwa miaka miwili au mitatu mwelekeo huo umepungua, kama si kuondolewa kabisa.

Kulikuwapo uangalifu kiasi fulani katika kutolewa kwa pendekezo hilo, msemaji wa kundi hilo la kitaaluma akieleza tu kuwa kutoza pombe na sigara "kutaongeza ufanisi wa huduma za afya na kuangaliwa wagonjwa."

Hakusema kinaga ubaga kuwa kiwango cha tozo kinachoweza kuingizwa katika biashara hizo kitatosha, au nini kingine kifanyike (au kiongezewe) ili kujazia mapungufu (mapengo) kibajeti yanayotarajiwa.

Ukwepaji huo ni sawa na kushindwa 'nani atamfunga paka kengele'. Hata hivyo, ni mwelekeo ambao umesaidia kuonyesha penye haja ya kuelekeza 'tozo' bima ya afya na hata mpangilio wenyewe, kwa kutoa wazo linaloashiria tu nini cha kufanya.

Wazo la tozo ya vilevi na sigara ni jema, ila jawabu rahisi mno kwa tatizo lenyewe, na kwa hali yoyote ile tozo ya jamii hizo za bidhaa haitoshi kufidia mapungufu makubwa ya NHIF, hasa mfuko huo unapohitaji kupanuliwa kufikia watu wa makundi yote.

Kinachoweza kuchukuliwa kama wazo jema kimkakati ni kuwa tozo hiyo isitokane na huduma za kiserikali kama ilivyopendekezwa katika muswada wa awali, ila ielekezwe katika ulaji, kila mtu alipe kwa kadri atumiavyo.

Ina maana, kuwekwe tozo katika bidhaa ambazo husababisha magonjwa yasiyoambukiza, kwani ni katika eneo hilo ambapo fedha za kodi kawaida, yaani Bajeti ya Serikali inashindwa kutoa viwango hitajika.

Iwe ni kujua ugonjwa huo ukoje na dawa zinazofaa ni zipi. Inabidi mara nyingine mgonjwa apelekwe hospitali kubwa zaidi hata kama si ya rufaa, hivyo gharama za tiba kuongezeka na magonjwa yasiyoambukiza huchangia gharama za bima ya afya kwa kiwango kikubwa.

Ndiyo maana inakuwa vyema kwa tozo iwe kwa maeneo yote yanayochangia kuanzia vilevi, sigara, uingizaji magari, ununuzi wa mahitaji kama makochi, petroli, soda, juisi, sukari, usafiri wa gari unaochangia sana presha ya damu na kisukari.

Pia ziko nyama za aina mbalimbali, mafuta ya kupikia, mchele, unga ngano - tuseme ukweli, hata ingekuwa ni sembe au dona. Suala la kuwa maskini si hoja.

Viwango vya uchangiaji kujengeka presha ya damu au visukari mwilini hutofautiana, pia ununuzi wa bidhaa huendana na uwezo wa mtu kifedha, ambao unahitaji kuzingatiwa vilevile.

Tozo inaonyesha kuingiza katika mchakato na kuchangia bidhaa tofauti, hata kumfanya mtu apelekwe kwenye magonjwa yasiyoambukiza. Ni wazi kuwa, raha za magari na makazi, ambazo kwa sehemu kubwa huendana na vyakula vya aina kadhaa, ndiyo mchangiaji mkubwa.

Vilevi, navyo vina nafasi muhimu katika hali hiyo, wakati sigara inaweza kuleta madhara kwa miaka michache kabla ya kifo, si kama ilivyo presha na sukari.

Hivyo suala lililoko mbele ya wataalamu wa NHIF na Wizara ya Fedha, ni kuangalia kwa kina mfumo wa vichangiaji vya presha na kisukari, halafu saratani na waangalie ajali na gharama zake za matibabu, ili kila sekta ya 'ulaji raha' au kuonyesha ufahari wa matumizi itoe mchango katika mfuko wa tiba.

Kuongeza tozo katika leseni kadhaa itakuwa bure, ni fedha ndogo na ni fedheha kwa serikali kufukuzana na Wamachinga kuchangia wanaougua magonjwa ya anasa na maraha, ili watibiwe bure. Vinginevyo suala la bima liachiwe waajiri maeneo tofauti na viwango viendane na tiba zao halisi - hali isiyowezekana.

Hivyo ni suala la kupanua mfumo wa kodi uongezee tiba au tozo pana kulipiana matibabu; la sivyo suala hili labda liachwe kama lilivyo.

- ***Ni sehemu ya maoni binafsi, katika hoja ya kuipa uhai kibajeti Bima ya Afya.***



Shughuli ya kusajili uanachama wa bima ya afya. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

AFYA

# Safari ndefu ya malezi, makuzi na saikolojia, hadi iliko afya ya akili

**NA MICHAEL ENEZA**



Picha za wazazi wakiwa na watoto wao katika malezi ya ukaribu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

UDHAIFU wa maadili unaoonekana katika nyanja karibu zote za kijamii, kiasi kwamba hata nyimbo za dini zinabadilishwa zifanane na zile za starehe kwani vijana wanachoshwa na 'kulialia,' ni tatizo la kijamii linalowapa tabu wataalamu kueleza ama kinachotokea, au hatma yake.

Mwelekeo uliopo ni kwamba, hakuna aliye tayari kusema kuwa jamii ya sasa ni tofauti inaendeshwa kwa misingi mingine, kwani hakuna fikra rasmi au mambo mapya, na kwa kila hali jitihada bado zinafanyika kuwezesha malezi stahili kwa watoto.

Swali linaloweza kuulizwa ni hili hitilafu hutokea wapi? Bila kuitafuta mbali, yako maeneo mawili ya hitilafu na labda kuna sehemu nyingine ya kisheria, nje ya mazingira ya kijamii na kitamaduni jinsi yanavyobadilika.

La kwanza katika mpangilio mzima wa malezi ni nafasi ya mama katika mazingira mapya ya wengi kuwa waajiriwa au kufanya biashara ambazo haziwaweki karibu na watoto muda wote.

Baadhi ya watoa maoni, wakionyesha uhafidhina au falsafa za kulinda, kusimamia na kufuata mila, desturi na taratibu za jamii au taifa fulani wanaunganisha 'wazazi wote wawili' wakati kwa jadi baba si mlezi ila mlinzi. Hutafuta kinachotakiwa kwa kuilinda familia isitetereke, mama ndiye mlezi kihisia, hasa awali.

Mtoto anavyozidi kukua, nafasi ya baba inakuwa zaidi katika kuhakikisha nidhamu kwani anajisikia huru zaidi akiwa na mama ila siyo rahisi awe huru mno na baba.

Tatizo linatokea endapo kutakuwa na pengo la upendo au hisia chanya kwa jumla kati ya mama na baba kwa upande mmoja halafu baba na mtoto kwa upande mwingine.

Mtoto akishahisi hali hiyo anaingia katika 'gamba la kobe' akianza kujitegemea kihisia, huwa hahangaiki tena kumfurahisha baba yake kwa kufaulu shuleni, au nidhamu.

Si mara nyingi mtoto anayetegemea dira ya hisia zake mwenyewe kwenda njia inayofaa, kwani eneo la kwanza la kuvutwa na hisia ni starehe, na kufaulu katika maisha, kile wataalamu wanachoita ndoto za mtoto, lazima ziambatane na nidhamu na kutimiza wajibu.

Hawezi kupoteza nidhamu, kuwa na hisia potofu kuhusu wajibu (kwani jukumu si kwa waalimu au serikali ila kwa wazazi) halafu awe na ndoto ya kufaulu.

Mdogo huyo anaelekea katika starehe kwa mantiki ya njia rahisi zaidi ya kupita kwa mtoto au kijana anayefuatilia uhuru na siyo wajibu.

Ngazi hiyo ya malezi na halafu makuzi inafafanuliwa na msemo kwamba 'mtoto umleavyo ndivyo akuavyo,' ambayo inaleta hisia kuwa hakuna kitu halisi kama 'makuzi.'

Ni matokeo ya malezi kwa maana ya matokeo ya mtiririko wa hisia, ikichanganya na vipaji au vinasaba vya mtoto husika kwani siyo kwamba hajui kitu au afananishwe na karatasi nyeupe ambako 'malezi' huweza 'kuandika' chochote kile, kumpeleka mtoto pale mzazi anapotaka.

Ukweli uliopo ni kwamba, urithi ni muhimu zaidi katika dhamira, halafu mazingira hulegeza uwezo wa kufuatilia kilicho chema hasa nidhamu, kwa kuongeza uhuru.

Inaweza kusemwa kuwa uhakiki wa suala hilo una hitilafu katika chanzo hicho, kwani wazungumzaji hujiweka katika nafasi ya kilezi zaidi, yaani wao ni wazazi wema wanaotaka kuwalea watoto wao katika maadili mema, yanayozingatia amri au maelekezo ya dini.

Mtu akiangalia katika hali halisi, anakuta udhaifu mwingi na uelekeo wa wazi wa hisia za mtoto kwa kurukia mianya ya kuvuruga ndoto za wazazi inaendana na hitilafu hiyo ya mfumo wa fikra ya maadili.

**KUYUMBA MAADILI**

Unafiki wa maadili unaelezwa katika ujumla wa mawazo likija swali maadili ni nini? Kipi kinafaa kwa mtoto, kwa kuwa hakuna tofauti za wazi kwa upande huo. Ila mtoto anapopata umri kidogo, huanza kujazwa hisia tele, misukumo halisi inayotofautiana kabisa na maadili tarajiwa.

Moja ya maeneo yanayoleta udhaifu katika kuchambua mazingira ya malezi na makuzi kwa maana ya matokeo ya malezi, ni uwepo wa hitilafu zisizohesabika katika nyumba za watu.

Kuna hisia ya kikuhani vilevile kuwa nyumba bora ya mtoto kukua ni ile ambayo ina baba na mama wakikaa pamoja, bila kujali kufafanua zaidi.

Au wanasema hata wangejaribu kutoa maelezo ya ziada, watajitahidi kujikita katika msingi huo, ambao kwa wachambuzi wengine ni potofu.

Nyumba sahihi ya kukua mtoto, inatawa kuwa ni ile yenye amani ambako wanaokaa huko wanapendana kwa njia isiyo na hitilafu hata chembe. Kama ni mama na baba wawe wanapendana, ikiwa ni mama tu basi awe anawapenda watoto, daima ana matumaini katika maisha ili awajaze mema.

Inatosha kusikiliza vipindi viwili vitatu vya redio za mijadala ya masuala ya maadili au jamii kwa mfano vile vya asubuhi katika redio tofauti, katika kutanzua nani mbaya ndoa zinapoharibika.

Ni hapo kunakuwapo uwazi wa kutokuwapo mazingira ya amani, utulivu na picha bora ya jamii, ambayo mtoto anapata kama anakaa katika nyumba ya wazazi wawili na machungu tele, hasa kwa upande wa mama.

Mtoto anapobaki na mama peke yake na watoto halafu, huku akiwana hitaji kuhanagikia maisha na ndipo arudi nyumbani kwa muda anaotaka katika biashara na hata mahusiano, viwango vya woga kwa mtoto hupungua akipata mahitaji bila kufuatiliwa.

Dhana ya jadi ya malezi ya mtoto inaweza kujumuishwa katika usemi wa Mfalme Sulemani, uliotumiwa sana na wahenga yaani 'weka fimbo pembeni, umharibu au umpoteze mtoto.'

Baba na mama wakiwa wanafanya kazi, hakuna wa kuchukua fimbo kwa asilimia 90 ya muda wa kazi na ikifikia hatua ya kuhitaji kuchukua fimbo atajenga chuki.

Hivi sasa, siyo ku am mageuzi. Kuna ngazi za kisheria na kiuasalama, ikiwapo polisi pale mtoto anapodaiowa au kulalamika ananyanyaswa.

Haitakuwa rahisi kwa mzazi kuhangaika tena na mtoto huyo, ila amwache afuate mwelekeo autakao, na kama ana umri kiasi, atamhamisha hapo.

Akifanya vizuri shuleni ni majaliwa, haitakuwa tena suala la huyo mzazi na huwezi kutegemea kuwa kwa 'mbegu' hiyo utavuna kizazi cha vijana wenye ari kusoma na kufaulu katika maisha, ila kung'ara katika starehe.

Kijana mmoja miezi miwili iliyopita alimpiga ngumi usoni mama yake mdogo kwenye ukingo wa jicho, akitaka mama yake mzazi apelekwe hospitali. Anatoa amri, ilhali hana chochote cha kuliwezesha hilo. Hayo ndiyo malezi ya sasa yalikofikia.



# Ajenda kukabili ukatili inavyoshika mtaani Mabwepande kunusuru afya

**Na Yasmine Protace**

IKO wazi katika jamii sasa, mada za ukatili katika jamii zimekuwa ajenda kubwa kwa pande zote kijamii, huku vita vyake vikipiganwa kila kona. Kimsingi, ni ajenda rasmi duniani.

Hilo ndilo nalo linajiri hata ndani ya mkoa wa Dar es Salaam, katika eneo la Mabwepande pembezoni mwa mkoa wa Dar es Salaam, wilayani Kinondoni, ambako Nipashe imemulika kurunzi hata ikakutana na Athuman Njama, Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Mitaa mitano mahali hapo.

Anasema katika mitaa yao mitano ya Kata ya Mabwepande, ukatili uliokuwa unawaumiza kichwa ni matukio ya msuguano wa wanandoa, ambayo tafsiri yake inazama hata katika maisha binafsi kisaikolojia na hata kiafya.

Anaeleza kwamba katika mitaa yao, daima huwa hawalali,wakijikita zaidi kupambana na kuyatafutia suluhisho masuala hayo ya ukatili.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, wamejiwekea mikakati kufuatilia kwa namna nyingi, ikiwamo nyendo za siri kwa maisha ya wakazi na matukio ya kikatili, hata wanachukua hatua stahiki kuondoa kasoro hizo.

Njama anasema, katika mitaa yao mitano ya Mabwepande, anasema baada ya kuripotiwa katika ofisi zao, wameweza kuyasuluhisha na sasa msuguano wa wanandoa anautaja kwa takwimu umepungua kwa asilimia 89.



Wakazi wa Mabwepande mkoani Dar es Salaam, wakiwa katika kikao chao ngazi ya mtaa. **PICHA: MTANDAO.**

"Awali kulikuwa na ukatili sana unaofanyika kwa wanandoa, wapo waliokuwa wakipigana, wapo walioamua kutengana na wapo waliowatelekeza watoto.

"Lakini, baada ya kuwasikiliza wanandoa na matatizo yao, tumeweza kutoa elimu na hali hiyo imechangia matukio ya ukatili kupungua kwa asilimia 89," anaeleza mwenyekiti huyo.

Sehemu mojawapo anayoitaja kuchangia magumu hayo, ni kuwapo imani za kishirikina zinazochangia matukio hayo ya kikatili, akishukuru jamii za mahali hapo

kuibua kasoro zinazochangia ukatili, hatimaye kuvuka na wakafikia suluhisho.

Fatma Nuru, ni Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Mabwepande, anasema wameamua kuleta mrejesho, baada ya kuibuliwa changamoto katika mitaa yao na hadi sasa zimeshatatuliwa.

Anataja eneo lingine walikoibua shida, ni kwenye huduma za maji, ambayo ni muhimu kiafya na kimazingira, zikitatuliwa, hata wakasaidia baadhi ya maeneo kupata maji.

"Watu walikuwa wanafuata huduma ya maji kwa kutembea umbali mrefu. Baada ya kuibuliwa changamoto ya maji, imesaidia kufanikisha maji kupatikana katika baadhi ya maeneo," anafafanua.

Fatma anaeleza kwamba wakaamua

kutembelea maeneo mbalimbali ya mitaa yao kwa ukaguzi, hata wakafanikiwa kuibua changamoto hizo tajwa za maji, afya, elimu na miundombinu.

Anasimulia namna eneo la Mabwepande lilikuwa linakabiliwa na changamoto ya maji, hata baada ya kupaza sauti kwa mamlaka, sasa maji yanapatikana katika baadhi ya maeneo hayo

"Pamoja na kupatikana maji baadhi ya maeneo, lakini katika maeneo ya chekanao na Kiwanda cha Mboji Maji, bado haujafika," anasema.

Fatma anaongeza kwamba, kulishakuwapo changamoto ya kituo mahali hapo Mabwepande, lakini kutokana na kupaza sauti zao, wamesapotiwa fedha shilingi milioni 150 za kujenga kituo hicho.

Pia, anataja shida nyingine ni kwamba penye Kituo cha Afya Mbopu, kuna daktari mmoja hadi sasa na ombi kuu walilo nalo ni serikali iwasaidie watoe huduma zaidi, ili kuwapo ufanisi mahali hapo.

Anasema, pia wana upungufu wa shule za elimu ya msingi na sekondari katika mitaa hiyo mitano, vilevile kukiwapo watoto wenye ulemavu, lakini hawana fursa za kimasomo kwa wenye ulemavu.

Katika hilo, Fatma anafafanua kwamba wazazi wa watoto wenye ulemavu wamekuwa wakilazimika kuwapeleka mbali watoto wao wenye kasoro hizo za kiafya, wakati huo huo, baadhi yao wanakumbanana na changamoto kutomudu gharama na mazingira ya usafiri.

"Serikali isaidie kujenga shule za watoto wenye ulemavu katika maeneo ya Mabwepande, ambako hakuna shule hizo kuweza kuwasaidia wanafunzi walemavu kufika shule kwa urahisi," anasema.

Anataja sababu za wao kukwama, wazazi wengi hawamudu gharama husika za kuwafikisha watoto hao katika maeneo hayo tajwa.

Anasema, kinachofanyika sasa wao wameibua vitendo vya ukatili na kwamba kila shule kuanzishwe klabu zitakazozungumzia masuala ya ukatili.

---

## CHEMSHABONGO NA -00 12 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. waeneza habari
5. mnyama afugwaye
7. wingi wa neno dirisha
11.kazi ya ujenzi kwa kutumia mawe na matofali
13.nung'unika
15.ugwe
16.Wazee
17.Maskini
18.uzawa

Chini:
2. mji mkuu wa Eritrea
3. mtu mvivu
4. shetani
6. umbwa vizuri kwa sura na umbo
7. wingi wa neno fuvu
8. huvuta vitu vya asili ya chuma
9. heba
10.mtu asiye raia
12.kisichotosha
13.mji mkuu wa Peru
14.ami



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | | | | 3 | | | | | 4 |
| | | | | | | | | | | |
| | 5 | | 6 | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| 7 | | | | | | 8 | 9 | 10 | | |
| | | | | | | 11 | | | 12 | |
| | | 13 | | | 14 | | | | | |
| 15 | | | | | 16 | | | | | |
| | | | | 17 | | | | | | |
| 18 | | | | | | | | | | |

## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

BUNGE
BONGO
BURAHA
KICHAA
NANDI
NENDANA
UKUBWA
GADIMU
AMUA
IMARIKA
ADHABU
UDAKU
MNARA
SHABIKI
GADI
ABUDU
IBUA
TABU
MHAYA
UNAA
MKOA
ACHA
ADABU
ONEA
KATAA
UJI
MJA

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |
| | | | | | M | H | A | Y | A |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

Majibu toleo lililopita



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | M | E | M | E | | | M | | M | |
| M | E | M | A | | B | W | A | N | G | A |
| A | Z | A | N | I | A | | D | | E | |
| | A | U | A | | G | U | A | | N | |
| | | | | F | A | M | I | L | I | A |
| | | | | A | M | A | | | | |
| | | | | N | O | N | G | O | N | A |
| | | | | A | Y | A | R | I | | L |
| M | O | R | O | K | O | | E | L | E | A |
| T | | A | G | A | | | D | I | P | U |
| U | M | I | A | | U | Z | I | | A | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| G | O | M | A | | K | A | M | B | A |
| U | K | I | W | A | | | A | | F |
| S | O | K | A | | T | I | S | H | A |
| A | T | A | M | I | A | | H | | N |
| | A | S | U | B | U | H | I | | D |
| K | | I | | A | S | A | N | T | E |
| A | | | M | R | I | M | A | | |
| S | H | O | K | A | | A | | O | |
| H | | | A | | | S | O | K | A |
| A | N | G | A | L | I | A | | A | |





# Wakulima watakiwa kuzingatia matumizi ya mbegu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI), imewaomba wakulima wa zao hilo kuzingatia mafunzo wanayopatiwa juu ya matumizi ya mbegu bora na teknolojia ili kuongeza uzalishaji.

Meneja wa Programu za Utafiti TaCRI Kanda ya Mbeya, Dk. Dismas Pangalasi alitoa ombi hilo jana alipozungumza na Nipashe juu ya mikakati waliyoiweka katika kuhakikisha teknolojia na elimu kuhusiana na zao hilo zinawafikia wakulima.

Dk. Pangalasi alisema TaCRI imetoa mwongozo na mafunzo ambao unaelekeza wakulima mbinu mbalimbali za kilimo cha kisasa.

Aliongeza kuwa taasisi hiyo imebuni aina 19 za mbegu bora za arabika zenye sifa ya uzalishaji wa mavuno mengi na kuwa na vionjo tofauti kulingana na mahitaji ya soko la dunia pamoja na virutubisho.

Alisema mbegu hizo ni miongoni mwa mbegu zilizobuniwa katika kipindi cha miaka 19 ya utafiti uliofanywa na TaCRI na kusaidia hadi sasa kupata aina 24 za mbegu zilizobuniwa.

Licha ya kueleza mikakati na mafanikio ya taasisi hiyo katika kuwasaidia wakulima, alieleza pia vikwazo wanavyokabiliana navyo ikiwa ni pamoja na uhitaji mkubwa wa miche ya kisasa ukilinganisha na uzalishaji uliopo.

Alisema mahitaji ya miche ya kahawa ni makubwa kuliko uzalishaji wenyewe kutokana na ukata wa fedha, hali inayosababisha wakulima kushindwa kulima mazao ya kutosha.

Kutokana na hali hiyo aliiomba serikali na wadau wengine kuendelea kuwapatia fedha kwa ajili ya kuzalisha miche mingi itakayokidhi mahitaji ya wakulima na kuongeza uzalishaji.

**Mahitaji ya miche ya kahawa ni makubwa kuliko uzalishaji wenyewe kutokana na ukata wa fedha, hali inayosababisha wakulima kushindwa kulima mazao ya kutosha.**

# Wadau wataka mitaala kuandikwa kwa Kiswahili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa elimu wameishauri serikali kutengeneza mitaala mipya ambayo itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kusaidia kukuza lugha hiyo.

Wamesema hatua hiyo itawawezesha wanafunzi kuanzia darasa la awali hadi vyuo vikuu kujifunza kwa ufasaha lugha hiyo.

Walitoa maoni hayo juzi wakati wa Kongamano la Kumbukizi la Miaka 23 ya kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Walisema umefika wakati wa Tanzania kuanza kuienzi lugha ya Kiswahili kwa kuitumia kujifunzia kuanzia darasa la awali mpaka elimu ya juu.

Mhadhiri Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Richard Mabala, alisema umefika wakati wa Taifa kufanya uamuzi wa kuachana na lugha za kigeni na kutumia lugha ya Kiswahili katika kuwapatia elimu watu wake.

**Licha ya Mwalimu Nyerere kuhamasisha matumizi ya lugha za Kiswahili lakini hakuna jitihada zozote zilizofanyika ili kuifanyia lugha hiyo kuwa rasmi kwenye mitaala ya elimu.**

"Wakati ni huu, uamuzi ufanyike wadau na wachambuzi mbalimbali wa elimu wapewe nafasi ya kuchambua mambo muhimu ambayo yatahitajika katika mitaala ya elimu ili kuruhusu lugha ya Kiswahili itumike kwa ngazi zote za elimu hapa nchini," alisema Mabala.

Alisema msingi wa elimu ni kuwasaidia wanafunzi kuelewa masomo kwa lugha wanayoijua na kuzoea na kwamba katika kufanikisha hilo serikali inapaswa kutoa nafasi kwa wadau wa elimu wazungumzie ili kufanyika kwa marekebisho ya mitaala na mifumo mingine ya elimu.

Mtaalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki (CUCoM) kilichoko jijini Mbeya, Prof. Joshua Madumulla alisema kuna tatizo kubwa kwa wananchi juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili ikiwamo kwenye sekta ya elimu tangu enzi za utawala wa Hayati Mwalimu Nyerere.

Alisema licha ya Mwalimu Nyerere kuhamasisha matumizi ya lugha za Kiswahili lakini hakuna jitihada zozote zilizofanyika ili kuifanyia lugha hiyo kuwa rasmi kwenye mitaala ya elimu.

Aidha alitoa tahadhari kwa serikali kutoweka kando lugha ya Kiswahili katika mitaala ya elimu ili kukuza na kueneza lugha hiyo kinyume na hapo Watanzania wanaweza kuwa watumwa wa lugha za wenzetu.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Samora jijini Mbeya, Magreth Millinga alipendekeza lugha ya Kiswahili kutumika kujifunzia na kufundishia kuanzia ngazi ya chini hadi chuo kikuu.

Alisema serikali ifanye mazungumzo na wamiliki wa shule binafsi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye masomo yao kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kuelewa masomo wanayofundishwa.





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wa tatu kushoto), akipokea msaada wa vifaa tiba vya kupambana na ugonjwa wa Uviko-19 vyenye thamani ya Sh. bilioni moja kutoka kwa Makamu wa Rais na Mtendaji Mkuu wa Shirika la Henry Johnson Foundation Medical Research Insitute (HJFMRI), Elizabeth Folk, kwa ajili ya mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Shirika latoa msaada vifaa tiba mapambano corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Henry Johnson Foundation Medical Research Institute (HJFMRI), limekabidhi msaada wa vifaa tiba vya Sh. bilioni moja kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Vifaa hivyo ni mitungi ya gesi ya oksijeni, mashine za msaada wa kupumua kwa wagonjwa hospitalini na vitendanishi Mikoa itakayonufaika na vifaa hivyo ni Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi ambako vitasambazawa katika hospitali za mikoa hiyo.

Vifaa hivyo vilikabidhiwa jana katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, (MZRH), Mwakilishi wa Shirika hilo nchini Tanzania, Sally Chalamila, alisema lengo ni kuongeza nguvu kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 ambao umegharimu maisha ya wananchi wengi.

Chalamila alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha wanakabiliana na ugonjwa huo hasa kwa mikoa ya nyanda za juu kusini ambayo ina mwingiliano mkubwa wa mataifa mbalimbali.

Mratibu wa Chanjo, Mkoa wa Mbeya, Danford Barnaba, alisema shirika hilo limesaidia kuanzisha huduma za kliniki tembezi kwa ajili ya utaoji wa chanjo ya UVIKO-19, kuanzia Novemba 2021 hadi mwaka 2022 walifanikiwa kuanzisha vituo 333, kuwajengea uwezo watumishi 666 waliopata mafunzo kwa ajili ya utoaji wa chanjo nyumba kwa nyumba.

"Hata hivyo shirika hili limetusaidia kufanya usambazaji wa chanjo na vifaa vyake kwa ajili ya kuyafikia maeneo mbalimbali ya utoaji wa huduma za chanjo sambamba na hilo pia watumishi 125 wamejengewa uwezo wa namna ya kuingiza taarifa kwenye mfumo na kutuwezesha kuingiza taarifa hizo kwa asilimia 16,"alisema Barnaba.

Alisema mkoa umefanikiwa kuchanja watu zaidi ya milioni moja ambao wamepata chanjo ya UVIKO-19 na kwamba wamefikia asilimia 97 ya utoaji.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya wakuu wa mikoa minne Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka watumishi wa afya kuvitunza vifaa hivyo ili viendelee kutoa matibabu dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.





# Majibu malalamiko wafanyakazi Kampuni Barrick ndani siku 10

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu imesema timu iliyoundwa kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi 427 waliokuwa wa Kampuni ya Barrick imekamilisha kazi yake na majibu yatatolewa kwa barua ndani ya siku 10 za kazi.

Malalamiko hayo yalihusiana na wafanyakazi kutopimwa afya wakati wa kuachishwa kazi, kutopatiwa huduma ya matibabu na kutopewa malipo ya fidia kutokana na ajali au magonjwa waliyoyapata kutokana na kazi.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu, aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali za malalamiko hayo.

**Barua hizo zitatolewa kupitia Ofisi za Idara ya Kazi za Mikoa au Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama kwa kutumia anwani walizobainisha katika barua zao za malalamiko.**

Alisema wafanyakazi hao waliachishwa kazi kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 2007 na mwaka 2022, timu iliyoundwa imekamilisha uchambuzi na kuwasilisha taarifa hiyo kwake.

"Katika taarifa hiyo imeainishwa kuwa wapo walalamikaji waliobainika kuwa na magonjwa yanayotokana na kazi na hivyo mwajiri atawajibika kuwapatia matibabu, wapo wenye magonjwa yatokanayo na kazi na wamefikia ukomo wa kuimarika afya zao na mwajiri atatakiwa kuwafanyia taratibu za kuwalipa fidia," alisema.

Vilevile, alisema wapo waliobainika kuwa na magonjwa yasiyotokana na kazi na kutokana na matokeo hayo, walalamikaji wote waliowasilisha malalamiko yao watapatiwa majibu yao kwa barua ndani ya siku 10 za kazi.

"Barua hizo zitatolewa kupitia Ofisi za Idara ya Kazi za Mikoa au Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama kwa kutumia anwani walizobainisha katika barua zao za malalamiko," alisema.

Aliagiza uongozi wa kampuni uandae utaratibu wa kupokea malalamiko kwa kutoa namba ya simu maalum na watumishi ambao watashughulikia malalamiko.

Alitoa rai kwa waajiri na wafanyakazi katika sekta ya madini kutekeleza wajibu na majukumu yao kwa uadilifu na kufuata misingi ya kitaaluma ili kudumisha mahusiano kazini.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri (kulia), akizungumza na watoto wa Mtaa wa Nzuguni, katika ziara ya kikazi jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ummy aomba viongozi wa dini kukemea matumizi dawa kulevya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, ametoa rai kwa viongozi wa dini kuendelea kuhimiza jamii kuepuka uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya.

Nderiananga aliyasema hayo jana jijini hapo kwenye Kamati ya Bunge ya masuala ya Ukimwi na Dawa za Kulevya baada ya kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

Alisema ni vyema kuelimisha jamii kuhusu madhara ya dawa hizo ili kutopoteza nguvu kazi.

"Pia tutashirikiana na wizara nyingine kuona namna nzuri ya kuandaa maudhui ya mtandaoni ili kuelimisha vijana athari ya dawa za kulevya kama Tume ya Kudhibiti Ukimwi inavyofanya," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Alice Karungi, aliipongeza serikali kwa kiwango cha fedha kilichopelekwa kwenye mamlaka hiyo ili kuwasaidia vijana waliopata nafuu ya uraibu wa dawa za kulevya kupatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Gerald Kusaya, alisema mamlaka imeweka msukumo mkubwa katika kukabiliana dawa zinazotoka nje ya nchi, Heroin, Cocaine na Methamphetamine.

"Tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo waweze kushauri wananchi badala ya kulima bangi walime zao gani ambalo litawasaidia kupata fedha nyingi," alisema.

Awali, Mbunge wa Viti Maalum, Asia Halamga, aliomba serikali kubadili baadhi ya sheria zinazoizuia mamlaka hiyo kufanya kazi zake kikamilifu.

# KADCO yaeleza Royal Tour ilivyoongeza abiria KIA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI ya Uendelezaji na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO), imetaja mafanikio manne yaliyopatikana kutokana na filamu ya Royal Tour ikiwamo ongezeko la abiria kwa asilimia 88 kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

Aidha, amesema kutokana na ongezeko hilo pia miruko ya baadhi ya mashirika ya ndege ya kimataifa imeongezeka nchini ikiwamo Shirika la Ndege la Qatar litakalofanya safari zake mara 12 kwa wiki.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Christine Mwakatobe, alisema tangu kuzinduliwa kwa filamu hiyo pamoja na uwapo wa corona, watalii wengi wametua kwenye uwanja huo.

Alisema ongezeko la abiria ni kutoka 347,757 mwaka 2020/21 na kufikia 654,159 mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 88.

"Kupata Shirika jipya la Ndege la Eurowings Discover (part of Lufthansa Group) iliyoanza safari zake kutoka Frankfurt, Ujerumani kuja KIA kuanzia Juni, 2022. Shirika hili linachangia kuongeza idadi ya abiria na mizigo," alisema.

Alisema kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na mashirika mbalimbali ya ndege za kukodi ambayo yameendelea kutumia KIA kwa kuleta makundi maalumu ya watalii kutoka sehemu mbalimbali duniani.

"Shirika la Qatar hii ndege ya tatu itakayokuwa tumefanikiwa kupata dili ambalo watalii watakuwa wanatoka moja kwa moja Doha kuja KIA, na hawa watakuwa watu wanaokwenda kushuhudia kombe la dunia na hata wachezaji watakuja na kwenda kwenye vivutio na kurudi kuendelea na mechi," alisema.

Kuhusu janga la UVIKO-19, alisema katika kipindi hicho shughuli za uendeshaji KIA zilishuka kwa kiasi kikubwa kutokana na nchi nyingi kufunga anga.

"Ugonjwa huu ulisababisha idadi ya abiria kushuka kwa kiwango kikubwa kutoka 794,337 mwaka 2019/2020 hadi kufikia abiria 347,757 katika kipindi cha mwaka 2020/2021 ikiwa ni punguzo la abiria kwa asilimia 56."

"Kupunguza kwa shughuli za uendeshaji KIA kuliathiri mapato, ikizingatiwa kwa chanzo kikuu cha mapato ya KADCO ni tozo zinazotokana na abiria wanaopita KIA pamoja na kutua na kuruka kwa ndege kiwanjani, hali hii ilipelekea menejimenti ya KADCO kuchukua hatua ya kubana matumizi na kusimamisha kwa muda baadhi ya shughuli za maendeleo ili iweze kupita katika kipindi hiki kigumu ikiwa inaendelea kujiendesha,"alisema.

Kuhusu vipaumbele vya mwaka 2022/23, alisema ni kuongeza idadi ya abiria kwa asilimia 18, kuongeza mashirika mawili mapya ya ndege ya kimataifa yanayotumia Kiwanja cha KIA, kiwango cha mizigo kwa asilimia 16.

Kadhalika, alisema ukarabati na upanuzi wa eneo la maegesho ya magari kiwanjani kutoka uwezo wa kuegesha magari 83 mpaka 200 ili kuliwezesha kuhudumia ongezeko la magari, kuongeza mapato pamoja kuboresha mwonekano wake utagharimu Sh. bilioni 2.65.

Pia alisema kununua mitambo ya kisasa ya ulinzi na usalama yenye thamani ya Sh. milioni 700.



# Miradi kufikisha asilimia 80 majisafi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji na Nishati, Joseph Kilangi, alisema kukamilika kwa miradi ya maji kutapunguza uhaba wa huduma hiyo hasa katika mkoa wa Mjini Magharibi.

Kilangi aliyasema hayo jana baada ya kukagua miradi ya ujenzi wa matangi ya kuhifadhia majisafi na salama katika maeneo ya Dimani, Kwarara, Masingini, Kijichi, Mfenesini na Mgeni Haji ambayo miradi hiyo inatekelezwa na serikali.

Alisema kuna shehia 36 zitanufaika na miradi hiyo baada ya kukamilika na kwamba shehia hizo ni kutoka mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya ya Kati Unguja.

**Miradi hiyo itawanufaisha Wazanzibari, hivyo akawataka wananchi kulinda miundombinu ili kukamilisha miradi hiyo.**

Miradi yote, alisema imefikia katika hatua nzuri na mwazoni mwa mwaka 2023 inatarajiwa kukamilika na kuzinduliwa.

"Tunategemea ifikapo Machi, mwakani, kama hakutakuwa na changamoto yoyote, miradi yote itakamilika na wananchi watanufaika na tatizo la maji litakuwa halipo tena," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema kuna tatizo limejitokeza la upatikanaji wa vifaa ambavyo huagizwa kutoka nje ya nchi na kumekuwa na ucheleweshaji wa utoaji wa vifaa katika Bandari ya Malindi, Zanzibar.

Kutokana na tatizo hilo, aliliomba Shirika la Bandari Zanzibar kuharakisha utoaji wa mizigo inapofika bandarini hapo hasa kwa meli ambazo zimebeba makontena yenye vifaa vya miradi ya maendeleo.

"Nitaenda kuwasiliana na wenzetu wa bandari waruhusu vifaa vilivyoko bandarini ambavyo vinahitajika kutumika katika miradi ya maendeleo ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati," alisema.

Pia alisema kuna changamoto ya wananchi kuvamia maeneo ya maji kwa ajili ya ujenzi wa makazi wakati maeneo hayo serikali imeshayalipia fidia kwa ajili ya upitishaji wa mabomba ya maji.

Alitaka Serikali ya Wilaya ya Magharibi B Unguja, kubomoa maeneo ya maji yaliyovamiwa likiwamo la Kidundani Kwarara ili kupitisha miundombinu ya maji. Alisema miradi hiyo ya ujenzi wa matangi 15 ya kuhifadhia maji, itagharimu dola milioni 92.18 na kwamba tangi moja lina uwezo wa kuhifadhi zaidi ya lita milioni 14.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Maji Zanzibar, Mudriki Fadhil Abbas, alisema miradi hiyo itawanufaisha Wazanzibari, hivyo akawataka wananchi kulinda miundombinu ili kukamilisha miradi hiyo.

Alisema wakati miradi hiyo ya maji inaendelea hali ya upatikanaji wa maji Zanzibar ni asilimia 50 hivyo kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza kufikia asilimia 80.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Joseph Kilangi (wa pili kushoto), akiongoza watendaji wake kupanda juu ya tangi la kuhifadhia maji wakati akikagua miradi ya majisafi na salama, Dimani, Wilaya ya Magharib B, Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Samia kuanika matokeo sensa mwisho wa mwezi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kutoa taarifa rasmi ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika Agosti 23, mwaka huu, ifikapo Oktoba 30 katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makazi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika kikao kazi kilichofanyika ukumbi wa Hoteli Verde, Mtoni kisiwani Unguja.

Alisema katika hafla hiyo, makundi mbalimbali yanatarajiwa kualikwa wakiwamo viongozi wastaafu, viongozi wa dini, vyama vya siasa, mashirika binafsi na wageni kutoka nchi mbalimbali.

Alisema kukamilika kwa Sensa ya Watu na Makazi, kumechangiwa na miongozo iliyokuwa ikitolewa na viongozi wakuu wa nchi.

Majaliwa alisema kamati imeridhishwa na taarifa za matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi ambayo imeonyesha asilimia 98 ya Watanzania wamehesabiwa.

Kwa mujibu wa Majaliwa, Watanzania wengi waliona umuhimu wa kuhesabiwa na kutoa ushirikiano mkubwa kwa makarani, hali ambayo itairahisishia serikali kufikia malengo iliyojiwekea kwa wananchi.

Pia alisema asilimia mbili iliyobakia ni ya wale ambao hawakuhesabiwa kutokana na mazingira ya kutatanisha waliyokuwa nayo.

Hata hivyo, alisema watu hao bado wanakwenda kazi ofisi za serikali za mitaa kwa lengo la kuhesabiwa ingawa muda wake umeisha.

Naye Mwenyekiti mwenza wa kamati hiyo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema haikua kazi rahisi kukamilisha sensa na kwamba kazi hiyo ilipita katika changamato tofauti lakini kupitia hekima na busara za viongozi pamoja na ushirikiano wa wananchi, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Hemed aliwashukuru Watanzania wote na wadau walioshiriki katika jambo hilo ambalo litairahisishia serikali kuwaletea wananchi maendeleo endelevu.

# Bodi Shirika la Nyumba yatwishwa mzigo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, ameitaka Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) kulisaidia shirika hilo katika utekelezaji wa majukumu yake ili lengo la serikali la makazi kufikiwa.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua bodi hiyo katika ofisi za wizara, Maisara visiwani hapo.

Waziri huyo alisema Zanzibar kuna maendeleo ya makazi lakini bado haijaonekana katika shirika hilo, hivyo ni lazima kuhakikisha bodi inasaidia kwa nguvu zote ili lengo la serikali la kuboresha makazi kwa wananchi kufikiwa.

Alisema serikali inatumia kila mbinu na jitihada chini ya wizara ili kuhakikisha wananchi wanapata makazi bora Unguja na Pemba.

Pia alisema shirika hilo lina changamoto nyingi, hivyo uwapo wao utasaidia katika kuzitatua na ushirikiano wao utalipeleka mbele shirika ili kupata maendeleo.

Waziri Rahma alisema bodi hiyo imeanzishwa kisheria na kuamini kila jambo lake litafuata sheria hasa katika uendeshaji wa vikao vyao.

Alisema shirika hilo linatakiwa kutoa tija kwa serikali na tayari wawekezaji wameshajitokeza kutaka kuwekeza katika eneo hilo hasa la ujenzi wa nyumba za makazi.

Rahma alisisitiza ushirikiano kwa kuwa kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiuza nyumba za shirika na kuzifanya mali yao, hivyo ni vyema kuwasaidia ili kupunguza changamoto hiyo.

Naye Naibu Katibu wa Wizara hiyo, Mzee Ali Haji, alisema lengo kubwa la shirika hilo ni usimamizi wa taasisi na miongozo iliyoko na dhamana kubwa ya shirika hilo ni kusimamia nyumba za maendeleo ambapo ni mustakabali mzima wa kuimarisha maendeleo ya makazi Zanzibar.

Alisema ni imani yake kwamba bodi hiyo itayafanyia kazi maagizo iliyopewa hasa katika suala la kutunza siri za shirika.

Mkurugenzi Mkuu ZHC, Mwanaisha Ali Said, alisema shirika lina nyumba 2,046 Unguja na Pemba zikiwamo nyumba za maendeleo, vijiji na za Mji Mkongwe.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2022/23, shirika hilo lina mpango wa kuanza ujenzi wa jengo la biashara na makazi Pemba na Mombasa kwa Unguja, kuanzisha matengenezo ya nyumba 68 za maendeleo zikiwamo 48 za Unguja na Pemba 20 zinazomilikiwa na shirika hilo.





# Mimba za wanafunzi Shy zamchefua mkuu wa wilaya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amekemea mimba za utotoni katika wilaya yake na kusema hataki kusikia mwanafunzi wa kike amepata ujauzito wala kuozeshwa ndoa ya utotoni.

Mboneko alisema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, ambayo yalifanyika kimkoa katika Shule ya Sekondari Mazinge yaliyokwenda sambamba na ugawaji wa taulo za kike kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Alisema mimba na ndoa za utotoni zimekuwa kikwazo kwa wanafunzi wa kike kutimiza ndoto zao na kuwaagiza wakuu wa shule, maofisa elimu ngazi zote na watendaji, kuhakikisha wanawawafuatilia wanafunzi na kuwashughulikia watu ambao wanawarubuni pamoja na wazazi wanaotaka kuwaozesha.

**Shule hiyo ina wanafunzi 854, na kuishukuru serikali na wadau kuendelea kutatua matatizo ambayo yanaikabili sekta ya elimu.**

"Katika wilaya yangu sitaki kusikia mtoto wa kike amepata ujauzito wala kuozeshwa ndoa ya utotoni. Nataka wasome hadi wafike vyuo vikuu ili taifa tupate wataalamu wetu wakiwamo madaktari, wahandisi, walimu na viongozi mbalimbali," alisema Mboneko.

Pia aliwataka wanafunzi wasome kwa bidii na kuacha kujiingiza kwenye mambo ambayo yataharibu uelekeo wa maisha yao pamoja na kutoa taarifa kwa viongozi juu ya watu ambao wanawarubuni au mzazi kutaka kumwozesha, ili serikali ishughulike nao ili kuokoa ndoto zao.

Katika hatua nyingine, Mboneko alikemea utoro kwa wanafunzi wa kike katika shule hiyo kwa sababu ya ukosefu wa taulo za kike. Wanafunzi wote 433 waligawiwa taulo hizo kutoka Taasisi ya Flaviana Matata na watazitumia hadi siku ya kufunga shule.

Mmoja wa wanafunzi wa kike wa shule hiyo, Clara Joseph, alishukuru kupewa taulo hizo ambazo alisema itawasaidia kuhudhuria vipindi vya masomo wanapoingia katika hedhi sababu wana vifaa tayari vya kujistiri.

Mkuu wa Shule hiyo, James Msimba, alisema shule hiyo ina wanafunzi 854, na kuishukuru serikali na wadau kuendelea kutatua matatizo ambayo yanaikabili sekta ya elimu.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (katikati), akionyesha taulo za kike pamoja na wanafunzi wasichana wa Shule ya Sekondari Mazinge, Manispaa ya Shinyanga juzi, baada ya kuwagawia taulo hizo zilizotolewa na Flaviana Matata Foundation, kwa ajili ya kuwastiri katika hedhi ili wasikose vipindi vya masomo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wenye ulemavu watengewa shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imetenga Shule ya Msingi Mwime iliyoko Kata ya Zongomela kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu mkubwa.

Hatua hiyo itawawezesha wanafunzi hao kusoma kwa uhuru na kuzitimiza ndoto zao kama walivyo wanafunzi wengine.

Shule hiyo inatarajiwa kuanza na wanafunzi 140 wenye ulemavu mkubwa kati ya wanafunzi walemavu 300 walioko manispaa hiyo kutoka kata 20 na itafuguliwa mwishoni mwa Desemba, mwaka huu.

Ofisa Elimu, Elimu Maalumu wa Manispaa hiyo, Agnes Ntalimbo, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake na kutoa taarifa ya kutenga moja kati ya shule zilizoko kuwa shule ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuhakikisha hawakatishi masomo yao.

Alisema kati ya hao wanafunzi 140 wenye ulemavu mkubwa wa viungo, sita ni wenye ualbino, 35 wenye ulemavu wa kusikia (viziwi), 29 wenye ulemavu wa akili, 39 ulemavu wa viungo, 25 uoni hafifu. Pia mmoja ana usonji na watano wanafunzi wasioweza kuongea (mabubu).

Kuhusu walimu katika shule hiyo, Ntalimbo alisema, mpaka sasa wana walimu wanane wenye taaluma ya kuwafundisha wanafunzi hao, wawili ni wa kike na sita wa kiume.

Pia alisema wanafunzi wenye ulemavu wa kawaida wataendelea kusoma mchanganyiko pamoja na wanafunzi wasiokuwa na ulemavu na kwamba shule hiyo ili iwe na walimu wa kutosha, wanahitajika walimu 30 lakini kwa sasa wataanza na wanane walioko.

# Wanafunzi wa kike waomba miundombinu kumudu sayansi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imeombwa kufanya maboresho ya miundombinu ya kujifunzia mazoezi kwa vitendo pamoja na kuongeza walimu wa masomo ya sayansi shuleni ili kuwapa fursa watoto wa kike kujifunza masomo hayo kwa weledi ili kufikia ndoto zao.

Wakizungumza na Nipashe wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike juzi, wanafunzi hao wakieleza uhaba wa walimu wa sayansi pamoja na miundombinu ndicho chanzo cha wao kushindwa kufikia malengo yao.

Katika maadhimisho hayo, wanafunzi wa kike mkoani Mwanza walisema kuwapo kwa miundombinu na walimu wa kutosha wa masonmo ya sayansi, kutawasaidia kuongeza uwezo wao na ufaulu.

Wanafunzi hao walitembelea Hospitali ya Bukumbi iliyoko wilayani Misungwi kujifunza kwa vitendo kupitia mradi wa Chomoza Stem chini ya Shirika lisilo la kiserikali la Adilisha.

Asia Abdallah, mwanafunzi wa kidato cha tatu kutoka Shule ya Sekondari Buhongwa, alisema licha ya yeye kupenda masomo ya sayansi, bado miundombinu katika shule yao si rafiki.

Alisema maabara zilizoko shuleni hapo ni vyumba vya kawaida na hazina vifaa vya kutosha kufanyia mazoezi, hivyo kuwafanya washindwe kufanya mazoezi kwa vitendo.

"Tunawashukuru Adilisha kwa juhudi zao za mara kwa mara kwetu wanafunzi wa kike katika kuhakikisha tunasoma masomo ya sayansi ila katika upande wa miundombinu tunaomba serikali iweke mkono wake ili tufike mbali zaidi," alisema Asia.

Naye Sada Tabu, mwanafunzi wa kidato cha nne Buhongwa, mwenye ulemavu wa ngozi, alisema uchache wa walimu wa masomo ya sayansi ni kikwazo katika kufikia malengo yao ya kuwa wanasayansi.

"Unaweza kukuta walimu wawili tu wanatufundisha somo moja la sayansi kwa madarasa yote mpaka mnashindwa kupata muda mzuri wa kufanya nao mazoezi ya vitendo," alisema Sada.

Aidha, Sada aliiomba serikali kuajiri zaidi walimu wa sayansi ili kuongeza ufanisi kwa wanafunzi katika masomo ya sayansi.

Akizungumza na Nipashe, Sarah Lulandala, daktari mfawidhi katika Hospitali ya Bukumbi alisema watoto wa kike hushindwa kufikia malengo yao kutokana na kutokujiamini pamoja na imani potofu za baadhi ya familia kuwa mtoto wa kiume ni bora zaidi ya wa kike.

"Tunawahimiza watoto wa kike kujiamini na kusoma masomo ya sayansi ili baadaye tuwe na wanasayansi wanawake wa kutosha nchini na duniani kwa ujumla," alisema.

Mwanaidi Omarym Mratibu wa Klabu ya Chomoza Stem kutoka Adilisha, aliieleza Nipashe kuwa licha ya serikali kuweka juhudi katika kukuza kiwango cha elimu nchini, bado wadau wa elimu wana nafasi ya kubuni njia za kutatua changamoto za watoto wa kike katika kufikia malengo yao.

Siku ya mtoto wa kike huadhimishwa kimataifa Oktoba 11 kila mwaka na kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa 'Haki Zetu Hatima Yetu, Wakati ni Sasa'.

## HABARI KIMATAIFA

# Russia yazidi kuivuruga Ukraine

**MOSCOW, Russia**

WAKATI kundi la nchi tajiri duniani G7 wameahindi kuiunga mkono Ukraine, Russia imesisitiza haitarudi nyuma na mashambulizi yake na kwamba hatua zitakazochukuliwa tayari walizitarajia.

Katika kikao chao cha jana, kundi hilo la G7 walikubaliana kuongeza vikwazo kwa Russia, sambamba na kuisaidia Ukraine kifedha na silaha.

Msemaji wa Ikulu ya Russia, Dmitry Peskov, aliwaambia waandishi wa habari kwamba hali ya mbeleni inatabirika na makabiliano yataendelea.

Aliongeza kwamba nchi yake itafikia malengo yake iliyojiwekea nchini Ukraine. Hatua hiyo imeenda sambamba na Russia kuikosoa Marekani kutokana na ahadi yake ya kuipatia Ukraine msaada zaidi wa kijeshi, hususan ya mifumo ya ulinzi wa anga.

Katika hatua nyingine, Russia imerusha ndege zingine zisizokuwa na rubani katika anga la mikoa kadhaa ya Ukraine na mamlaka ya miji kadhaa imeripoti kuzuka kwa mashambulizi mengine karibu na mji mkuu Kyiv na hakuna vifo wala majeruhi walioripotiwa mpaka jana.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amezitaka nchi za Magharibi kuiwekea Russia vikwazo zaidi ili kukabiliana na kile alichokiita wimbi jipya la ugaidi baada ya mashambulizi ya Jumatatu dhidi ya nchi yake.

Watu 19 waliuawa na wengine wengi kujeruhiwa huku makombora yakipiga maeneo tofauti nchini.

Kufuatia mashambulizi zaidi siku ya Jumanne, Zelensky alitoa wito kwa nchi za Magharibi kutafuta njia mpya za kutumia shinikizo la kisiasa kwa Russia na kuunga mkono Ukraine. Wito huo unakuja baada ya mkutano wake na viongozi wa mataifa saba tajiri zaidi duniani G7 kwa mazungumzo ya dharura.

G7- ambayo inajumuisha Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan, Uingereza na Marekani, iliahidi kuendelea kutoa msaada wa kifedha, kibinadamu, kijeshi, kidiplomasia na kisheria kwa nchi yake kwa muda mrefu iwezekanavyo.

Zelensky alisema kwa wimbi jipya la ugaidi lazima kuwe na wimbi jipya la uwajibikaji kwa Russia.

"Serikali ya kigaidi lazima inyimwe hata mawazo kwamba wimbi lolote la ugaidi linaweza kuleta chochote," alisema Zelensky.

Rais wa Russia, Vladimir Putin alisema mashambulizi hayo yalikuwa ya kulipiza kisasi milipuko wa Jumamosi kwenye daraja muhimu linalounganisha Russia na Crimea.

Nchi za Magharibi tayari zimeweka vikwazo dhidi ya biashara za Russia na washirika wa Rais Putin tangu uvamizi wa Ukraine mwezi Februari.

**WALIOLIPUA DARAJA WAKAMATWA**

Russia ilisema inawazuia watu wanane kuhusiana na mlipuko uliotokea kwenye daraja muhimu linalounganisha Urusi na Crimea.

Idara yake ya usalama ya FSB ilisema watano kati ya waliokamatwa ni Warussia, huku wengine wakiwa ni raia wa Ukraine na Armenia.

FSB imeshutumu idara za usalama za Ukraine kwa kuhusika na shambulio hilo.

Hayo yanajiri huku milipuko yakiripotiwa kutokea katika miji ya Kherson, Zaporizhzhia na Nikopol Ukraine.

Mwandishi wa BBC aliyeko Kyiv, Hugo Bachega alisema milipuko mitano imesikika huko Kherson, mojawapo ya miji mikubwa inayokabiliwa na uvamizi wa Russia, huku kukiwa na ripoti ambazo hazijathibitishwa kuwa mfumo wa ulinzi wa anga katika mji huo umeanzishwa.

Alisema haijabainika ni nini kilisababisha milipuko hiyo.

Mlipuko huo kwenye Daraja la Crimea ulikuwa pigo kubwa kwa Rais wa Urusi Vladimir Putin, ambaye alilifungua 2018, miaka minne baada ya Urusi kunyakua Crimea.

Rais Putin alikiita kitendo cha kigaidi, akisema vikosi vya kijasusi vya Ukraine vilikuwa na lengo la kuharibu kipande muhimu cha miundombinu ya kiraia ya Russia.

**UN YAONYA KUONGEZEKA WAKIMBIZI**

Mkuu wa shirika la kuwashughulikia wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) Filipo Grandi, ameonya kuongezeka kwa idadi ya watu wanaolazimika kukimbia makazi yao nchini Ukraine baada ya Russia kuvurumisha makombora katika mji wa Kyiv na miji mingine.

Grandi, alisema hali ya ukatili inayotokea Ukraine hausameheki, na kuwa mashambulizi ya raia, majumba na miundombinu isiyo ya kijeshi katika namna isiyochagua, inazidi kuwa vigumu kwa raia.

**BBC**


MWANGA HAKIKABANK

MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 15,000.00 | 7,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 60,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| New ATM Card | 15,000.00 |
| Replacement of lost/demaged ATM cards OR ID | 15,000.00 |
| ATM PIN Reset | 5,000.00 |
| Annual ATM Mantainance Fee | 1,000.00 |
| ATM Balance enquiry | 200 |
| ATM Min statement | 300 |
| ATM withdrawal fee per transaction | 1,300.00 |
| Uncollected Destroyed ATM Card | 4,000.00 |
| Internet Banking Monthly fee | 3,000.00 |

AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquire | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| Up to 50,000 | 850.00 |
| 50,000 - 100,000 | 1,000.00 |
| 100,000 - 300,000 | 2,000.00 |
| 300,000 - 500,000 | 3,500.00 |
| 500,000 - 1,000,000 | 4,500.00 |
| 1,000,000 - 3,000,000 | 6,000.00 |
| 3,000,000 - 5,000,000 | 10,000.00 |

MOBILE BANKING CHARGES

WITHDRAWAL CHARGES

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 50,000.00 | 1,500.00 |
| 50,001.00 | 100,000.00 | 2,000.00 |
| 100,001.00 | 250,000.00 | 3,000.00 |
| 200,001.00 | 750,000.00 | 5,000.00 |
| 750,001.00 | 3,000,000.00 | 7,000.00 |
| 3,000,001.00 | 5,000,000.00 | 10,000.00 |

EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

| FUND TRANSFER CHARGES | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

CUSTOMERS COMPLAINTS REDRESSAL MECHANISM

One of our core values is Customer Focus and we always strive to put satisfaction of our customers first. However, there could be instances when you are dissatisfied with our services as the same did not meet your expectations or that our services were deficient, then you can lodge your complaint as given below:

1. Meet the Branch Manager and lodge your complaint orally or in writing.
2. Drop your complaint in the suggestion Box provided at the branch
3. Email: info@mhbbank.co.tz
4. You can also email directly to the following senior officers
   - Managing Director at info@mhbbank.co.tz
   - Director of Business Development at info@mhbbank.co.tz
   - Senior Operations Manager at operation@mhbbank.co.tz
   - Head of Shared Services at info@mhbbank.co.tz; operation@mhbbank.co.tz
5. P.O.BOX 11735 Dar es Salaam, Tanzania
6. Call us on +255 747 666 511

Sasa ni Commercial Bank
Tunajivunia Mafanikio yetu.

Sasa Unaweza Pakua MHB App!
Available on the Google Play
Download on the App Store

+255 747 666 511 www.mhbbank.co.tz info@mhbbank.co.tz @mhbbank

217090102


# Uganda, Mali kusaidiana kijeshi

**KAMPALA, Uganda**

NCHI za Uganda na Mali zimekubaliana kushirikiana kwenye mafunzo ya majeshi, ukusanyaji wa taarifa za kijasusi, operesheni za anga na ardhini pamoja na mapambano dhidi ya waasi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotangazwa na jeshi la Uganda hapo juzi, Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo, Vincent Ssempijja na mwenzake wa Mali, Kanali Sadio Camara, walisaini makubaliano hayo mjini Kampala.

Ssempijja alisema Uganda ina hamu ya kuingia kwenye ushirikiano wa kiulinzi kwa imani ya udugu wa Kiafrika na kuimarisha usalama wa bara hilo.

Kanali Kamara kwa upande wake alisema Mali itafaidika na utaalamu wa jeshi la Uganda.

**DW**

# Kanye afungiwa Twitter, Instagram

**LOS ANGELES, Marekani**

RAPA mtukutu wa Marekani, Kanye West, amefungiwa kutumia mitandao ya kijamii ya Twitter na Instagram baada ya kutuma ujumbe wa chuki dhidi ya Wayahudi.

Mwishoni mwa wiki, Instagram iliifungia akaunti ya Kanye baada ya kumshutumu rapa na mjasiriamali, Sean Combs (P.Diddy) kwa kudhibitiwa na baadhi ya "Mayahudi wenye nguvu", bila kuwataja majina.


Kanye alijibu kufungiwa huko kwa kujitokeza tena kwenye ukurasa wake wa Twitter, ambao aliacha kuutumia miaka miwili iliyopita, akisema kwamba sasa atawasha "Njia ya kifo" dhidi ya Wayahudi.

Mitandao yote ilifuta machapisho yake na kusema kuwa alikiuka kanuni ya uchochezi, ubaguzi wa rangi na chuki za kidini.

Matukio hayo yametokea baada ya Kanye kuibua hasira za wanaharakati wa haki za watu weusi kwa kujitokeza katika Wiki ya Mitindo ya Paris akiwa amevalia fulana iliyoandikwa "White Lives Matter" akitetea haki za wazungu na kuzihaki ile inayotetea haki za watu Weusi.

Maneno hayo yalionekana kama dhihaka ya kaulimbiu ya ubaguzi wa rangi dhidi ya Weusi ya "Black Lives Matter".

West, ambaye hivi karibuni alibadili jina na kujiita "Ye", alikuwa akionyesha mkusanyiko wake wa mavazi huko Paris, ulioonyeshwa na mwanamitindo, Sela Marley ambaye ni mjukuu wa gwiji wa muziki wa rege duniani, Bob Marley.





# BURNA BOY AJIMWAGA NA BEYONCE

**PARIS,** Ufaransa

MSANII maarufu wa muziki kutoka nchini Nigeria, Burna Boy alionekana kwenye pati binafsi ya nyota wa muziki duniani, Beyonce iliyofanyika jijini Paris nchini Ufaransa.

Katika picha ambayo imesambaa kwenye mitandao ya kijamii kuanzia jana inamuonyesha Burna Boy akimkumbatia Beyonce ambapo ni watu wachache pekee walialikwa kwenye pati hiyo, hasa kutoka Afrika.

Hii si mara ya kwanza kwa Burna Boy kuwa karibu na Beyonce.

Kwani itakumbukwa katika Albamu ya 'Soundtracks' inayopatikana kwenye Filamu ya The Lion King (2019), iliyofanywa na Beyonce, miongoni mwa wasanii walioshirikishwa ni Burna Boy.

Mbali na Burna Boy, Beyoncé pia aliwaalika wasanii kadhaa kutoka Afrika, ambao ni Wizkid, Mr Eazi, Yemi, Shatta Wale, Busiswa, Tiwa Savage na Tekno.

Mashabiki wengi wa Burna Boy baada ya kuonekana kwa picha hiyo, waliandika kutaka wawili hao kufanya kolabo ya wimbo angalau mmoja.

# *Konde Gang yawatupa Killy, Cheed*

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa lebo ya muziki ya Konde Gang umetoa taarifa kwa umma kuweka wazi makubaliano ya kusitisha mikataba na Wasanii wao wawili waliokuwa chini yao, Killy na Cheed.

Barua hiyo iliyochapishwa kupitia kurasa za mitandao ya kijamii za Konde Gang ilisomeka hivi:

"Uongozi wa Konde Music Worldwide unachukua fursa hii kuutaarifu umma leo (juzi, 10/10/2022), tumefikia makubaliano na wasanii tajwa hapo chini ya kusitisha mikataba kutokana na sababu mbalimbali zilizopo nje ya uwezo wetu.

"Ally Kili Omary a.k.a (Killy), Rashid Daudi Mganga a.k.a (Cheed), Wasanii hawa watakuwa huru na kuweza kufanya kazi na kuingia mikataba na kundi au mtu yeyote na kuendeleza kazi zao. Kwani tunaamini ni vijana na wasanii wenye uwezo mkubwa wa kufanikiwa katika safari ya muziki.

"Aidha, Konde Music Worldwide haitahusika na jambo lolote litakalohusisha wasanii hawa kuanzia tarehe tajwa hapo juu.

"Tunapenda kuwashukuru Killy na Cheed kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha kuwa pamoja na tunawatakia mafanikio mema katika kazi zao hapo baadaye."



HABARI MICHEZO

# EUNIC YAFUNGUA FURSA KWA WASANII TANZANIA

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI za Kitaifa za Utamaduni za Umoja wa Ulaya (EUNIC), kupitia Mradi wa Ruzuku ya Nafasi za Utamaduni za Ulaya (UMOJA), imezindua 'Makazi ya Msanii' yatakayo wakutanisha wasanii kutoka Afrika Mashariki na Ulaya kwa wiki tano nchini.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo jijini Dar es Salaam jana, Balozi wa Hispania nchini, Jorge Sanchez, alisema makazi hayo yaliyoanza juzi, lengo lake ni kuimarisha uhusiano kati ya wasanii kutoka Tanzania, Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya kupitia kazi zao za kibunifu.

Alibainisha kuwa mradi huo unakuza ushirikiano wa kisanii, elimu bora, ushirikiano wa kibinafsi na umma, mtandao na kukuza masoko ya kimataifa. Pia, unatoa ajira na ukuaji wa uchumi kwa wadau pamoja na mafunzo ya usimamizi wa sanaa na utamaduni kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mkuu wa Ujumbe wa Umoja wa Ulaya (EU), Emilio Rosseti, alisema mradi wa UMOJA unaamini kwamba ushirikiano huleta uvumbuzi, uelewa wa kitamaduni na kuinua uchumi wa ubunifu.

Aidha, alisema mpango huo utasaidia kufungua mazungumzo ya kitamaduni kati ya wasanii wa Afrika Mashariki na Ulaya pamoja na kukuza usawa wa kijinsia na mshikamano wa kijamii kupitia ngoma, muziki na sanaa ya kuona.

Alisema EU imekuwa ikisaidia matukio ya kitamaduni katika sehemu mbalimbali ili kukuza ushirikiano wa tamaduni kupitia sanaa na imejipanga kuendelea kushirikiana na sekta ya utamaduni nchini Tanzania.

Msimamizi wa Mradi huo, Germaine Sigoda, alisema jumla ya wasanii 14 watakusanyika kwenye makazi hayo na kufanya maonyesho ya moja kwa moja Oktoba 29 na Novemba 12 , mwaka huu, katika kumbi za Nafasi Artspace na UDSM Idara ya Sanaa Bunifu, na hakutakuwa na kiingilio chochote kwa matukio hayo na kwamba kila mtu anakaribishwa.

Aidha, Sigoda alilishukuru Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), kwa kuwapa ushirikiano wakati wote na anaamini kuwa makazi hayo yatakuza vipaji vya sanaa kwa wasanii hao.

Mmoja wa washiriki kutoka Tanzania, Tadhi Alawi alisema anajivunia kupata fursha ya kuonyesha kazi yake ya sanaa yenye kuelimisha na kuburudisha jamii yake, pia ni fursa kubwa kwa upande wake kwa sababu itamtambulisha kitaifa na kimataifa.

**MBUNI FC...**



Wachezaji wa Timu ya Mbuni FC, inayoshiriki Ligi ya Championship Tanzania Bara, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana, kujiandaa na mchezo wa ligi hiyo dhidi ya African Sports ya jijini Tanga. Mbuni FC ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 12 baada ya kushinda mechi zote nne za kwanza.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Morocco aita 27 kuivaa Nigeria

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 23, Hemed Morocco, ametangaza wachezaji 27 watakaoingia kambini leo kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika kwa umri huo dhidi ya Nigeria.

Timu hiyo ambayo hivi karibuni iliiondosha Sudan Kusini kwenye mechi ya awali ya michuano hiyo, kwa sasa inakabiliwa na kibarua cha kuiondosha Nigeria ili kufuzu fainali hizo.

Vijana hao watacheza mechi ya kwanza nchini kati ya Oktoba 21 hadi 23 kabla ya kurudiana Oktoba 29, mwaka huu.

AFCON hiyo ya vijana chini ya umri huo inatarajiwa kufanyika Juni mwakani nchini Morocco.

Tayari timu ya Nigeria chini ya umri huo, 'The Dream Team' iliingia kambini wiki iliyopita chini ya Kocha Mkuu, Salilu Yusuph ikiwa na wachezaji 32.

Hemed aliwataja makipa watatu ambao ni Aboutwalib Mshery kutoka Yanga, Arjif Ally Amour kutoka Chipukizi na Zuberi Masoud Foba kutoka Azam FC.

Mabeki ni David Kameta wa Mtibwa Sugar, Alphonce Mabula (FK Spartak Subotica-Serbia), Pascal Msindo (Azam), David Bryson (Yanga), Haji Mnoga (Gillingham- England), Abdulrazack Hamza (Namungo), Twalib Mohamed (Azam), Twalib Mohamed (Azam), Mukrim Issah Abdallah (JKU), Hatibu Kombo (Coastal Union), Dickson Mhilu (Kagera Sugar) na Abdulmalik Zacharia kutoka Namungo.

Upande wa viungo walioitwa ni Novatus Dismas (Zulte Waregem- Ubelgiji), Ally Msengi (Moroka Swallows-Afrika Kusini), Edmund John (Geita Gold), Tepsi Evance (Azam FC), Abdul Suleiman 'Sopu' (Azam FC), Vicent Aboubakar (Coastal Union), Yusuph Jamal (Coastal Union), Mundhir Abdallah Vuai (Kipanga FC), na Khalid Habib Idd wa KMKM.

Kwa upande wa washambuliaji ni Kelvin John (Genk -Ubelgiji), Annuary Jabir (Kagera Sugar), Oscar Paul (Prisons) na Clement Mzize (Yanga).

## Simba Queens na ubani CAF Iringa

**Na Saada Akida**

SIMBA Queens imeonyesha kwamba imedhamiria kufanya kweli na kuipeperusha vema bendera ya Taifa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake inayotarajiwa kuanza Oktoba 30, mwaka huu nchini Morocco baada ya kutangaza kwenda kujichimbia mkoani Iringa.

Simba Queens inatarajia kuondoka nchini Oktoba 25, mwaka huu na itakuwa na kibarua kigumu katika mchezo wa kwanza dhidi ya wenyeji wa michuano hiyo, ASFAR utakaopigwa Oktoba 30, mwaka huu nchini humo.

Katika michuano hiyo itakayoanza Oktoba 30 hadi Novemba 13, mwaka huu nchini Morocco, Kikosi cha Simba Queens ambacho kinawakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kipo Kundi A na timu ya ASFAR (Morocco), Green Buffaloes (Zambia) na Determines Girls ya Liberia.

Kundi B linaundwa na mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Bayelsa Queens (Nigeria), Wadi Degla ya Misri na mwakilishi wa Ukanda wa UNIFFAC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Erasssy, alisema maandalizi yanaendelea na tayari kikosi chao kipo mkoani Iringa kikiendelea kujiweka imara na Ligi ya Mabingwa Afrika na kesho, Ijumaa kitacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Ceasiaa Queens FC.

## Chipukizi yazidi kuwika ugenini

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Chipukizi FC imeendelea kutamba ugenini Kisiwani Unguja kwa kupata alama sita katika michezo miwili iliyocheza kisiwani hapa.

Chipukizi FC tayari imecheza michezo miwli kati ya mitano inayotakiwa kucheza ikiwa Kisiwani Unguja kabla ya kurejea Pemba.

Katika michezo hiyo mzunguko wa sita iliifunga timu ya JKU bao 1-0, wakati mchezo wake wa saba juzi iliwafunga Maafande wa Mafunzo mabao 2-1, ambao uliochezwa Dimba la Amaan majira ya saa 10 alasiri.

Akizungumza na gazeti hili juzi huku akiwa na furaha tele ya ushindi, Kocha wa timu ya Chipukizi FC, Ali Bakari 'Mngazija', alisema ushindi wa mechi mbili mfululizo umetimiza robo ya malengo yake ya kufanya vizuri katika michezo ya ugenini.

Alisema ushindi huo mfululizo umezidi kuongeza hamasa kubwa kwa wachezaji kuhakikisha wanaweza kufanya zaidi katika michezo mitatu iliyobaki.

"Tumetimiza robo ya lengo letu la kuhakikisha tunatumia vema uwanja wa ugenini kwa kupata alama tatu, tumefanikiwa mechi mbili sasa tunaendelea kujipanga kuhakikisha mechi tatu zilizobaki tunashinda tena," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE EURO MIL. 350

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe atagharimu kati ya Euro milioni 300 hadi milioni 350 kama klabu yoyote itataka kumnunua, ingawa Paris St-Germain hawana nia ya kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 baada ya ripoti kuibuka kwamba anataka kutimka katika dirisha la Januari. ***(Telegraph)***

### HAALAND KWA EURO MIL. 200

MKATABA wa mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22, una kipengele cha kuuzwa kwa euro milioni 200 ambacho kitaanza msimu wa majira ya joto wa mwaka 2024. Meneja Pep Guardiola aliwahi kusema mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway hakuwa na kipengele hicho kwa ajili ya "Real Madrid au timu nyingine yoyote" lakini kifungu hicho kinatumika kwa klabu yoyote nje ya Uingereza. ***(Athletic)***

### SPURS WAMTAKA TONEY

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney wakiwa wanamtazama mara kwa mara mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### MOUNT MKATABA MPYA

CHELSEA wameanza mazungumzo na kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 23, kuhusu mkataba mpya. ***(Standard)***

### ZAKARIA KURUDI CHELSEA

CHELSEA wanataka kusitisha mkataba wa mkopo wa kiungo wa kati wa Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 25, kutoka Juventus Januari, na wako tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya winga, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29. ***(90min)***

### FAMILIA KUMWAMULIA SILVA

MLINZI wa kati wa Brazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 38, amesema familia yake itaamua iwapo ataongeza mkataba Chelsea, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Standard)***

### DALOT ATAKIWA JUVE

JUVENTUS wanataka kumsajili mlinzi wa Manchester United, Diogo Dalot huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 23 akitaka kuondoka Old Trafford. (***Calciomercato***)

### UMTITI KUUZWA JUMLA

BARCELONA wanakusudia kumuuza beki wa kati, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 28 katika majira ya joto. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwa sasa yuko kwa mkopo Lecce. ***(Sport)***

### CAMPOS KUONDOKA PSG

MSHAURI wa masuala ya michezo wa PSG, Luis Campos aliyejiunga na klabu hiyo Juni mwaka huu, anaweza kuwaacha mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1. ***(Le Parisien)***

### FOREST YAFUKUZA WAWILI

KLABU ya Nottingham Forest imewafuta kazi vigogo wawili wa usajili, George Syrianos na Andy Scott, baada ya uchunguzi wa matumizi ya fedha ya klabu hiyo katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Telegraph)***

### RICHARDSON ATAJWA BROM

KOCHA wa Wigan, Leam Richardson yuko kwenye orodha ya makocha wanaotajwa kuchukua mikoba pale West Brom, baada ya kufukuzwa kwa Steve Bruce. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AHISI KUSALITIWA PSG SASA KUSEPA JANUARI

●●● Tulijua kulikuwa na mvutano na sasa ameamua kuwa ataondoka, anaangalia dirisha la...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe anahisi "amesalitiwa" na Paris St-Germain na anataka kuondoka katika klabu hiyo Januari mwakani, kwa mujibu mwandishi na mchambuzi nguli wa michezo wa Ufaransa, Julien Laurens mwenye makazi yake jijini London, England.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa alisaini mkataba mpya wa miaka mitatu Mei mwaka huu, lakini sasa anahisi alifanya "kosa".

Mbappe, ambaye amefunga mabao 12 katika michuano yote msimu huu akiwa na PSG, angependa kuhamia Real Madrid.

Lakini Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Luis Campos, amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, "hajawahi kuzungumza chochote kuhusu kuondoka" klabuni hapo Januari.

Mbappe aliifungia PSG katika sare ya bao 1-1 na Benfica kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne usiku na kumfanya kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo kwenye mashindano hayo makubwa kwa ngazi ya Klabu Ulaya.

Akizungumza na BBC, Laurens alisema: "Mbappe anahisi kusalitiwa na klabu kwa maana kwamba mambo yote ambayo ilimuahidi aliposaini mkataba huo mpya hadi 2025 hayajafanyika.

"Ahadi kwamba wangesajili mshambuliaji mpya ili (yeye) aweze kucheza katika nafasi yake bora, Neymar kuuzwa, kusajili beki wa kati, na atakuwa katikati ya mipango ya timu, mambo yote haya hayajafanyika.

"Tulijua kulikuwa na mvutano na sasa ameamua kwamba ataondoka, anahisi alifanya makosa kwa kuongeza mkataba na alipaswa kuondoka wakati wa majira ya joto, sasa anaangalia dirisha la Januari la uhamisho ambapo anaweza kutimka."

Mbappe aliyeshinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, ametwaa mataji 11 akiwa na PSG, yakiwamo manne ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, tangu ajiunge nayo akitokea Monaco mwaka 2017.

Ijumaa, Jarida la Forbes lilimtaja kuwa anaongoza katika orodha ya wanasoka wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani- ikiwa ni mara ya kwanza mtu mwingine kuwa kwenye nafasi hiyo ukiacha Lionel Messi au Cristiano Ronaldo waliokuwa wanabadilishana namba moja kwa miaka tisa mfululizo.

"Ni wazi katika akili yake kuna kitu hakiko sawa kati yake na klabu," aliongeza Laurens.

"Real Madrid walikuwa tayari kuja msimu wa majira ya joto na kumsajili kama mchezaji huru. Ni lazima bado wanaweza kuwa na fedha za kumnunua na pia za mshahara."

Lakini, akizungumza baada ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya PSG dhidi ya Benfica, Campos alikanusha madai kwamba, Mbappe hayuko sawa pale Paris.

"Niko na Kylian Mbappe kila siku," alisema akikiambia Kituo cha Televisheni cha Ufaransa cha Canal Plus.

"Hajawahi kuzungumza nami kuhusu kuondoka Januari. Hizi taarifa hazitoki kwa mchezaji, ni (kutoka kwa vyombo vya habari), na kuwa na habari kama hii kwenye mechi kama hii ni mbaya sana. Ndiyo maana niko hapa, kukanusha na kusema wazi kwamba Kylian Mbappe hajawahi kuzungumza na mimi au kwa rais (Nasser Al-Khelaifi) kuhusu kuondoka PSG Januari."


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/-
1,039,5

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
OMONIA NICOSIA
1 | 1.12
X | 7.86
2 | 19.23

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POTTER: USHINDI WA CHELSEA NI BAHATI



**MILAN, Italia**

GRAHAM Potter alikiri kwamba, Chelsea ilipata "bahati kidogo" kwa kadi nyekundu ya Fikayo Tomori wakati wa ushindi wao wa mabao 2-0 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya AC Milan, nchini Italia, Jumanne.

Tomori alionyeshwa kadi nyekundu dakika ya 18 kwa kumchezea vibaya, Mason Mount, huku penalti ikitolewa na Jorginho akaipatia Chelsea bao la kuongoza.

Pierre-Emerick Aubameyang alifunga bao la pili muda mfupi baadaye na kuwafanya Chelsea kuwa kifua mbele.

Baada ya mchezo huo, Potter alionyesha kufurahia matokeo na alikiri kwamba, haikuwa rahisi bali ni bahati kidogo.

"Kuja hapa na kushinda hakika si rahisi, hiyo ni hakika," alisema Potter akiiambia BT Sport.

"Walikuwa wazuri sana. Tulipata bahati kidogo na wapinzani wetu walibakiwa na wachezaji kumi, lakini kwa ujumla walicheza vizuri."

Kuhusu tukio la kadi nyekundu, Potter aliongeza: "Ni vigumu kuona vizuri mahali nilipoketi. Inaonekana kama alikuwa ameweka mkono wake juu ya Mason Mount na kumzuia kufunga bao.

"Ninahitaji kuangalia tena kwa uwazi. Ni nzuri kwa penalti na nzuri kwa Jorginho kufunga. Ilikuwa hatua nzuri kuongoza. Ndivyo ilivyo. Wakati mwingine wanaenda kwa ajili yako.

"Ni jambo gumu. Unataka kudhibiti mchezo, lakini si kwa kupita kiasi. Kwa mazingira ya hapa, hatua moja inaweza kusababisha bao."

# Simeone hana mpango kuondoka Atletico

**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone wa Klabu ya Atletico Madrid amesisitiza kwamba, hana nia ya kuachia nafasi ya ukocha baada ya miaka 10 ya uongozi katika klabu hiyo.

"Siendi popote, nipo hapa," alisema. "Ninahisi nina usalama sawa na siku zote. Niliulizwa siku moja kama najiona mahali pengine na jibu langu lilikuwa hapana, kabisa.

"Ikiwa nitafikiria hivyo, ni kwa sababu ninaondoka, lakini sasa niko hapa. Natumaini kufikisha kile ninachohisi na ndio maana nimekuwa katika klabu hii kwa miaka mingi."



Simeone pia alikubali lawama kuhusu Joao Felix, huku mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22, akiwa bado hajafunga bao msimu huu.

"Kila kitu kibaya anachofanya Joao Felix nakifanya kibaya zaidi kwa sababu ni mimi ndio ambaye simpi anachohitaji ili kufikia uwezo wake," alisema.

"Hajabadilika hata kidogo, wachezaji wenzake anaoshindana nao ni bora na kocha analielewa hilo.

"Joao ni muhimu kwa klabu na kwa timu. Katika kampeni hii hajapata kitu muhimu zaidi kwake na hilo linamsumbua."

HABARI MICHEZO

594,915/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.15/10/22 | 19:00 | Torino vs Juventus | 3.11 | 3.11 | 2.37 |
| 02.15/10/22 | 19:30 | Mallorca vs Sevilla FC | 2.77 | 2.97 | 2.72 |
| 03.15/10/22 | 21:00 | GO Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.89 | 3.29 | 2.41 |
| 04.15/10/22 | 21:45 | Watford vs Norwich City | 2.64 | 3.24 | 2.64 |
| 05.15/10/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.45 | 3.23 | 2.88 |
| 06.15/10/22 | 22:00 | Cambuur vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.39 | 2.60 |
| 07.16/10/22 | 13:15 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 2.33 | 3.44 | 2.89 |
| 08.16/10/22 | 14:30 | Standard Liege vs Royal Antwerp | 2.95 | 3.45 | 2.30 |
| 09.16/10/22 | 15:00 | Celta Vigo vs Real Sociedad | 2.54 | 3.19 | 2.79 |
| 10.16/10/22 | 16:00 | Spezia vs Cremonese | 2.48 | 3.18 | 2.88 |
| 11.16/10/22 | 16:00 | Southampton vs West Ham | 2.79 | 3.38 | 2.44 |
| 12.16/10/22 | 16:00 | Troyes vs AC Ajaccio | 2.25 | 3.13 | 3.28 |
| 13.16/10/22 | 16:00 | Rennes vs Lyon | 2.26 | 3.51 | 2.92 |
| 14.16/10/22 | 17:00 | Hull City vs Birmingham | 2.50 | 3.20 | 2.85 |
| 15.16/10/22 | 17:15 | Real Madrid vs Barcelona | 2.42 | 3.45 | 2.77 |
| 16.16/10/22 | 17:45 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.43 | 3.48 | 2.74 |
| 17.16/10/22 | 18:30 | Union Berlin vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.38 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 13/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4726 | Welayta Dicha FC vs Ethiopia Electricity | 1.72 | 3.45 | 5.00 |
| 16:00 | 1906 | Coastal Union vs Geita Gold FC | 2.59 | 2.69 | 2.93 |
| 16:00 | 4669 | Sidama Bunna SC vs Saint George FC | 4.65 | 3.24 | 1.73 |
| 16:00 | 5858 | Kiyovu Sports vs Etincelles | 1.33 | 4.37 | 8.35 |
| 16:30 | 5147 | Gol Gohar vs Nassaji Mazandaran | 2.00 | 2.82 | 4.08 |
| 16:30 | 5550 | Persepolis FC vs MES Rafsanjan | 1.68 | 3.11 | 5.44 |
| 17:00 | 2049 | ES Metlaoui vs Sportive Zarzis | 2.01 | 3.32 | 3.32 |
| 17:00 | 2266 | ES Hammam Sousse vs ES Sahel | 3.31 | 2.77 | 2.29 |
| 17:00 | 3019 | Northeast United FC vs Hyderabad FC | 3.59 | 3.54 | 1.85 |
| 17:30 | 2444 | ES Setif vs USM Khenchela | 1.68 | 3.36 | 4.87 |
| 17:45 | 3389 | AL Arabi vs Al Fehaheel | 1.59 | 3.79 | 4.86 |
| 18:00 | 3557 | Foolad Khuzestan vs Peykan FC | 1.94 | 2.90 | 4.80 |
| 19:45 | 1615 | Fiorentina vs Hearts | 1.13 | 7.59 | 18.99 |
| 19:45 | 2248 | Betis vs Roma | 2.48 | 3.36 | 2.71 |
| 19:45 | 2508 | Nantes vs SC Freiburg | 3.50 | 3.40 | 2.04 |
| 19:45 | 2768 | Partizan vs FC Koln | 3.35 | 3.50 | 2.06 |
| 19:45 | 2951 | Basaksehir vs Rigas Futbola Skola | 1.23 | 5.79 | 11.99 |
| 19:45 | 3494 | Dynamo Kiev vs Rennes | 4.31 | 3.61 | 1.78 |
| 19:45 | 3672 | Apollon Limassol vs AZ Alkmaar | 4.10 | 3.65 | 1.81 |
| 19:45 | 3902 | Karabakh vs Olympiakos | 1.78 | 3.70 | 4.20 |
| 19:45 | 3961 | CFR Cluj vs Slavia Prague | 3.44 | 3.44 | 2.09 |
| 19:45 | 3986 | Djurgardens IF vs KAA Gent | 2.95 | 3.35 | 2.31 |
| 19:45 | 4127 | Union Saint Gilloise vs Sporting Braga | 2.29 | 3.40 | 2.95 |
| 19:45 | 4400 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.59 | 3.34 | 2.59 |
| 19:45 | 4939 | AEK Larnaca vs Fenerbahce | 4.20 | 3.65 | 1.79 |
| 19:45 | 5155 | Feyenoord vs Midtjylland | 1.59 | 4.30 | 4.80 |
| 19:45 | 5811 | Austria Vienna vs Villarreal | 5.00 | 4.20 | 1.58 |
| 19:45 | 5822 | Bodo Glimt vs Arsenal | 5.82 | 4.42 | 1.49 |
| 20:00 | 3706 | Mirandes vs Levante | 3.56 | 3.46 | 1.96 |
| 20:00 | 5400 | UD Ibiza Eivissa vs Eibar | 3.12 | 3.17 | 2.25 |
| 20:05 | 5737 | AL Sahel vs Al Jahra | 3.05 | 3.40 | 2.23 |
| 21:00 | 3624 | River Plate (URU) vs Liverpool (URU) | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 22:00 | 1431 | Ludogorets Razgrad vs HJK Helsinki | 1.54 | 4.21 | 5.41 |
| 22:00 | 1482 | Lazio vs Sturm Graz | 1.45 | 4.51 | 6.22 |
| 22:00 | 1726 | Hapoel Beer Sheva vs Lech Poznan | 2.10 | 3.40 | 3.35 |
| 22:00 | 2325 | Real Sociedad vs Sheriff Tiraspol | 1.22 | 6.00 | 12.00 |
| 22:00 | 2345 | FC Vaduz vs SC Dnipro 1 | 3.06 | 3.51 | 2.18 |
| 22:00 | 2363 | PSV Eindhoven vs FC Zurich | 1.22 | 6.38 | 10.97 |
| 22:00 | 2424 | KF Ballkani vs Sivasspor | 2.88 | 3.33 | 2.42 |
| 22:00 | 3044 | Nice vs Slovacko | 1.39 | 4.61 | 7.41 |
| 22:00 | 3272 | Shamrock Rovers vs Molde | 4.88 | 3.89 | 1.64 |
| 22:00 | 3881 | Zalgiris vs Pyunik Yerevan | 2.03 | 3.25 | 3.70 |
| 22:00 | 4605 | West Ham vs Anderlecht | 1.43 | 4.49 | 6.79 |
| 22:00 | 4818 | Union Berlin vs Malmo | 1.34 | 5.01 | 8.01 |
| 22:00 | 5303 | Steaua Bucuresti vs Silkeborg | 2.55 | 3.40 | 2.60 |
| 22:00 | 5639 | Trabzonspor vs Monaco | 3.39 | 3.49 | 2.05 |
| 22:00 | 5702 | Manchester Utd vs Omonia Nicosia | 1.12 | 7.86 | 19.23 |
| 22:00 | 5898 | Ferencvaros TC vs Red Star Belgrade | 2.33 | 3.45 | 2.85 |
| 22:00 | 5965 | Granada vs Sporting Gijon | 1.79 | 3.37 | 4.47 |
| 23:10 | 3177 | Deportes Tolima vs Alianza Petrolera | 1.65 | 3.45 | 4.86 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MANDONGA AJA NA 'NDOIGE' KIDUKU AKIMVAA MUARGENTINA

**Na Sabato Kasika**

BONDIA Karim Mandonga, amekuwa kivutio katika mkutano wa waandishi wa habari ulioitishwa jijini Dar es Salaam jana na Kampuni ya Mo Green International wakati wa kutangaza pambano la bondia Twaha Kiduku anayetarajiwa kumvaa Damian Bonell kutoka Argentina.

Pambano hilo, linatarajiwa kufanyika katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, Novemba 25, mwaka huu huku likitanguliwa na mengine likiwamo la Mandonga na Said Mbelwa, ambao katika mkutano huo wa jana walitambiana kila mmoja akidai kuwa 'atamuua' mwenzake.

"Mandonga mtu kazi, sasa nimekuja na ngumi inaitwa 'ndoige' ninakupiga inapinda kona kumfuata kokote uliko hata ukikimbia, na itaanzia kwa Mbelwa, hivyo ajiandae kwa kipigo, nitampiga kama ameniulia mama yangu," alitamba Mandonga.

Wakati akitamba hivyo, mpinzani wake, Mbelwa alisema atamwomba mkuu wa mkoa wa Morogoro kuleta gari ya kubebea maiti, kwa madai kwamba atapambana na mtu ambaye hana uwezo wa kuhimili masumbwi yake.

"Huyo si mtu kazi kama anavyojiita, bali ni mtu kiazi, hivyo nimuombe mkuu wa mkoa wa Morogoro kuandaa gari la kubeba maiti, kwani atafia Uwanja wa Jamhuri," alisema Mbelwa.

Akizungumzia siku hiyo ya pambano, Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya Mo Green International, Kessa Mwambeleko, aliwataja mabondia wengine watakaotangulia kupanda ulingoni siku hiyo kuwa ni pamoja na Dulla Mbabe dhidi ya Mbiya Kanku kutoka Congo, Said Stops na Juma Pande, George Udongo na Kipaji, Babu Luda dhidi ya Amazing, huku Maozeme akitwangana na Mwaki Sondo.

"Mabondia wengine wa utangulizi ni Ayubu atakayepambana na Imma Mgogo, Edger Kiduku dhidi ya Mchapen, Jenti atavaana na Swed, Msumari atapambana na Magambo, huku Ubingwa Abu akimkabili Damian," alisema Mwambeleko.

Mratibu wa pambano hilo, Killer Boy, alisema kwenye siku hiyo pia kutakuwa na burudani ya muziki wa dansi kutoka Bendi za Waluguru Original, Town Classic na msaani wa Bongo Fleva, Belle 9.

Meneja wa Town Classic Band, Andrew Sekidia, alisema bendi hiyo inamilikiwa na Kampuni ya Mo Green International na kwamba itatambulishwa rasmi kwa waandishi wa habari wiki chache zijazo.




Mratibu wa mapambano ya ngumi, Deo David (katikati), akiwatambulisha mabondia, Karim Mandonga (kushoto) na Selemani Mbelwa, kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuelekea maandalizi ya pambano lao la awali wakati Twaha Kiduku atakapopambana dhidi ya Damian Bonell kutoka Argentina katika Uwanja wa Jamhuri, Morogoro Novemba 25, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga mapema tu yawahi Sudan

INATOKA UK. 32

mchezo wetu ujao na kutimiza malengo, hakuna anayeamini kwamba mchezo utakuwa mwepesi, hilo lipo wazi lakini tunafanya kila kitu kiwe sawa ili tupate ushinda ugenini," alisema Nabi.

## Simba yaishtukia De Agosto

INATOKA UK. 32

sababu yoyote itufanye tukose kufuzu hatua ya makundi," alisema meneja huyo.

Alisema hawatadharau na kuridhika na ushindi wa Angola, hivyo watashuka dimbani kwa tahadhari kubwa na kutowachukulia poa wapinzani wao katika mchezo wa Jumapili.

"Tunaingia kivingine, tunahitaji kufuzu...tunaenda kucheza mchezo huu kana kwamba hatujacheza mechi ya awali, tumekumbuka kucheza makundi Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Lazima tuwe makini, lakini kuna taarifa njema kwa mashabiki wetu kurejea kikosini kwa Peter Banda, amefanya mazoezi na atakuwa sehemu ya mchezo wa Jumapili, kuhusu Shomari Kapombe anaendelea kufanya mazoezi hospitali, baada ya De Agosto atakuwa vizuri na kuanza kuonekana mechi za Ligi Kuu," alisema Ahmed.

Alisema wageni wao wanatarajiwa kuingia nchini Ijumaa mchana pamoja na waamuzi wanaotokea Afrika Kusini huku kamishna wa mchezo akitarajiwa kutua leo.

"Alhamisi tukiwa na hamasa katika Uwanja wa Mo Simba Arena, hapo mashabiki watapata nafasi ya kuona timu ikifanya mazoezi na siku ya Jumapili kutakuwa na burudani uwanjani kabla ya mchezo na kila shabiki atapewa bendera kwa ajili ya kuhakikisha wanapepeRusha uwanjani wakati tunampelekea pumzi ya moto De Agosto," alisema.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 13, 2022

Nipashe




UKURASA 31

**Mandonga aja na 'ndoige akitishia kuua'**

# SIMBA SC YAISHTUKIA DE AGOSTO, BANDA AREJEA

## ●●●Yawataja Jwaneng Galaxy FC, yawahi kambini, burudani kutawala kwa Mkapa Jumapili...

**Na Saada Akida**

HUKU winga hatari wa Simba, Peter Banda, akirejea rasmi na kuungana na wenzake kikosini akitoka chumba cha majeruhi, uongozi wa klabu hiyo umewashtukia wapinzani wao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Primeiro de Agosto na kuwataka wachezaji kuingia kambini mara moja kuepuka yasije yakawakuta ya msimu uliopita dhidi ya Jwaneng Galaxy FC ya Botswana.

Katika hatua kama hiyo ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy, huku wakiamini wamemaliza kazi na kilichobaki ni kukamilisha tu ratiba nyumbani, mechi ya marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa wakaachwa mdomo wazi baada ya kubugizwa 3-1 na timu hiyo ya Botswana kutinga hatua ya makundi.

Tayari Simba hadi sasa ina ushindi wa mabao 3-1 iliyoupata ugenini nchini Angola dhidi ya Primeiro de Agosto, hivyo mechi ya marudiano Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Mkapa, inahitaji sare yoyote ama kutokubali kufungwa zaidi ya mabao 2-0 ili kufuzu hatua ya makundi, jambo ambalo uongozi unaepuka kujiaminisha kwamba wamemaliza kazi.

Hivyo, kuelekea mchezo huo kikosi cha Simba kimeingia kambini baada ya mazoezi ya jana jioni ili kujiandaa vema kwa mechi hiyo itakayopigwa Jumapili majira ya saa 10 alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema maandalizi yameanza rasmi jana katika Uwanja wa Mo Arena kujiandaa dhidi ya De Agosto, kuhakikisha wanapata ushindi ili kufuzu kucheza hatua ya makundi.

Alisema wameshinda ugenini lakini hawajafuzu na wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kucheza hatua ya makundi na baada ya hapo kusonga mbele zaidi.

"Ushindi wetu ugenini dhidi ya De Agosto umetukumbusha msimu uliopita tuliopotolewa katika hatua hii ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi Jwaneng Galaxy.

"Mechi hiyo inatukumbusha msimu uliopita hatutaki kurudia makosa hayo, tumeshinda bao 3-1 ugenini, haijatufurahishwa kwa sababu imetukumbusha msimu uliopita, sasa tunaenda kama hatukucheza mechi ya kwanza," alisema Ahmed.

Alisema kiwango walichokionyesha dakika za mwisho zimewashtua na wanatolea macho kweli mechi hiyo kwa kupambana na kuhitaji kufuzu kwa matokeo mazuri mengine na si kutegemea yale ya Angola.

Ahmed alisema baada ya mapumziko ya siku moja waliyopewa wachezaji waliporudi kutoka Angola walianza mazoezi na jana jioni waliingia kambini moja kwa moja.

"Tumejipanga kuingia katika mchezo wa Jumapili bila kuangalia matokeo mazuri ya mechi ya kwanza, hatutaki kwa

INAENDELEA UK. 31



Winga wa Simba, Peter Banda

## Yanga mapema tu wawahi Sudan

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha hawafanyi makosa kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan, baadhi ya watu akiwamo Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, wametangulia nchini humo kwa ajili ya kuweka mazingira sawa ili kuepuka hujuma, imeelezwa.

Yanga ambayo inatarajia kutua nchini Sudan Jumamosi wiki hii na kesho yake kushuka dimbani kuwavaa wapinzani wao hao, katika mechi ya awali Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ililazimishwa sare ya bao 1-1, hivyo inahitaji ushindi wowote ama sare ya kuanzia mabao mawili ili kutinga hatua ya makundi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wamesikia kauli ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, na wanaifanyia kazi kwa lengo la kutafuta ushindi katika mechi hiyo ya marudiano.

Alisema malengo makubwa waliyojiwekea ni kuhakikisha msimu huu wanafanya vizuri katika mechi za awali na kwenda hatua ya makundi kitu ambacho wanalazimika kushinda ugenini dhidi ya Al Hilal ili kutimiza azma hiyo.

"Mashabiki wanapenda kuona timu yao inafanya vizuri, tumesika kauli ya waziri (Mchengerwa), uongozi umefanya maandalizi, benchi la ufundi na wachezaji wanaendelea kujiimarisha na tuko tayari kwa ajili ya kwenda kupambana kupata matokeo mazuri ugenini," alisema Hersi.

Alisema malengo yao makubwa ni kuona timu hiyo inacheza hatua ya makundi na anaimani kubwa Jumatatu wataamka Yanga ikiwa imeingia hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa upande wa Kocha Nabi, alisema maandalizi wanayofanyia kazi ni mapungufu waliyoyabaini katika kila safu ikiwamo ulinzi na ushambuliaji, kujilinda kusaidiana katika kushambulia.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa na mikakati inapangwa kuelekea mchezo huo kwa sababu kila mmoja wao anahitaji kupata ushndi ili kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo.

"Tumepata sare nyumbani mechi ya kwanza haina maana tumeondolewa, bado tuna nafasi ya kufanya vizuri katika dakika 90 za kipindi cha pili, tunaendelea na mipango yetu ya kuandaa kikosi kutafuta matokeo mazuri nchini Sudan.

"Bado tuna nafasi ya kufanya vizuri

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >